Maswali na majibu 131 ya malezi

# Maswali na majibu 131 ya malezi

MaarifaMtandaoni.com
RohoYaUnabii.Org

# MASWALI   NA MAJIBU 131 YA MALEZI

MaarifaMtandaoni. Com
Jersey 2012, 1st Edition, 2026, 2nd Edition
Grace Momadi-Masaka Jersey, Marekani

MASWALI NA MAJIBU YA WAZAZI (mifano )--------------------Uk 16

**WAANDISHI, WAHARIRI, WASHAURI**
**Grace   Momadi-Masaka-Jersey, Marekani**
**Daniel Masaka-Kisii, Kenya**
**Bettie Magesa -Muasya-Nairobi, Kenya**
**Suzana Nyakrere-Rorya, Tanzania**
**Stephen Letta-Masasi, Tanzania**
**Kwandu Kasiri-Kibaha, Tanzania**
**Mbusi Mpagalushu-Bariadi, Tanzania**
**Innocent Wayoga-Dar-Es-Salaam, Tanzania**
**Maggie Nenge-Mwanza, Tanzania**

**UTANGULIZI**

Mpendwa msomaji kwa kumalizia, tumeona maswali ni mengi tuliyoulizwa katika semina za malezi, hivyo email address yetu ni masakamomadi@aol.com au jambomuhimubooks@gmail.com

Baada ya kutembea muda mrefu na kukosa vitabu vya Kiswahili vya malezi ya watoto mtandaoni. Tuliona tuandike kitabu, si kwa vile tuna utaalamu sana, la hasha bali kwa vile tuliona kwamba hakuna ambaye ni mtaalamu wa kulea. Kila mtu ana mizoga yake! Ni Mungu tu ambaye ndiye Mzazi mtaalamu na MWEZA. Zamani mashangazi, mabibi walisaidia, ila siku hizi hata wao waonyesha mmomonyoko wa malezi kwa vile hawajapata maarifa hayo yaliyotolewa kwenye jamii zetu za zamani. Uvumilivu wetu wazazi unazidi kupungua jinsi dunia inavyoendelea, wiki hii nilisoma gazeti na kuona mama aliyemwambia mtoto wake wa miaka saba asinywe maji kwa vile anakojoa kitandani! Mtoto huyu alikufa kwa kuishiwa maji, madaktari walipompima walikuta hana maji. Walimlinganisha na pacha wake wakakuta ni kweli. Wazazi tunajitia bize kweli kweli hata sijui tulizaa kwa ajili gani na tuko bize hivi, tukiwapa wengine kutunza watoto wetu. Kumfundisha mtoto kutawala nafsi, kujikana nafsi, huduma, kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu, utii na kazi ni mambo makuu na ya muhimu sana. Katika kitabu cha Nabii Musam cha Kumbukumbu ya torati asema, "Mwana akiwa mlafi na asiyetii, waitwe wazee na apigwe mawe auawe. Yaonekana jambo hili ni zito sana mbele za Mungu, yaani kutokuwa na kiasi na kutotii.

Mara nyingi mtoto akiwa ni mbaraka si kwamba wazazi wamebahatisha! Bali mara nyingi ni neema za Mungu na kazi waliyoifanya. "Nawapenda wale wanaonipenda, na wale wanitafutao mapema wataniona." Methali 8:17. Anza malezi mema mapema, mtoto akifika miaka mitatu tabia imejengeka, na miaka sita, tabia inakuwa imekamilika! Ila kama umekosea mahali, kama sisi, mwombe Mungu maana ni mwenye rehema akufanyie miujiza kubadilisha tabia mbovu. Pia usisite kuwaomba wengine msaada ambao wana upendo na wanamjali Mungu mara zingine mtoto amsikia mwingine kwa Njia zile anazotumia, ila katika yote Mwombe Mungu sana. Uzazi si kazi ndogo kwani nimegundua uzazi definition yake ni mwenye dhambi mmoja anamkuza na kumlea mwenye dhambi mwingine! Sote tumefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Ila Mungu anatupenda sana, na anatasa tufanikiwe, na ana ahadi zaidi ya 10,000 kwenye Neno Lake*, na kati ya hizo 265+ zasema "Usiogope". Nina changamoto nyingi kama mzazi, nimeshakosea

mengi sana ila leo nasikia neno "usiogope". Nashuka magotini saa hii na kumwomba Mungu anipe nguvu, nishinde siku moja nitakapoulizwa "wapi kundi lako dogo nililokupa" niseme ni hawa kwa Neema ya Mungu tu na si nguvu zangu masikini. [Angalia Biblia ya Ahadi kwenye MaarifaMtandaoni.Com ili kusoma Biblia iliyopigiwa mistari ahadi za Mungu, na Maneno Mungu aliyotamka kwa Kiswahili- Promise Bible and Red-lettered Bible]

Kama mtume Paulo anavyosema, "Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kutii;" Warumi 8:7. Ni mapambano siku zote, kuwa na tabia njema ya mbinguni! Mambo ya dunia yalivyojiseti, au mkao wake ni kukuharibia malezi ya mtoto. Kila siku omba Mungu na kuendelea na vita. Hakuna mbabe wa shule hii awe China, Tanzania au Urusi! Hata Kaini alimwua ndugu yake Abel kabla ya televisheni. Angalia maisha ya Nadab, Abihu, Absalom, na wengine ambao wazazi wao walikuwa wazee wa imani. Usiogope, hata sisi tungeogopa tusingeandika, kwani hatuna uzoefu wala ushindi wowote. Tumejitosa tu! Mama mmoja alimkatisha tamaa mwenzake "Watoto wako ni wabaya sana utawasaidiaje watu nawe yako yakushinda!". Hii si kweli kwani uzoefu ni msaada au daraja la wengine kupitia pale tulipokosea, na pia kuna wajukuu Mungu akitujalia. Pale tulipokosea kwa watoto bado kuna watoto katika jumuiya tunaweza kusaidia tukipata maarifa mazuri ya malezi toka kwa Baba wa mbinguni. Tunadai lile Fungu la "kuangusha mawazo yetu "1Kor 10:5.

Mtoto mchanga uliye naye mkononi si malaika ila mtenda dhambi kama binadamu wote. Kila mtoto anayezaliwa ni mdhambi, mpaka aongoke na kumkiri Bwana kuwa Mwokozi wake. Ni wewe wa kumleta kwa Mungu na kumlea katika kicho cha Mungu. Usiwe na roho ya malalamiko na manung'uniko. Hayo yaliwafanya Waisrael wafie jangwani wote, kasoro wawili. Mungu hajibu manung'uniko, bali hujibu maombi. Neno kubwa ni kumfundisha mtoto wako aweze kuishi bila wewe. Aweze kumtegemea Mungu na kuwa mtii, endapo upo au haupo. Aweze kujikana nafsi, na kujitafutie riziki, na kumudu maisha yake endapo upo au haupo.

Jaribu kuepuka kukaa mijini, ni pabaya kulelea watoto. Yalimpata Lutu japo Petro alisema alikuwa mtu wa haki, kwa kukaa mjini alipoteza watoto na mke. Tusome ile ngazi Ambayo Petro anaisema…. nukuu. Pengine Nuhu alikaa mashambani, yeye aliokoa jamaa yake. Miji ina majaribu ni mengi, japo ina mashule, maduka na huduma, ina mengi mabaya zaidi. Vijiji vya ujamaa vilikuwa na shida hii ya kuleta vijana wengi pamoja wasio na shughuli, ila kupeana utalaam wa uovu. Wanasema kujenga tabia kijijini ni mara kumi bora kuliko mijini.

Twaona Isaka na utii wake, japo alikuwa kijana mwenye nguvu kumshinda baba alitii kutolewa dhabihu na baba yake Ibrahimu. Watoto wengi wakorofi wameharibu ndoa za wazazi wao na wale ambao wana tabia njema wamejenga ndoa za familia zao. Angalia maisha ya Yakobo na Esau yalivyotenganisha wazazi wao. Hata na wazazi walifanya kosa la kupendelea watoto, nayo ikawa sumu kubwa. Rebeka aliharibu mambo hapa. Kina mama, "Mvuto wa mama na maombi una nguvu nyingi."

Angalia maombi na kazi ya mama Musa, na jinsi Musa alivyokuwa jemedari na kiongozi wa kiroho. Wakina mama tusijiachie, hakuna kazi ya muhimu kuliko hii ya kumsaidia mtoto kuwepo mbinguni siku moja.

Mama lazima awe na kiasi, kutawala nafsi na kujikana nafsi. Vita vikubwa ni vya kushindana na nafsi (battle of self). Nafsi ife, au yule mtu wa kale atokomee. Mama wote wa wanadhiri waliambiwa wafanye mambo fulani; kama kutokunywa pombe n.k. Tunaona Hana, mama ya Samuel alitaka kumtunza mtoto amtumikie Mungu. Wazazi wengi tunataka kumlea mtoto atutumikie sisi! Mungu anapendezwa na maombi yasiyo na uchoyo au ubinafsi. Anza kuomba hayo leo. Ombea na watoto wa wenzio na kuwasaidia mashauri bora ya uzima. Wokovu ni kazi ya Roho wa Mungu bali kuwaambia wengine habari Njema ni kazi ya kila kiumbe. Ondoa chuki, ili mtoto asione una uadui na mtu naye ajifunze kupenda na kuwa bora. Adui angalia mazuri yake ana mengi, hata ni kwa adui ndiyo utapata ukweli na kujikakamua kusonga mbele.

Ndoa ya Hana na Elkana na nyingine zaonyesha mitara ni mibaya mno kwa ndoa na matunzo ya mtoto! Katu, siyo mpango wa Mungu! Hana alilea mtoto kwa miaka pungufu ya sita na mtoto akakumbuka yale mafunzo, na kuwa jemedari wa kumtetea Mungu. Katika kitabu cha Danieli, tunaona Danieli, Mishael, Anania na Azaria walikuwa vijana wadogo, ila waliweza kushinda majaribu makubwa walipotekwa. Walijifunza haya wapi? Si utumwani, bali nyumbani walifunzwa kiasi, kujikana nafsi, na kuepuka tamaa. Mama zao waliwafundisha kutokula ovyo ovyo.

Hata Kristo, mwalimu wake wa kwanza aliyekuwa binadamu alikuwa mama yake. Hakwenda mashule ya marabi kujifunza! Mzazi ndiyo mwalimu wa kwanza. Alijifunza kwa kuishi maisha magumu, ya kufanya kazi, akijikana nafsi. Na ndiyo maana ni muhimu mtoto akae nyumbani na kufundishwa mpaka afike umri wa miaka minane hadi kumi hivi. Hata hivyo shule nyingi zina watoto wengi darasa

moja, na nilitembea pengi ambapo watoto hata wa darasa la tatu hawajui kusoma. Shule moja mvomero, ilisemekana ina mwalimu mmoja na watoto mia saba! Mama asiyeenda shule ila anajua kusoma, atamfundisha mtoto wake kujua kusoma akiwa na kitabu kwa miezi michache tu! Atamshinda mwalimu mwenye watoto mia moja darasani, kwani yeye ana mmoja!

Twaona Mariamu na Yusuf kwa kutoangalia mtoto kwa siku moja, walipotelewa na mtoto Kristo, na ilichukua siku tano kumpata. Hata nasi wazazi kwa kupuuza, kupiga masoga na watu, au kutosali twaweza kupoteza watoto wetu na kumpoteza Mungu katika maisha yetu. Usiogope kazi ngumu ya kulea hata kumtelekeza mtoto kwa jamaa, ni bora kuwa na mtoto mmoja na kumshugulikia kuliko kupeleka watoto wako kwa wengine ambao hawathamini mambo unayothamini. Usiwekeshe watoto kwa ndugu na jamaa, labda iwe dharura. Ni wakati wa kupanga kuwa na watoto wachache tutakaomudu kuwalea.

Siku hizi ni ngumu, si za kuwekeza watoto kwa mjomba au shangazi. Mzazi mmoja alilalamika kwamba alimweka mtoto kwa mjomba na akamfundisha ulevi. Mababu na mabibi pia japo wanasaidia, ila usitoe uongozi wako kwao, maana wao wanadekeza watoto au hawana makini ya kutosha kushugulikia watoto. Tunarudia,Iwe dharura tu kumwekeza mtoto wako kwa watu hapa na pale.

Kuna wengine hawataki kutunza watoto, aidha, walipata mimba bila kutarajia. Kwa hawa nashauri watafute njia ya kuwapa wazazi ambao watamtunza mtoto huyu vizuri. Usifikirie kumwua mtoto kwa njia yoyote. Yeye ni kiumbe kamili, hata kutoa mimba iwe mwiko. Mtoto si mnyoo ambao tunatoa ndani ya tumbo. Tabia hii imejengeka pengi. Nchi kama ya Marekani wanawake milioni nne hutoa mimba kila mwaka!

Wazazi tutaulizwa hukumuni tulivyolea watoto wetu. Watu wakikusaidia ni bonasi isiwe sehemu ya programu yako! Hata hivyo ukiwa mzee kama uliacha watoto wako walelewe na wengine muda wote itakuwa vigumu kukusaidia maana umekuwa kama mpita njia.

Wale wenye wasaidizi nyumbani muwe waangalifu, kwani tumesikia mengi. Mfano dreva aliyeingia katika uhusiano wa kimapenzi na binti aliyekuwa anampeleka shuleni. Yaya aliyemweka mtoto mchanga kwenye oven na kumwua kwa sababu tajiri alimgombeza. Mayaya wanaowafanya wavulana wadogo kuwa

waume zao, au yaya aliyetumia mswaki wa mtoto na kumpa mtoto ukimwi na kadhalika.

Kuna wazazi wengi wanaotesa mayaya na watenda kazi pia na hiyo ni maada nyingine ya kuzungumzia. Kama unaona kwamba kazi yao haikuridhishi, kuliko kuwatesa, fanya mwenyewe majukumu yako ili usisigane na watu. Pale inapobidi uwe nao, lazima kuwafundisha vizuri (train) ili wajue cha kuwalea vizuri, si kuwapa Chakula na kufua nguo zao tu, bali kuwasaidia kihisia na kitabia na hata kiroho pia. Watathmini, na kuzungumza nao mara kwa mara kama mwajiri wa ofisini. Yaya asiyeweza kusoma na watoto neno la Mungu, ikiwa unaenda siku nzima, itakuwa ni shida. Wazungu wengi wakiajiri yaya wanauliza mambo mengi, kama vile anajua kusoma na kuandika, amefika darasa la kumi na mbili, anaweza kumsaidia mtoto kiafya akizidiwa, anaweza kuamua magomvi ya watoto, anaweza kuwafundisha watoto mambo ya taaluma n.k. kama una uwezo usichukue mtu tu, eti ni bei rahisi kumlipa, wakati Ambayo una uwezo wa kumlipa hata Yule aliyesomea ualimu na akakosa kazi akusaidie mengi zaidi. Au ukapata mwenye uzoefu wa kufundisha watoto mengi, na japo utamlipa zaidi watoto Wako watapata mengi zaidi.

Ni muhimu mzazi aseme na kueleweka asiache maswali fulani, ndiyo iwe ndiyo, na siyo, siyo (ambiguity). Lazima nyumba iwe na kanuni za kufuata, na mikutano ya familia na watoto pengine kila wiki au mwezi. Mzazi asiogope kufuata sheria akiona atamkasirisha mtoto. Eli kuhani alijua ubaya watoto wake. ila hakuwakataza kufanya kazi ya hekaluni, waliendelea kuifanya. Aliona atawakosea au aliwaogopa. Alisikia malalamiko ya watu, ila pengine alipenda watoto sana na kuona watu wanamsakama na watoto wake.

Kutoka udogo mtoto afundishwe kuheshimu neno la mzazi. Wazazi wengi wanafikiri mtoto ni mdogo sana hawezi kusikia maagizo! Muda ukishaenda unakuwa umepoteza mvuto. Mtoto aliyezaliwa tu anaanza kufundishwa, mfano, kutokula ovyo ovyo, ale baada ya masaa matatu n.k. Wazazi wengi waliokua katika hali ya umasikini au shida wanafikiri kwamba watawalea watoto wao' ili wasipate shida kama wao. Wanawaacha kufuja vitu, na kufanya watakavyo. Jambo la kusikitisha ni kwamba watoto hawa ambao hawajapata shida wanashindwa kuishi na watu au wanaingia magenge mabovu ya uvutaji au tabia nyingine za uovu.

Wazazi wanapaswa kujua kwamba utajiri wao waliupata kwa sababu ya nidhamu na kazi ngumu. Watoto waliokuta vitu tayari kama vile majumba, magari na mashamba imekuwa si mbaraka kwao. Mara nyingi wanaingia majaribu ya

shetani kwa namna moja au nyingine. Yaweza usione vizuri, ila ukiangalia kanuni za mbingu utaona mashimo. Chunguza maisha ya wale ambao wamekuwa mbaraka kwa wengine na kuwa majemedari kwa mambo fulani, utakuta maisha yao yalikuwa na kanuni, kujikana nafsi, na kazi nyingi ngumu kama kukamua ng'ombe au kulima saa kumi na moja asubuhi na kadhalika.

Watoto wengi pia wamelelewa bila baba. Nchi ya Marekani ni asilimia hamsini. Jambo hili ni gumu katika tabia na malezi ya mtoto. Ni masikitiko; kama Charles Spurgeon alivyosema kwamba wazazi wengi hata wanaompenda Mungu, wanafurahi tu pale mtoto wao anapokuwa na akili darasani hata kama hamjui Mungu. Je watoto wetu wana vitabu vya Neno la Mungu na wanavisoma?

Masomo ya darasani ni mazuri ila sijawahi kusikia mtu aliyesema, "Hesabu imenifanya nisiwe mwizi," au "Jiografia imenifanya nisiwe mwongo au mwasherati." Ni neno la Mungu tu, ndilo lina nguvu ya kubadilisha tabia. Tunakaza kwa kurudia, ni NENO TU LA MUNGU linasaidia tabia. Filosofia za watu hazifui dafu.

Wazazi wengi wanahakikisha watoto wana mabegi makubwa yenye vitabu vya shule wakienda asubuhi, ila hawajali kama watoto wana Neno la Mungu na wanalisoma au wanabadilishwa nalo katika maisha yao. Watoto wetu waendapo ibadani wawe na penseli au peni na Neno la Mungu angalia wimbo ambao umeimbwa na TotoEtu 'Begi langu la Kanisani. Darasani wakienda bila vitabu itakuwaje? Tunakazana waende na nguo nzuri kwenye ibada ila bila Neno la Mungu itasaidia nini? Je, wanasoma masomo yao ya lesoni? Kama una pesa za vocha za simu na kujisumbua na "halo, halo;" siku nzima, basi una pesa ya kuwanunulia watoto wako neno la Mungu.

Tunaagiza jamaa zetu wa mijini watuletee vitu vingi, kwanini wasituletee Kitabu kikuu pia? Agiza vitabu vya nyimbo za kuabudu ili watoto waimbe, wakariri mafungu ya Neno la Mungu kila siku. Huo ndio urithi bora utakaowapa, si majumba na mashamba. Shughulika nao sasa, kuna siku watasikiliza marafiki zao kuliko wewe, na utakuwa umechelewa. Utaonekana kwamba umepitwa na wakati, (old fasheni au zilipendwa). Ikiwa runinga ni shida itupe. Nilipata shida na watoto wangu walipokuwa wanaangalia runinga, wakakosa adabu kabisa! Ukiwaita hawaitiki, ukiwauliza swali hawajibu. Mawazo yao yametekwa kabisa, wanakodolea runinga macho na wanapigwa na butwaa kwa wanayoyaona na kuyasikia! Runinga amekuwa kimungu au msukule fulani (hyponotic).

Mtoto mmoja Nairobi, aliyekuwa na mikanda ya ponografia; alikuja nayo shuleni na kuwapa watoto wengine. Iliposhikwa, mama alikana, "Mnamsingizia mtoto wangu, hawezi kufanya vile nyumbani kwangu! Ni mtoto mwema." Mtoto akaitwa mbele ya mama, na kuulizwa, akakiri kwamba amekuwa akiangalia nyumbani mikanda hiyo nyumbani, wakati mama hayupo!

Kina mama msitetee watoto, tabia inajengwa wakati wowote na popote. Wakina mama wengi wamekuwa adui wa kwanza wa watoto wao kwa kutetea uovu. Uwe kibaruani usiku na mchana. Wafanye watoto wako wawe marafiki wa karibu ili mambo yakiharibika wakwambie. Mzazi ndiyo kiongozi si mtoto. angalia mtoto anayofanya na umwelekeze. Umpe uhuru pole pole kutokana na vile anavyokabili majukumu yake. Mtoto asikae kivivu bila kazi ya la kufanya. Kusali asubuhi na jioni na watoto ni muhimu.

Ni sehemu yetu kama waumini wa Mungu. Kukosa kutelekeleza wajibu ni dhambi. Lazima kuwe na kanuni ili kujenga tabia (regularity). Wakati wa kulala, kula, kuomba, kucheza, yahitaji uvumilivu na uendelevu (consistency). Kiasi na kujikana nafsi inatokana na maisha yenye mpangilio (order). Usifanye ratiba ya mtoto kuwa holela.

Mama mmoja na mume wake wenye watoto katika shule ya msingi na sekondari walijivinjari na marafiki na ndugu kila siku kuanzia saa kumi jioni, wakitoka kibaruani mpaka saa mbili usiku. Walifika kwetu karibu kila siku, wakifanya mazoezi pamoja na kutembelea majumba ya watu kwa minuso wakati wa chakula. Watoto wao walikuwa wakijikuza wenyewe. Mwanamke mmoja ambaye alikuwa hajawahi kuolewa au kuzaa, aliwaona akashangaa walipotoka. Akaniuliza, "Hivi huyu mwanamke anatembea na bwana saa zote akimchunga, badala ya kuchunga watoto!"

Usiache watoto wajikuze wenyewe. To a child is folly alisema Sulemani; (mtoto ana ujinga mwingi kwa tafsiri nyingine). Usiache mtoto kwa muda kila siku unaenda mahali.

Maisha ya Yohana mbatizaji yanaonyesha kwamba japo wazazi walimpata uzeeni kabisa hawakumdekeza. Aliishi mashambani na kufanya kazi mahali ambapo majaribu yalikuwa machache. Japo alikuwa wa ukoo wa kifalme na ukuhani, uvivu haukuwa sehemu yake!

Mara nyingi wazazi wengi tunakazana na matendo ya nje tunayoyaona, na si matengenezo ya moyo. Hili ni kosa kubwa. Watafanya ya kutufurahisha ili wasiadhibiwe, ila mioyo yao haijabadilika. Jaribu kufanya mabadiliko ya moyo, akili na nia ya ndani, yale matendo ya nje yatakuwa rahisi. Yusufu alifundishwa asiwe mzinzi akiwa mdogo. Yeye hakuwa jitu. Hata alipokuwa mwenyewe Misri alimkimbia mwanamke aliyemshika kwa nguvu, huku amefunga taulo, akasema "Nimfanyiaje Mungu ubaya kama huu?" Ila Samson aliyekuwa Raisi na jitu lenye nguvu nyingi alishindwa jaribu hili akaanguka kwenye uasherati. Ilikuwa rahisi yeye kutumia nguvu zake kumpiga konde mwanamke na kumtupa mbali hata kumzuia asimfuate! Hapa pia ni nafasi ya kufundisha watoto wetu wa kike katika ulimwengu wa leo, kuwa na kiasi na tabia bora. Watoto wetu wengine wasichana siku hizi wanakimbiza wanaume, na kupunguza hadhi yao kama mke wa Potifa badala ya wanaume kuwatafuta. Watoto wetu wapaswa kujistahi, na kuwa na uungwana hii itawasaidia kupata wachumba na waume bora, kuliko kujipeleka au kuonyesha tabia ya ukahaba. Sisemi kwamba wakati wote wachumba ndiyo waje kwao kutawatafuta, kwamba hawana usemi kabisa kwa yule wanayempenda, bali wafanye haya kwa hekima na kujistahi, bila ya kujionyesha "chema chajiuza, kibaya chajitembeza". Na hata sisi wakina mama tulioolewa kama mke wa potifa, hebu na tujisitiri na kuepukana na uasherati, zamani wanaume ndiyo walijulikana kw.a tabia hii mbovu, siku hizi baada ya sisi kupata vibarua na kwenda shule tumeingia katika uovu huu pia, na haya ni mafundisho mabaya mno kwa binti zetu.

Kila siku wapanda mbegu bustani ya mtoto. Yeye haangalii sana vile unavyosema, maana hayo ni maneno tu, anangalia vile unavyoishi. Je, unajua? Unasema yale unayowaza, ila unaishi yale unayoamini! Saidia watoto katika jumuiya yako pia wakiharibikiwa nawe umeharibikiwa. Watakuja kwako na kukuibia, au kukupiga.

Uwe tayari kadiri ya uwezo wako kunyoosha mkono wako kusaidia wengine, "Amhurumiaye masikini humkopesha Bwana naye atamlipa kwa tendo lake jema. Je, umeshawahi kumkopesha tajiri mkubwa kama vile Bill Gates? Au Rais wa nchi yako? Basi hapa unamkopesha MWENYEZI MUNGU mwenyewe! Nikisikia fungu hili natetemeka. Mimi Kinyangarika nimkopeshe BWANA WA MAJESHI WA MBINGUNI kweli? Mungu ambaye wataalamu sasa wanasema kuna sayari zaidi ya trilioni alizoumba! Mimi ndiye namkopesha? Nimepata mawazo mazito kila naposoma hili fungu.

Kwenye vituo vya ibada, wawepo mama na baba wa imani wa kusaidia watoto ambao hawana wa kuwaelekeza vizuri, watoto wengi wanazaliwa katika mazingira magumu, mfano, na wakina mama ambao ni watoto pia, wasiokuwa na maarifa n.k. wengine hata uvumilivu unakuwa mgumu katika kuwafundisha watoto.

Usifurahie moyoni mwako uonapo mtoto wa mwenzako anaharibikiwa; ni kama kufurahi wakati mgonjwa ni mahututi kwenye hospitali hata ICU (Intensive Care Unit). Mara nyingi tukiwa na mwenzetu mgonjwa tunasikitika na kwenda kumtazama hata kupelekea chakula. Je, umeshawahi kwenda kwa mgonjwa mahututi na kuanza kumcheka akiwa pale kitandani kwenye hospitali? Nafikiri utaonekana una wazimu. Nilimsikia mama mmoja akimng'akia mwenzake, alipomwambia shida ya mtoto wake, "Wewe unasema mtoto wako atakuwa mbaya zaidi ya wa kwangu?" Roho ya maneno ya jazba kama haya ni ya ibilisi. Omba msamaha na msaada ikutoke.

Tumeona Ibilisi aliua watoto wadogo wa kiume kwa kumtumia Herode na Farao kwenye Neno la Mungu. Na hata leo anataka aue watoto wa kiume. Baadhi ya Vijana wetu wa kiume wamekuwa wakijiunga kwenye makundi ya tabia mbovu. Wengine hawataki kwenda shule hata wale ambao wazazi wao wana uwezo wa kuwasomesha. Hawataki kwenda ibadani. Asilimia sabini ya walio katika nyumba za ibada ni wanawake. Wakina Baba mtusaidie na hili. Nimeona wakina baba wengi wanapenda watoto wao na wake waende ibadani ila wao wanakaa nyumbani!

Baba jitahidi jinsi ya kumsaidia mtoto wako wa kiume akue katika mazingira bora, apate ustadi ili aweze kukabiliana na mahitaji ya familia, na zaidi ya yote aweze kuwa kuhani nyumbani mwake ili siku moja aingie Paradiso. Hili ni jambo kubwa mno. Maisha yetu duniani yana maana tu kama tunajitayarisha kupata uzima wa milele mbinguni, zaidi ya hapo ni kupoteza muda, maana sidhani kama kuna mtu anapanga kuungua katika ziwa la moto, kupiga mayowe na kusaga meno. Japo neno la Mungu linazungumzia upendo wake, ila kuna siku ya hukumu Ufunuo 1:7. Na ni vizuri tuelewe hilo kwa undani kwamba ni Mwenye rehema ila pia ni Mwenye haki. Itakuwa mbaya sana endapo watu wabaya waende mbinguni. Je, ungependa kukaa karibu na mwizi asiyeacha hiyo tabia mbinguni? Ila Nahumu 1:9 yasema, "Atakomesha kabisa, mateso na dhambi haitainuka tena mara ya pili."

Wazazi tuanze kuweka mkazo jinsi ya kuwasaidia watoto wetu wa kiume, wana majaribu mengi nje ya nyumbani, kama Samsoni Mnadhiri. Japo wazazi wake

waliuliza, "Tumtunzaje huyu mtoto;" na wakaambiwa; Samson alizidiwa nguvu na msukumo wa rika na marafiki.

Baba wengi walio na mabinti watulivu waliosoma, wanasema wanaogopa kwamba wanaume waungwana wa kuoa watoto wao wamepungua. Mmoja aliniambia, "Binti yangu anakutana na vijana wasio na tasnia yoyote, wanaotaka mtu wa kuoa na akae kama kupe." Uwe muwazi kwa mtoto wa kiume kuhusu majukumu yake, na upate maarifa ya hii shughuli. Hakuna mwongozo waliokuja nao kutoka tumboni wa maarifa ya kuwatunza (parenting manual).

Tuwalete watoto wetu kwa Mungu kwa njia ya maombi, na kisha tuwatambulishe kwake. Tuwafundishe jinsi ya kutatua matatizo, hatuwezi tukawatatulia matatizo yao lazima wajifunze nyenzo za kutatua. Kwa kawaida baba anazungumza na mtoto wake dakika tisa Marekani na mama dakika ishirini na nne hivi. Nafikiri kwa vile hakuna mayaya, mababa wengi hutumia muda na watoto wao Marekani kuliko Afrika.

Wazazi tufundishe watoto watu kusamehe, na kujisamehe. Mungu anatusamehe kila siku. Katika Neno la Mungu tunaona dhambi iliingia duniani kupitia wazazi wetu Adamu na Hawa, waliambiwa wafanye kafara, ikiwa kama kielelezo cha Kafara yake Mungu kubwa ambayo ilikuwa inakuja. Kutosamehe kumeleta maumivu mengi kwenye familia nyingi, mtoto aelezwe somo la kusamehe, kufuta hasira na kutoa visasi. Kutosamehe ni kama kunywa sumu na kufikiri yule aliyetukosea atakufa. Kusamehe kunatufanya sisi tuwe huru na kuwa ukurasa mmoja na Mungu wetu. Tunaambiwa tusiposamehe wengine nasi hatutasamehewa. Mungu ndiye anayetuwezesha tusamehe watu, hivyo mtoto amwombe Mungu "ahadi zako za Kweli, umesema tusamehe, ni vigumu kwangu, naomba unisaidie nisamehe". Kujisamehe pia ni muhimu sana ili tuondokane na hatia, Mungu anatusamehe dhambi zetu zote, hata iwe ya aina gani, nasi tuwe tayari kujisamehe.

Kazi ni muhimu. Ijapokuwa mtoto anaona mfano wako hata katika kazi, ni lazima pia kumfundisha, kukagua kazi yake na kumtia moyo. Angalia website (401 ways to get your child working) na doorpost.com. Wazazi wengi hawatumii 'kutia moyo' kama nyenzo moja muhimu. Mtoto analaumiwa na kutukanwa bila mzazi kutambua alichofanya. Mzazi anaacha makovu ya huzuni kwa mtoto. wengine wanakejeli watoto wao. Mtu mzima unapokejeli watoto, inaonyesha kutopevuka (immaturity). Mtoto ni mtoto tu, usiwe kila mara unamkatisha tamaa.

Watu wa nchi za magharibi ambao wampenda Mungu wanasoma na kujifunza mbinu za kulea kwenye neno la Mungu toka kwa waandishi mbalimbali. Najua utamaduni wa kusoma ni mdogo nyumbani. Nilisoma gazeti fulani na kuona jinsi mwandishi mmoja akiwaandikia wamarekani weusi, naye alikuwa mmarekani mweusi; alisema "Ukitaka kuficha kitu kwa mtu mweusi, kiweke kwenye karatasi. Maana hasomi. Ukiweka hata dola mia moja kwenye kitabu, utaenda miaka kumi; ukirudi utaikuta. Wana mzio (allergy) wa kusoma!" Ni lazima tujikaze na kutafuta maarifa ya kulea watoto, si kuwapa chakula, nguo na malazi tu! Kuna zaidi ya hapo. Tabia na kujitegemea ni muhimu.

Zamani watu wengi waliacha wazazi wakajitegemea na kusaidia wazazi. Siku hizi watoto wazee wanakaa kwa wazazi na watoto wao, au hata wajukuu zao. Magomvi madogo madogo yanatokea walipooa au kuolewa na warudi nyumbani. Aidha tabia zao ni ngumu au hatukuwafundisha uvumilivu. Lazima uwe na ratiba na watoto wako, usiache wajikuze. Panga magoli au malengo ya unayotaka watoto wako wafanye! Sisi ndiyo tunaleta tofauti katika maisha ya watoto wetu. Ukimwona mtoto ana huruma, uchoyo, mchapa kazi, ana hekima, au msema kweli ujue mara nyingi hivi vinatokea nyumbani. Tunda halianguki mbali na mti.

Gazeti la Times la May 20, 2013 lilionyesha kwamba watoto wengi wapo nyumbani, na kushugulikia mambo yao mengi (kizazi cha mwaka 2000 au Millenium). Wanapenda kujipiga picha mpaka 85 kwa siku wakituma kwa face book "niangalie nakula, niangalie naendesha pikipiki" n.k. Tabia ya umimi imeanza kutapakaa, hivyo watoto wasaidiwe kujikana nafsi ili watakapoishi katika jumuiya na familia wawe raia bora kwenye falme hizi za dunia na ile ya paradiso.

Sulemani asema moyo wa mtoto una upumbavu, ila yabidi asahihishwe. Apewapo kazi usiachie hivyo ila uitathmini na kuisahihisha. Na pia aone matokeo ya kazi mbaya au tabia mbovu (natural consequence). Usipoteze muda wako kibaruani au masomoni kama mzazi wakati mtoto anakua. Sijasikia mtu aliyestaafu aliyesema, "Ninajuta, kwa nini sikukaa ofisini muda zaidi!"

Wazazi, adui wa roho anafanya kazi ovataimu kupotosha watoto wetu. Anawachukia ni ajabu. Ni kama simba angurumaye akitafuta awameze. Anajua ana muda mdogo. Macho yetu yamefungwa tusione hawa malaika walioanguka. Wana uzoefu wa miaka 6000 wapo kibaruani. Ila tujipe moyo kuna malaika wa Mungu pia wa kutusaidia endapo tunachagua upande wa Muumba. Tuko vitani, vita vya kiroho. Hebu tusiwe na upendo ulio na upofu kwa watoto wetu. Upendo huo potofu

utafanya tusiwaadilishe jinsi tunavyotakiwa. Vifaa vya vita ni neno la Mungu, haki, imani, kiasi, kukesha na uvumilivu.

Usiache watoto wajifunze uovu eti wataweza mbeleni kuchagua mema au mabaya! Magugu ya uovu yataongezeka kwa kasi kuliko wema. Muda wa kulea unapita haraka, na ni mfupi. Hivyo usiweke magugu bila sababu eti ajue maovu pia, na kisha achague.

Linda kwa uangalifu milango ya macho, masikio, mionjo, hisia na harufu! Mtoto asisikilize muziki wowote. Miziki kama ya rap na Rock imeonekana kuleta mivuto mibaya ya tabia kama uharamia na ulevi. Jaribu kuangalia kwenye tovuti kwa vichwa kama "rap na tabia ya watoto". Si siri, hata kwa wale wasiojali Mungu. Muziki ukoleapo unaacha fahamu za ubongo (frontal lobe) kutofanya kazi zinabaki hisia (feelings and emotions) na hii inamfanya mtu awe dhaifu kufanya maamuzi mema. Epuka miziki inayorudia rudia maneno hata kama ni maneno ya Mungu mfano "Nakusifu, nakusifu, nakusifu." Baada ya muda hufikiri inakuwa kama ulevi. Unasahau hata unamsifu nani! Hata utungapo nyimbo maliza maneno mfano "nakusifu Mungu kwa vile umenijalia maisha n.k."

Hata runinga ina tabia hii, mtoto akitazama baada ya muda hatumii ubongo atakuwa tayari kusikiliza chochote aambiwacho na kufanya (bypass the frontal lobe). Siku hizi runinga ana dada yake anaitwa compyuta. Wengi tunanunua hivi vitu na dhamira nzuri kusikiliza taarifa, na historia (documentary) ila udhibiti inapungua na hata ukienda kulala watoto wanaendelea kuangalia wanachotaka.

Pia nimeona hata matangazo ya biashara yana watu waliovaa nusu uchi na kusema maneno ya ajabu. Mtoto hawezi kutofautisha maisha halisi na yale ya kwenye runinga.

Mtoto wa miaka minne alimkimbilia baba yake nje na kugumia, "Baba huyu mtu anataka kumwuua mama aliyekaa dukani." Tumesikia watoto walioua, wakifikiria mtu huyo ataamka na kuwa katika kipindi kingine. Runinga inaonyesha watu wanaoishi pamoja bila kuoana. Hii ni dhambi kwa maagizo ya utamaduni wetu na Neno la Mungu.

Kwa nini runinga iwe mwalimu wa watoto wetu na maadili mageni? Watoto wa televisheni wana usikivu mdogo, wanatafuta mahaba mapema, wanapenda magomvi, makelele, na ghasi na hata ukatili . Runinga inakuwa mwalimu wake na

hivyo hata kupoteza maadili na mambo ya kiroho si kitu kikubwa kwake. Na hata sisi watu wazima mengi ya uovu tunapoyaangalia tena na tena tunapunguza nguvu ya kujaji uovu na wema. Hata mayaya wakiangalia siku nzima na watoto wetu pia wanapata dozi.

Ni muhimu mtoto achaguliwe shule nzuri ambayo itamsaidia kumjenga kiroho, kimwili na kijamii. Usipeleke watoto watakapopata majaribu ambapo tabia na mambo ya kiroho ni duni. Vitabu na magazeti wanayosoma watoto viangaliwe. Watoto wasisome vitabu vya waandishi makafiri wasiojali tabia ya mtoto. Vitabu vingi vinapanda mbegu za uovu kwenye akili za watoto, na kupunguza thamani ya neno la Mungu na maadili mema. Vimekuja vitabu vingi vya watoto, vya uchawi vimekuja, kama vile vya Harry Potter, Pica n.k. Burudani ziangaliwe, nyingi siku hizi ni za anasa au zinazohusiana na uchawi.

Computer pia ni shida. Watu wamewasiliana kwenye mitandao ya facebook, na wengi wametoroshwa. Nimesikia watoto wadogo wakitoroshwa na wazee kwa sababu ya kuwasiliana nao kimapenzi na kupata hisia zisizo halisi kimaisha za kubuni au kuwazia hivi(fantasy) au kuishi maisha ya anasa. Mtoto anaathiriwa kwa mvuto mkubwa zaidi na uovu zaidi ya wema. Mtoto asiachiwe kwenda kokote, na saa yo yote anapotaka. Mtoto wa kike ni tofauti na mtoto wa kiume. Japo tunazungumza juu ya usawa, madhara kwa mtoto wa kike akitembea usiku peke yake ni tofauti kidogo na ni makubwa kuliko ya mtoto wa kiume.

Talaka pia ni athari kubwa kwa watoto. Watoto wameonekana kuwa na shida kubwa ya nidhamu wakijiunga na magenge ya ulevi, kuvuta sigara, uharamia, wizi, umalaya na mengineyo. Na ndiyo maana katika kitabu hiki tumezungumzia ndoa kwa muhtasari.

Adui shetani anafanya kazi na mtoto hata aliyezaliwa leo! Mama wapaswa ndiye awe mpiganaji wa mtoto huyu. Ni ukatili kuacha makucha ya shetani yakimnyangua mtoto. Mama usiwe adui wa mtoto kwa kuruhusu uovu uanze au uendelee. Usalama wa watoto unategemea mno mzazi kuwa macho na kukesha. Wadumu katika kumpenda Mungu nakuomba msaada toka kwake kila saa!

Kanuni ya upendo wa Mungu iwe dira. Soma 1Wakorintho 13 na Zaburi 91. Mafungu haya yanatueleza kwamba Mungu anatulinda na analinda watoto wetu. Nafikiri wote tunangoja ile sauti siku moja, "Vyema mtumishi mwema, ulikuwa mwaminifu kwa madogo, ingia katika raha ya milele." Kwenye utafiti Marekani,

asilimia themanini na mbili walisema kwamba wana imani wataenda mbinguni. Ni nadra sana mtu kusema anapanga kwenda ziwa la moto au jehanamu; hakuna anayejipangia mambo mabaya! Shida ni kufuata ile njia nyembamba ya mashimo isiyo na uzuri, ukilinganisha na pana ya lami iliyojaa maua na mapambo.

Sisi wenyewe hatujiwezi. Kuwa mzazi ni kazi kubwa na mara nyingi inakatisha tamaa. Maana kila binadamu mimba yake ilitungwa dhambini: "Tazama mimba yangu ilitungwa katika dhambi." Zaburi 51 yatukumbusha tumezaliwa dhambini, na kila binadamu amefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

Hebu Bwana Atutegemeze na kutusaidia katika kazi hii nzito ambayo mara nyingi imenitia hofu, imeniletea machozi na kunikimbiza magotini kutafuta uso wa Mungu. Hebu tushirikiane kutafuta uso wa Mungu maana Bwana anajua watoto wetu toka wakiwa tumboni na kuwatakasa. "Usiseme mimi ni mtoto, maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema neno nitakalokuamuru." . tujipe moyo kwani Bwana anapenda watoto mno wetu kuliko hata sisi tunavyowapenda

Paulo anamwambia Timotheo kwamba, "Wewe umeyajua maandiko toka utotoni mwako, toka kwa bibi yako Lois na mama Yunisi!" Watoto wetu ni mbaraka kwa Mungu kufanya mapenzi yake, kwetu na kwenye jumuiya; hebu tuendelee kuwaombea.

**MASWALI NA MAJIBU YA WAZAZI** (**mifano** )

1. ***Mimi ni mama wa watoto wadogo watatu, nimesoma na ningepata kazi, ila wengi wananiambia kukaa na watoto ni vizuri.***

Mpango mzuri ambao watoto watafaidika kupita yote ni wa mama kukaa nyumbani. Na kama mna uwezo wa kuishi kwa mshahara mmoja jitahidini mama akae nyumbani. Watoto wanafurahi wakikaa na mtu mmoja anayewapenda na wa karibu kama mama. Hata kujifunza wanajifunza kwa urahisi zaidi. Hakuna mtu unayeweza kumlipa akatunza watoto wenu kama mama! Utafiti umeonyesha kwamba watoto wanaokaa na mama wana magonjwa machache kuliko wale wanaokaa na makundi ya watu wazima na watoto.

Nafikiri hii ni pamoja na magonjwa ya kuambukiza, ya kukosa jua, ya kukosa mazoezi n,k. Mahusiano yanajengeka zaidi na unakuwa na nafasi ya kumfundisha mtoto wako utii ukiwa naye kuliko akiwa na watu wengine. Kuna wakati inabidi mtoto wako akae na wengine, ila hakuna aliye bora kama mzazi. Jumuiya za kutunza watoto zisizomthamini Mungu hawafundishi watoto kuhusu Muumba, na watoto kunyanyaswa inakuwa rahisi.

Mama wengine wasema wanaboeka kukaa na watoto siku zima na wangependa wapate kazi iwachangamshe. Kusema kweli kazi nyingi zinaboa kwa namna fulani. Piga picha ya mtu wa maabara kwenye darubini siku nzima, au mwanariadha anayefanya mazoezi siku nzima. Nafikiri kitu ambacho huwa tunafikiria ni pesa, kwamba hulipwi. Jaribu kuangalia kama unaweza kutafuta biashara ukaifanya nyumbani kwako ili ukae na watoto wako. Pia utafute mama wengine na kuwa na mikutano nao, angalau mara moja kwa juma. Hii itasaidia kutoboeka kwako.

Hata hivyo mama ana kazi nyingi kuamka asubuhi, watoto wavae, awapikie, asali nao. Na akienda kibaruani akirudi mara nyingi anachoka hata watoto wakimwomba awahadithie hadithi anakuwa amechoka. Na mahusiano ya unyumba nayo yanavunjika siku hizi kwa vile kila mtu anakuwa amechoka na ugomvi kidogo ukitokea basi kila mtu yuko tayari kusambaratika aende kwake. Watoto wanahitaji wewe mama uwe nyumbani, kama haiwezekani basi itabidi uende kibaruani ukimwomba Mungu atoe nafasi siku moja utunze watoto nyumbani.

Mama mmoja rafiki yangu, tuliyesoma naye, aliamua kukaa na watoto wake nyumbani hadi walipofikia umri wa kwenda shule. Na walipoenda shule alifanya kazi asubuhi tu, na mchana alikuwepo nyumbani kuwapokea watoto walipotoka shuleni. Mama huyu alikuwa amesoma sana, alikuwa na PhD, lakini aliamua kutunza watoto kwanza. Watu walimcheka sana, wakamwita mjinga, hata kama ni msomi. Lakini leo, anavuna matunda hapa hapa duniani, make watoto wake ni tofauti, wana tabia nzuri, tofauti kabisa na wengine wa rika lao.

2. ***Tuna mtoto wa miaka miwili aitwa Baraka, ambaye anataka abebwe kila saa, na tukimkanya asifanye kitu, analia na kurusha vitu huku akijigaragaza (tantrums). Ukimwambia asishike vitu kama vile vyombo vya umeme hasikii. Je miaka miwili inatosha kumchulia hatua za nidhamu?***

Katika nia nzuri ya kumfurahisha na kutaka muwe na amani mumemfanya awe kisultani. Haiwezekani kumbemba kila saa! Mwacheni alie wakati mwingine, hatakufa! Akiwa amekula, hana kiu na ameenda chooni, muwe huru mkiendelea kumwangalia mkifanya shughuli zenu. Akipiga kelele msimwangalie sana, angalieni mbali kana kwamba kuna hatari ila msimbebe.

Kama mmezima taa usiku acheni apige mayowe, kumfundisha tabia na nidhamu kunaanza toka anapozaliwa! Soma, ujue namna ya kumfundisha mtoto hata wa miezi michache nidhamu, itakuwa huyu wa miaka miwili anayetaka kuwapa shughuli! Anajua mnampenda kweli, naye mnamwona anapendeza ila hajikani nafsi. Anataka maisha yote yazunguke kwa matakwa yake. Lazima awe na wigo wa vitu ambavyo aweza kuvifanya, mkimwambia la, iwe la!

Adhabu za kuchukua vitu anavyovipenda zitumike (consequences). Kiboko kitumike kwa nadra sana. Baada ya kumwambia mara kadhaa. Kutokana na umri wa mtoto, mzazi awe mwangalifu ili asimwumize mtoto. Usipige ukiwa na hasira. Mtoto ni vyema ajue kosa lake kwa uwazi kabisa. Mzazi anahitaji uvumilivu mwingi. Mtoto mdogo wa umri huu ana udadisi, ila haina maana aharibu vitu. Mwachie aguse kile ambacho hakina hatari ukiwepo ila awekewe wigo wa vitu vinavyopaswa kufanywa na visivyopaswa kufanywa. Mfundishe kwamba, kumwaga vitu, kuharibu, kuangusha vitu, au kuua hata wadudu ni kosa kama wadudu hawa si wa madhara. Ni kweli miaka hii ya awali ni changamoto, ila mambo haya ni kwa watoto wote wanaoendelea kukua. Washugulikie wawe na utii bora na wakiwa wakubwa utafurahi kama umefanya kwa upendo na kuwasaidia kuwa raia bora.

3. ***Watoto wangu bado ni wadogo, ila napoona wale wenye watoto vijana kuanzia miaka kumi na mitatu (teenager), naona wana shida nyingi na watoto wao, kuliko mimi. Je, nifanyeje niepuke shida hizo za mbeleni?***

Mafikara uliyo nayo ni ya wazazi wengi! Tunakusahuri utumie muda mwingi kujenga mahusiano na watoto wako wakingali wadogo, kama tulivyoshauri katika kitabu hiki. Pia mkabidhi Mungu huu woga ulio nao maana Yeye anajua ya mbeleni, ili tusikope shida za kesho na kuwa na wasiwasi au kusononeka. Tuendelee kujifunza zaidi, na kuombea malezi.

***4. Kwa nini inakuwa kazi watoto kutii tukiwaagiza kitu? Kwa nini mpaka tuwape adhabu au tuwafokee? Kwa nini hawaonyeshi ushirikiano na kukubali yale mambo ya maana tunayowaambia ili wapunguze ugomvi?***

Changamoto wanayotupa inatokana na roho ya binadamu ya kutaka kuwa na upinzani wa vitu ambavyo ni vizuri, vya Mungu, na kuvutwa na sumaku ya viovu. Roho ya binadamu, toka mwanzo wa dunia, ina ushindani wa falme hizi mbili: Ubaya na wema. Wanapenda kuonekana kama ni mashujaa na wanatawala ukumbi. Hata watoto wakiwa wenyewe kwa wenyewe wanataka kuonyesha ni nani ambaye ni bingwa au nyota! Hii inatokea shuleni, kwa wazazi na pengine. ''Sidhani kama unaweza kunifanya nikusikilize au nifanye utakavyo.' Roho hii ya ushindani ni lazima ishugulikiwe, mtoto ajue ni nani mwenye mamlaka mapema, maana hata watoto wengine wakisikia iwe darasani au nyumbani, nao pia wanataka kupinga mamlaka. Weka sheria na sema kile ambacho unatazamia, na fuatilia

***5.Nikiwa na miaka ishirini na mmoja nilipata mimba nje ya ndoa na sasa nina mtoto wa miaka mitatu. Najua si mbali mtoto atauliza baba yake ni nani. Nimwelezeje, na wakati gani?***

Wakati utafika, itabidi umweleze habari yote na uhusiano wenu na baba yake. Ila si sasa. Lazima awe amekomaa kidogo na hisia zake ziwe tayari kuchukuliana na jambo hili. Usifanye kitu hiki kuwa siri kubwa ambayo aidha wewe au yeye mnakuwa mnalifikiri wakati wote. Kina mama wengi wamefanya hili kuwa siri na ni makosa.

Jambo hili lapaswa uzungumze na mtoto na kuliweka wazi. Hasa akiwa mkubwa. Usimdanganye, utakapomweleza. Zungumza kwa faragha na kwa upendo kuhusu mzazi wake ukifika wakati wake. Anza kumpa habari chache kuhusu mzazi wake. Mfano, ''Baba yako aliondoka kabla hujazaliwa. Hakutaka tuishi pamoja. Sijui kwa sababu gani. Pengine ilikuwa haiwezekani yeye kunioa. Sifahamu. Ila nina uhakika angekuona angekupenda na kukutunza, ila hakuwahi kukuona. Pengine tuanze kusali ili Mwenyezi Mungu Atupe mtu mwingine kuwa mume wangu na baba yako. Je, unapenda tufanye hivyo?''

***6.Nakasirika kwa vile mtoto wangu wa miaka miwili tukiwa ibadani hakai mahali pamoja. Anajua hapaswi kukimbiakimbia, ila anapiga makelele na kukimbia kimbia, nifanyeje?***

Kwa kweli watoto wa umri huu hawawezi kukaa mahali pamoja. Na kwa vile ibada nyingine hazitengi vipindi vya watoto kwenye chumba chao. Nafikiri hakuna

haja ya kumwadhibu kwa hili ila lifanyie kazi kila mara. Mlete na vitu vya kushugulikia kama ni kuchora na rangi (crayons) apake rangi, au mwanasesere. Ila usimwache mtoto na yaya eti unaenda nyumba ya ibada. Mtoto huyu ni mkubwa na anajifunza kitu kanisani/msikitini, japo kidogo na anajenga tabia ya kicho kwa vitu vya Mungu.

Yeye anahitaji kumjua Mungu kuliko wewe maana ananza safari yake hivyo unafanya vizuri. Jaribu kuwa mvumilivu na kuendelea kuomba, ili kanisa lako liwe na sehemu ya watoto. Fanya mazoezi naye wakati wa siku za katikati ya wiki jinsi ya kukaa kanisani ili akifika awe amezoea. Watoto wakiwa na mwalimu wa watoto siku ya ibada, na ukimleta toka akiwa mdogo atazoea kukaa na kutulia, atakuwa anajua wakati huu ni wa kufanya nini? Usiende Ibadan bila mtoto ukimwachia mtu!

7.***Je, ni kwanini watoto ambao wanalelewa kwenye familia zenye wazazi wazuri wenye kila kitu wanatokea kuwa wabaya na wale wenye wazazi wabaya wenye hali ngumu ya maisha pia wana watoto wanaotokea kuwa wema?***

Si mazingira na urithi peke yake vinavyofanya watoto wawe kama walivyo! Wazazi wengi wanajipongeza hata kujitapa wakiwa na mtoto mwenye tabia nzuri na mafanikio, na kujilaumu wakiwa na tabia mbaya. Wanasema "Je, tulikosea wapi?' Ni kweli kabisa wazazi wana mvuto mkubwa wa tabia ya mtu ila siyo fomula yote. Mengine ni uzoefu wa mtoto, lishe ya mtoto, marafiki wa mtoto, uchaguzi wa mtoto maana Mungu ametuumba tuwe na uchaguzi.

Kwa kweli uzazi ni changamoto na zawadi pia. Unapofikiria unajua watoto wako na kwamba umewalea vizuri; unaweza kupigwa na butwaa kwa jambo usilolijua. Endelea kuishi magotini, hata watoto wako wakiwa wakubwa, usifikirie kwamba umechelewa. Bado wana muda wa kubadilika; na wasipobadilika utafanya tofauti hata kwa wajukuu zako. Hata kama kwa udhaifu wako ulifanya makosa ya wazi kwa watoto wako, una nafasi ya kusoma na kujua kwa ajili ya watoto wa jumuiya na ndugu na jamaa ili uwape uzoefu wako nao wanufaike.

7. ***Mtoto wangu alichanjwa na watu wengi wameniambia lazima niwe mwangalifu wa chanjo.***

Kwa kweli mambo ya chanjo ni topic ndefu sana. Kuna shirika linaitwa National vaccine information center (NIVC) lenye wanasayansi wengi wanaotoka dunia nzima wa biology, tiba, hisia za fahamu, bacteria, na wengineo. Wengi

wanaozungumza wanaona kwamba wanarisk kazi zao kwa kusema haya. Toka 1997 hoja ya chanjo inaendelea kukua. Wazazi wanahitaji kujielimisha kwa hili ili kusudi utafiti wa kinga uendelee kufanywa. Hatuna shaka kwamba chanjo zimesaidia wengi. Na tunaamini kwamba kinga ya mwili ya asili itawezeshwa kwa ubora kama tutafuata yale masharti kumi ya afya kwa magonjwa mengi. Usalama wa chanjo wahitaji kuendelea kuwa na utafiti mwingi. Ni vizuri mteja ajue uzuri wake na ubaya wake na zisitolewe kwa mpigo. Watoto wengine wamedhurika ubongo kwa ajili ya chanjo.

Utajuaje kama mtoto ameathiriwa na chanjo? Nafikiri kama mtoto hakuwa mgonjwa kabla, na akapata hiyo shida kwa sababu ya chanjo, mzazi ajue reaction ya chanjo inakuwaje na ajue jinsi ya kuiripoti. Ni vizuri ajue mtengenezaji wa chanjo na namba za hizo chanjo. Kwenye gazeti namba 105 la Family Living la US Mar/Apr 2001; mzazi aliandika kwamba aliagiza chanjo ya tetanas ili ije pekee yake kwenye famasia kuepuka chanjo za mseto.

Kwa sababu nchi zetu ni changa na mambo mengine ni vigumu kufanyika, hebu wazazi tusome zaidi kwenye mtandao habari za kweli za madhara ya chanjo na jinsi ya kusaidia familia zetu. Iwe mteja unayejielimisha, ni kweli chanjo zimeua watu, zimeletea watu kisukari, kuletea watoto utindio wa ubongo (angalia kazi ya Dr Sptizer walter wa Mc Gill university Canada). Chanjo zinaandikwa kwenye chupa kama dawa zozote; madhara na faida zake. Chanjo zingine zinahifadhiwa kwenye zebaki ambayo ina madhara kwa mwili. Kina mama wajawazito, inapendekezwa ni vyema wasipate chanjo mpaka wakati huu upite. Usiwe unachukua matibabu kusoma vizuri. Siko hapa kukwambia la, au ndiyo, ila jitahidi upate habari zaidi.

8. ***Waweza kukata kondo na mtoto wako mtu mzima bila kuharibu mahusiano?***

Hii ni shida hasa ya mama wengi kwamba hisia zao zinakuwa bado kwa watoto wao (attached) na hasa kwa wale ambao wamelea watoto solemba, bila baba mtoto. Watoto wengine watu wazima bado wanaishi nyumbani, au mama anaenda kuishi na watoto wake japokuwa hana kasoro yoyote ila kihisia anaona analiwazwa kwa namna fulani.

Mzazi ni lazima awaonyeshe watoto kwa matendo na kwa maneno kwamba wanaweza kuishi au kufanya lolote wanaloweza. Watoto wanajifunza kwa tabia zetu kwamba tumewaacha huru na si kwa maneno. Mzazi mmoja aliomba mtaji kwa mtoto wake ili ajitegemee, "Ili nikuache huru nisikufuate fuate hata ukioa na kukuharibia ndoa yako." Ila aliendelea kumfuata mtoto wake hata alipooa na kukaa

kwake kwa miaka. Kwa mazungumzo na matendo yake alikuwa anaharibu ndoa ya mtoto wake bila kunuia.

Ni kweli mtoto aweza kuwa na miaka kumi na minane ila ahitaji usaidizi wa shule na mengineyo. Mjue mtoto wako vizuri. Mtafutie njia ajitegemee ikiwa ni kibarua, elimu, rasilimali kama ardhi, au mtaji. Kwa mtoto aliyetoka na kurudirudi tena tafuteni shida iko wapi na kumsaidia. Mara nyingine hata mtoto aliye kwake, waweza kuwa haujakata kamba naye kuliko aliye nyumbani. Mambo haya yahusisha hisia sana na pengine mnalisha na kumvisha huko kwake! Zungumzeni kama wazazi msikae kimya na kulalamika lalamika tu hasa watoto wakiwa hawasaidii kazi wanazungumza tu, na hawasaidii mzigo wa maisha. Gazeti la May 20, 2013 Times limezungumzia shida hii, si yako peke yako! Mtoto wa namna hii aweza kuwa na upweke au hana uhalisi wa maisha, na hata kama ameoa au kuolewa yuko hatarini kuharibu ndoa yake wakati wowote. Wazazi pia wasiangalie tathmini za watu kwa kulazimisha binti yao aolewe maana watu wanawauliza kwa nini haolewi na awapatia wajukuu!

9. ***Je, kuna uzuri gani wa watoto wangu watu wazima kuishi nami nyumbani?***

Wazazi wengine wanapendelea kuendelea kukaa na watoto wao watu wazima kwa vile wanapatana katika mengi. Siku hizi hata kupatana mke au mume ni kazi! Tunaishi katika dunia ambayo watu wamekosa uvumilivu. Kila mtu anataka kuishi mwenyewe na akiishi mwenyewe anapata upweke, na kuwa kwenye simu saa yote, au kutembelea watu saa yote! Akipata mteja wa kuzungumza hamwachii. Ila akiwa na mtu kwenye nyumba, anatasa kugombana saa yote.

Watoto wanaoishi nyumbani ni msaada kwa majukumu, kumaliza shule vizuri na hata katika maisha ya jamii. Wasichana na wavulana wengi wamejiingiza kwenye hatari za ngono kwa sababu ya kukaa wenyewe; wanatembelewa na mtu wa jinsia tofauti na kuanza mahusiano mabaya ambayo walikuwa hawakupanga. Msichana akiolewa akiwa ametoka kwao shida hii inapungua sana, labda amfuate huyo mwanamume nyumbani kwake. Mtoto pia anakuwa hana upweke, na kupata mashauri toka kwa wazazi kuhusu yule anayeolewa naye kabla hajakaa naye au hajamtembelea anapoishi.

Mzazi pia aweza kupata nafasi ya kumwona vizuri huyu mkwe au mkamwana. Majaribu pia yanapungua ya kufanya vituko akiwa kwa wazazi maana ana mashahidi wengi. Mtoto pia anazidi kupevuka na kupata mawazo mazuri ya hekima akiwa na wazazi. Jambo jingine ni kwamba, wazazi wakiwa na mahusiano mazuri

na mtoto wanaweza kujadili shida zao na kuona waendelee kukaa namna gani. Watoto wanaweza wakapunguza bili za kodi ya nyumba na matumizi mengine ili wasaidie familia kitu kingine.

10. ***Ukiwa na watoto watu wazima na wakawa wana uasi nyumbani kwako uchukue hatua gani?***

Huu ni wakati mgumu kwa mzazi kumwambia mtoto aondoke. Mara nyingi mzazi anaumwa na dhamira kwamba pengine hakufanya jambo lisilo sawa. Na mahusiano yanaharibika kwa miaka mingi na pengine kidonda hicho kisipone. Kama mtoto anazidi kufanya uasi na ukaidi nyumbani ni vyema aondoke, maana anawatia huzuni wale wazazi mle ndani kwa kutofuata sheria za kimsingi, ambazo kila nyumba inazo.

Tabia ya kuishi katika dhambi za wazi wazi mfano madawa ya kulevya au ulevi, kuleta kimada na kuishi naye, na kufanya fujo za ugomvi nyumbani ni mojawapo ya vitu ambavyo itakuwa vizuri kuzungumza, kisha vikiendelea kuna haja ya kutengana kwa upendo ili mwendelee kuwasiliana mkiwa mbali. Mama mmoja alisema kijana wake alikuwa akileta rafiki wa kike na wanalala kwenye kochi lao sebuleni wakikumbatiana. Alimkanya kuhusu jambo hili na hakusikia, ilibidi wamwambie aondoke.

Kama wazazi, mna jukumu kwa lile linaloendelea nyumbani kwenu. Je, jambo hili, katika kesi hii, linamtukuza Mungu kwa imani yenu? Je, ukiwa na mtoto aliye na matusi au anapangua kila kitu kwenye nyumba utamwacha tu? Je, akiwa kupe na hataki kufanya kazi? Ni vizuri kumpa muda kama mwaka mmoja aondoke nyumbani, utashangaa atapata kibarua haraka! Ila usimtupe mtoto kwenye uhalifu zaidi ya alio nao; kama kuolewa mapema bila kupanga au kuingilia ulevi.

Lazima nyumba iwe na sheria na mawasiliano. Kukaa pamoja na kujadili mambo ya familia na kuishi ni muhimu. Jaribu kufuatilia sheria hizo kwako. Kama mtoto wako anakuwa na shida za kisheria na amewekwa jela kwa madawa au wizi msaidie aondokane na tabia hii; ila baadaye mwachie achukue majukumu ya matendo yake na kupokea matunda kwa tabia yake hiyo. Kumbuka wewe siyo Mungu uchukue majukumu ya uhalifu wake, itabidi aende ili uokoe jahazi la familia!

11. ***Je, tufanyeje ili watoto wetu wazima watuheshimu?***

Mzazi awe na upole, ukaribu upendo. Mtoto wako aliyetoka kwako akirudi pengine kufua nguo au kufurahia chakula cha mama mpe hiyo nafasi. Pia maneno yako yasiwe ya ugomvi na kutaka kuonyesha mamlaka yako kwake na kumwamrisha kufanya vitu. "Nipe pesa ya kununulia baiskeli, fanya hivi au vile."

Tujue wao ni binadamu na kuna mstari wa kuongea na mtu bila kumvaa au kumwingilia usoni. Ni vizuri kukaa pamoja na kujadili badala ya kumshtukiza. Je, atumie vitu vya familia kama vyake mfano gari, baiskeli, au lazima aombe ruhusa? Weka sheria ili mheshimiane.

Mara nyingi tunawazingira watoto wetu mno tukiogopa kuwapoteza, kwamba wataenda mbali na fimbo zetu hazitafika kule na bado tunahitaji kuwamiliki!

Tumeona mfano wa mwana mpotevu kwenye neno la Mungu: Aliishi akimlaumu baba yake na baba hakutaka atoke. Alipomwachia alirudi wakaheshimiana! Jadili haya tunaona mfano wa mwana mpotevu aliyebaki nyumbani akisema baba yake alimpendelea yule aliyeenda, baba alijibu; "Sikia mwanangu, wewe u pamoja nami siku zote, na vyote nilivyo navyo ni vyako. Tena kufanya furaha na shanngwe ilipata kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka, alikuwa amepotea naye amepatikana."

Mchukue mtoto wako na mjadili hili, ili mweze kuheshimiana. Mambo mengine si ya kuepa epa na kuinamisha nyuso yako kwenye mchanga tukifikiri yatajitatua. Epuka kuhadithia wema wa huyu mtoto na ubaya wa yule ukiweka maksi utapoteza wote na heshima yako pia. Kila mtoto ataka apendwe zaidi, usijiunge na kundi fulani.

12,***Ufanyeje ikiwa watoto wako wanarudi rudi nyumbani baada ya kujitegemea kutaka wakae nawe tena?***

Sijui nchi yetu ina watoto watu wazima wangapi ambao wanaishi na wazazi. Ila nchi ya Marekani ina watoto milioni kumi na sita! Watoto wengi wanarudi nyumbani kwa sababu ya ugumu wa maisha, yaani kukosa pesa au kuwa na talaka. Wanaporudi wanakuwa na familia. Kuanza maisha tena ya kuwapikia na kushugulikia wajukuu yahitaji kukaa pamoja ili kutatua pale wanapofika tu, na si baadaye.

Mama mwingine alilalamikia binti yake aliyekuja na watoto wadogo, akawa anawaacha na kwenda kutafuta wanaume na kuja usiku! Wazazi wakawa wanaogopa kumwambia maana wakimwambia aondoke, wajukuu wao watapata shida na mama kama huyu.

Wengine wameona kwamba kazi za kupika, kufua n.k zigawanywe ili mama huyu mzee asipate kazi ya kupikia watu wengi, kufua, kusafisha nyumba na kuosha vyombo. Je, una watoto ambao wakirudi hawachukui majukumu? Kaa nao uwaeleze, kama moyo wakuuma waambie uko tayari kukaa na wajukuu ila si wao. Ila wengine wakiona kwamba unawapenda sana watoto wao. wanasema wataenda nao ili wakuumize moyo.

Mababu na mabibi wengine hawapendi wajukuu wa mtoto fulani. Wengine wanawapenda na kuwashughulikia sana wajukuu wa msichana zaidi ya wale wa mvulana. Hawa ni rahisi kusema nenda na watoto wako! ila usiwanyime watu mema yaliyo haki yao, ikiwa yako katika uwezo wa mkono wako kuyatenda. Ila mababu/bibi wengi wamechoka kifedha, kihisia na hawana nafasi za kuweka hawa wote. Jiulize, je, umechelewa? Au kuna uwezekano wa kukarabati daraja? Zungumza, sikiliza na heshimu. Usipate hofu. Siku ya hofu yako umtumaini Mungu.

13.***Je, mtoto afanye kazi kiasi gani kwa siku?***

Ni vyema mtoto afanye kazi ila kuwe na balansi, siyo siku nzima ya kazi na wala hamna mchezo. Mtoto wa miaka minane ajue kufua nguo zake vizuri na asimamiwe. Kuwapa wanyama chakula, kufagia, kusafisha chumba chake na shughuli chache za jikoni. Asikae kwenye Tv au kupiga tu gumzo. Lazima ujue mtoto wako yupo wapi.

Simamia au fuatilia kazi ulizotoa kama zimefanywa, usipofuatilia utakuwa umepoteza somo. Usiseme huna nafasi. Mtoto anajifunza kazi vizuri ukimsimamia. Hii itamfanya awe mfanyakazi mzuri akiwa na wenzake au mume/mke bora. Magomvi mengi yametokana ya kuishi kivivu. Asiyefanya kazi asile. Kwa habari zaidi, angalia doorposts.org pam Foster au Rb Bradley( nogreaterjoy)website

14.***Je, mtoto asipopenda kula alazimishwe?***

La! Usimlazimishe mtoto kula kama si mgonjwa! Mara nyingi shida hii ipo kwa wale wenye chakula kingi, na mtoto anakiona saa zote, na kula kula tu siku nzima! Mtoto asile vitu vya sukari na kupishanisha muda wa kula, ikifika wakati wa kula atakuwa na hamu ya chakula. Mara nyingi mtoto anaishiwa hamu ya kula wakati wa kipindi

cha miaka ambayo hakui sana. Jaribu pia kujifunza mapishi na kile anachopenda ukiweza kama kinafuatana na milo ya afya tuliyozungumzia, mpe.

15. ***Je, wapaswa kumwomba mtoto wako msamaha ukimkosea?***

Ndiyo. Mara nyingi imebidi niwaombe watoto wangu msamaha kwa kuwa na haraka au hasira na kusema nisichopashwa, au kuwahahidi kitu nisifanye, au kuwalaumu kwa kosa ambalo hawakufanya. Nikifikiria baadaye au wakati wa kulala nikikumbuka na kuwaomba msamaha: "Jana nilifanya hivi kwa makosa, unajua mzazi ni binadamu tu naomba unisamehe." Mara nyingi watoto wamesema, "Tunajua ulikuwa umekosea, ni vyema umeomba msamaha, tumekusamehe." Na wote tunafurahi sana.

16. ***Je, nifanyeje kama mtoto wangu bado anakojoa kitandani na ni mkubwa?***

Kwanza usimwadhibu, hakuna anayetaka kukojoa kitandani kwa makusudi, utaleta shida zingine zaidi. Panga uwe unamwamsha usiku saa fulani. Waweza kutumia saa zenye kengele. Asinywe maji masaa kabla ya kulala. Dawa za asili kama pia zimetumika. Kumbuka ni shida ya watoto wengi hasa wa kiume, na mara caribú zote haihusiani na ukosefu wa nidhamu. Itakuja kuisha siku moja, ila utaona "ni siku nyingi mbona haiishi"

17. ***Tuna watoto watatu na tuko busy, tunajaribu kutafuta muda tunashindwa, je, tufanyeje?***

Mtoto anajaji upendo kwa muda mnaotumia kuwa nao. Kwa vile mlilewata watoto duniani, tafuteni muda. Ni vyema mama akae nyumbani kama imeshindikana kabisa. Tafuteni jinsi ya kuziba hili pengo. Mtu atakayepoteza ni mtoto maana anajenga tabia na ustadi. Watu wanaweka list ya vitu vya kufanya ila kushugulikia watoto kunachukuliwa kwamba si kitu cha kutiki, kwamba ni wajibu tu. Ni vyema kuwa na desturi ya vitu ambavyo mnafanya pamoja, kama kula pamoja, kuenda ibadani, kwenda kwenye sherehe au likizo. Familia ni zaidi ya kuishi chini ya paa moja! Ni vizuri kuweka vitu vizuri kwenye program kama mzazi ili uweke vizuri zaidi. Hii haina maana usiende ibadani ila angalia usiseme utafanya kila kitu kwa ndugu jamaa na rafiki na kusahau watoto wako. Twaambiwa kwamba tukiwakosesha watoto ni jambo kubwa " imepaswa kufungiwa jiwe kwenye shingo na kutupwa majini". Kumbe jukumu letu wazazi ni Kubwa mno.

Baba mmoja aliyekuwa busy sana, alikuwa hana wakati wa kukaa na watoto wake. Watoto walitamani sana wapate muda wa kubarizi na baba yao. Siku moja alipokuwa bafuni, wakachukua diary yake, wakaperuzi waone kama kuna siku

moja free. Walipoipata wakajibukia appointment, wakaandika "Siku ya kutembeza watoto." Ninadhani baba alikuja kuiona baadaye, lakini hakusema cho chote. Basi watoto wakipata nafasi, kama hayupo, walikuwa wanacheki kuona kama appointment yao bado ipo. Wakawa wanafurahi na kujiandaa; hadi siku mbili kabla, walipoangalia walikuta baba amekata na kalamu nyekundu na juu yake ameweka appontiment nyingine! Watoto walivunjika moyo sana.

18. ***Mtoto wangu wa miaka kumi na minane alitoroka nyumbani na tabia yake si nzuri, nifanyeje?***

Ni vigumu kusema kitu utakachofanya kama jambo kama hili likitokea. Pengine bila ya kumgombeza na kuropoka ropoka maneno mabaya, mwite na ujaribu kumwelekeza na kumtembelea Kama akikataa, si vizuri kwa mzazi kuwa dikteta kwa mtu wa umri huu; itampa uasi zaidi moyoni. Kwa vile ni mtu mzima, akiwa na shida wazazi waweze kumsaidia alipo, jinsi wanavyoweza. Kaa naye umweleze matokeo ya tabia hii na matokeo ya tabia njema; yeye afanye uchaguzi.

Mwana mpotevu alitoka kwa baba yake na baba alimwachia nafasi apumue anavyopenda, alipozinduka toka kwenye tabia mbaya alirudi mwenyewe na kupokelewa kwa shangwe.

19. ***Mnavyoandika kitabu cha malezi; Je, nyumba na watoto wenu wako shwari?***

La, hasha! Ni vita vya kila siku, ila kuna haja ya mtu kuandika na sisi kama wazazi tusaidiane; lile unalolijua utuambie ili tufaidike na lile tunaliojua tutakwambia. Hakuna mzazi mkamilifu. Ila tunajaribu kwa neema ya Mungu.

Kila binadamu amefanya dhambi tunaokolewa kwa neema, naona siku nyingine kwangu ni kama kimbunga kimepita; tunakuwa kama bisi tukingona hapa na pale, na nakosa nguvu kwamba nitaendeleaje na shughuli ya uzazi? Mungu ndiye Atupate nguvu sisi wote. Endelea kujisomea ili ujue zaidi. watu wengine waweza kukufanya uone kama umeachwa na basi kwamba wanaendelea vizuri ila kila mtu ana mizoga yake. Wewe mwangalie Mungu na jifunze zaidi jinsi ya kufaulu, atakuwezesha kwa yote na kukutia nguvu. Mlilie, mwambie kama Yakobo kwamba, "Sitakuacha mpaka unibariki."

20.***Tuna shida ya pesa kwenye malezi ya watoto, tufanyeje?***

Kwa kweli mimi si mataalamu wa ujasiliamali au biashara, ila kuna haja ya kutafuta wataalamu na kujifunza, kisha mitaji. Na kama kuna uwezekano wa kurudi shule kuongeza nafasi za kupata kazi fanya vile. Kama una ardhi lima. Nimeona mahali pengi kama Tanzania, kuna ardhi; wengi wangelima na kukabiliana na maisha ila uvivu unakuwa mwingi.  Shamba ni mali. Fanya kazi kwa bidii angalau masaa manane kwa siku, na endelea kuomba.''Kila aombaye hupewa, kila atafutaye hupata na kila abishaye hufunguliwa.''

Jihadhari na tamaa na ulafi. Je unataka uwe na vitu kama watu wengine, au ni mahitaji ya kawaida? Je, waweza kupunguza matumizi yako kwa kununua nguo za mitumba, kulima au kufanya vibarua vidogo vidogo? Je, wajua kupanga bajeti ya nyumbani? Jifunze. Je, kuna mashirika yanayotoa misaada fulani, kama kusomesha watoto? Peleleza utapata habari na maarifa ambayo hukuwa nayo.

Mkopo uje kama jambo la mwisho, labda kwa ajili ya mtaji. Epuka madeni kama ukoma, uwie watu upendo. Ila wakati mwingine waweza kupata mkopo au ruzuku ili uweze kuongeza kipato. Usizoee kutumia credit card! Ishi maisha rahisi, nimeona hata nchi maskini watu wakijenga majumba makubwa ya kutisha, yenye vyumba vingi, watoto wakienda mtu abaki kufuta vumbi. Hata wale wanaompenda Mungu wameingia ansa hii ya vitu (stuff).

20. ***Hivi kuna faida gani ya kuwa na watoto, maisha ya kulea siku hizi ni magumu?***

Ni kweli uzazi ni gharama na kifurushi chenye mengi magumu. Mwenyezi alitupa amri tuzae na kuongezeka. Tuliumbwa hivi. Mwulize yule anayetamani kuwa na mtoto, utakuwa na picha kamili.  Ni kweli uzazi na kulea si kazi rahisi' ila katika jamii zinazopenda kuwa na watoto sana ni Waafrika; hata kufikia hatua ya kuachana kama mke hazai! (Si mume asipozaa!). Kwa walio na watoto wanaojuta ni wachache sana. Wengi mlipenda mzae na mmefurahia watoto wenu.

Jiulize, hivi Mungu Mwenyezi, alituumba kwa sababu gani? Ili tumsadie kazi? La. Ni kuonyesha upendo na utukufu Wake. Wengi wamepata faida kuwa na watoto. Angalia yale mema ambayo watoto wanakutendea hata kama hawakupi kitu. Watoto ni urithi toka kwa Bwana, anatupa kama zawadi kwetu. Wengi nchi zingine wameamua wasizae na hilo kwa nafasi chache ni sawa, zungumza na mwenzi Wako akikubali. Hata hivyo maisha ya Manabii kama Henoka waliweza kumwelewa Mungu zaidi walipokuwa wazazi na kujua upendo wa Baba Mungu, kuna Vingi tunavyojifunza kama wazazi, mfano uvumilivu, kutojifikiria, upendo n.k. baada ya

kuzaa tabia zangu mbovu zilijitokeza zaidi, naomba Mungu anisaidie niziungame na kuziacha.

22. ***Kuna haja ya kumfundisha mtoto mambo ya imani? Je, haitakuwa kama kumlazimisha?***

Ni muhimu sana mzazi kumfundisha mtoto hasa kwa muda unaofaa wa utoto. Mema na mabaya na amri za Mungu lazima zifundishwe, na mtoto akikua anakuwa na uchaguzi mwenyewe. Mtoto anazaliwa na uchoyo na kujifikiria anakuwa na mawazo ya kumfuata Mungu na kumfuata shetani. Mtoto anazaliwa katika pambano la wema na ubaya. Hazaliwi akiwa mzuri; ila pagani. Hivyo anafundishwa kumjua Mungu. Ni kumrithisha mtoto umasikini usipomweleza kuhusu muumba wake.

Miaka saba ya mwanzo mfundishe mtoto upendo wa Mungu, neno la Mungu, kuomba, nguzo za imani, furaha ya kumjua Mungu, imani na uzuri wa Mungu. Ampende Mungu na jirani, ajikane na kutawala nafsi pia kutii (submission). Asiwe mchoyo, asiwe msengenyaji na tabia zile mbovu. Atii wazazi. Amheshimu na kumtii Mungu katika mali yake, kusujudu, kutokuwa na kiburi, uaminifu, kutunza siku ya Bwana, kutokuwa na tamaa ya mali n.k.

23. ***Unaonaje kuhusu TV; Je, wazazi watawale mambo ambayo watoto wanatazam?.***

Asilimia kubwa ya TV ni mambo yasiyosaidia kabisa. Maoni yetu ni kwamba, kama utaweza kuitoa kwako itasaidia! Au uwe na mikanda ya kusikiliza maana hata matangazo ya biashara yanaanza kuwa na watu waliovaa nusu nusu, ujangili,ukatili, uovu au kukosa adabu.

Watu wameona kwamba ukatili mwingi unaongezwa na watu wengi kutojithamini. Historia ya Hitler wa Uerumani ni mfano mzuri, alitaka kuwabamiza wengine kutuliza hasira zake. Shetani amejiinua pembe zake akitaka ateke watoto wako na kuchukua muda wa familia yenu na pengine hata afya zenu. Kama unataka kushughulikia TV sana, chukua kalamu na karatasi uandike programu zote, unazotaka watoto waangalie, na uwepo kuona yametimika hayo matakwa yako.

Nchi nyingine zina channel mia tisa! Watoto wanaamka usiku wazazi wakiwa wamelala na kutazama mambo ya ajabu! Vikatuni vyasema maneno ya watu

wazima na matusi. Pima haya kwa makini na zungumza nao. Pata ushauri pia. Usiwe dikteta.

24. ***Mimi ni kijana wa miaka kumi na mitano, nimeambiwa nitakuwa na mabadiliko ya kimwili ila siyaoni! Ni yapi hayo?***

Yatakuja tu, subiri. Mifumo mingine ya mwili yaweza kuwa na hitilafu hapa na pale ila mfumo wa uzazi ni nadra sana usifanye kazi. Kuna tezi yaitwa pitituary gland ndani ya ubongo wako, ambayo ina ukubwa kama harage. Hii ndiyo Bosi (master gland) ya tezi zote; inaongoza tezi zote na hata ile ya uzazi kufanya kazi. Mtoto asiyefahamu, kama msichana aweza kufikiri ni uvimbe. Mwili unajitayarisha kwa uzazi. Mwili utaanza kukua upesi (rapidly). Nywele kutokeza kwenye kwapa, na kwenye sehemu za siri. Nywele hizi, zinasaidia kupunguza unyevunyevu na harufu. Misuli kujengeka zaidi kwa wavulana, sauti kubadilika, ndoto nyevu na ndevu huota. Viungo vya uzazi vitakua.

Mara nyingine katika kupevuka uchovu unatokea kwa ajili ya mabadiliko mengi, pata usingizi vizuri angalau kwa masaa manane. Kula vyakula bora.

Kwa wasichana maziwa hukua, kuvunja ungo,, damu kutoka kila mwezi kupitia uke, kila baada ya wastani wa siku ishirini na nane. Hii ni kutayarisha mimba kutungwa na isipotungwa damu inatoka baada ya mishipa kubomoka na kutayarisha mfuko wa mtoto tena kwa mwezi ujao.
Mabadiliko mengi hutokea baada ya miaka kumi na miwili kwa wasichana, na kumi na minne kwa wavulana. Japokuwa nyama na maziwa siku hizi yana vichocheo vingi (hormones) ambavyo hufanya mwili kukua haraka na kuleta mabadiliko kwa watoto pungufu ya miaka kumi!

Usafi wa moyo na ngono ni muhimu (purity ya mawazo, matendo na maneno)Wengi wanaogopwa kuchekwa hasa wasichana wanakuwa na aibu, self conscious, la, hasha hautachekwa. Hakuna ambaye anafikiria mambo yako sana. Ila mzazi au mlezi, ni vyema kwa maarifa na vifaa, akupe pamba ili ujitayarishe kujitunza vizuri ili nguo zako zisichafuke. Pia akufundishe namna ya kuweka hiyo pamba, kubadilisha na mahali pa kuitupa na usafi kwa jumla. Usiitupe kwenye vyoo vya kuvuta. Kwa wavulana, wembe wa kukata ndevu na kadhalika.

Wengi waweuliza kama wanaweza kupata mimba bila ngono. Kamwe haiwezekani. Labda hospitali wanaochukua mbegu ya wanaume na kuipandikiza,

*kama inavyokuwa kwenye ngombe wa kisasa . Kuna hofu za kupevuka; hebu mzazi/mlezi ujadili jambo hili kwa undani zaidi. Tawala tamaa zako, japo umepevuka si wakati wa kuwa na rafiki wa jinsia nyingine (boyfriend/girlfriend). Jihadhari na urafiki wa namna hii uwe wa wazi au siri. Tumia nguvu na mawazo yako zaidi kujifunza kazi, maarifa na ustadi na kumjua Mungu. Chagua marafiki vizuri, wanaomcha Mungu. Usisikie dhamira kukushitaki ukifikiri ngono 'hapa na pale' ni kawaida ila usiweke mawazo yako katika hayo. Ikifika wakati wake utakuwa wa kawaida tu na wala si rahisi kuwa na dilema wa nyanja hii.*

Wengi wanaona aibu kutoa nguo kwenye ofisi ya tabibu, mara nyingi huna haja ya kuogopa na kama unataka mzazi wako aandaamane nawe fanya hivyo. Zawadi kubwa utakayompa atakayekuoa au utakayemwoa ni ubikira wako uwe mwanamume au mwanamke. Usafi wako wa mwili ni muhimu sana. Zaidi ya asilimia sabini ya vijana wamefikia siku ya ndoa wakiwa wamefanya ngono na watu wengine! Ila Mungu ni mwenye huruma sana anatusamehe pale tumekosa, ila tuanze safari mpya ya usafi/uaminifu wa moyo, matendo na maneno..

25. ***Nina mzazi ambaye anakuja kwangu na kutaka kuendesha nyumba yangu, na jinsi ninavyolea watoto wangu. amekuwa mzigo moyoni mwangu. Nifanyeje?***
Kila nyumba ina shida zake. Jaribu kumzungumzia, na muweke mipaka. Wewe na mume Wako mjadiliane na kumwambia kwa upendo, kama anakaa nanyi nyumba moja, basi ni bora mtafute jinsi ya kumsaidia ajitegemee,

26. ***Nina umri wa miaka 14, na napenda kuvaa kama wengine wa rika langu, ila wazazi wangu wanasema kwamba ni muhimu niangalie kama mavazi haya ni ya adabu, ya kumweshimu Mungu na watu. Naonekana kama nimeachwa na basi na fasheni hizi za kizee!***

Mara nyingi tunapungukiwa na kujithamini kwa kujifananisha na watu wengine. Unajali ukichekwa. Utakapokuwa mtu mzima, haya yatapotea kwa kujua kwamba hakuna anayetaka sana ufanane naye, na pia unahitaji kuwa na msimamo

au uti wa mgongo kwa mambo mengi! Huwezi ukawa unakopi yale yasiyo mema kwa vile unataka kufanya kama wengine! "kila mtu anafanya hivyo." Acha 'everybody' afanye, wewe siyo 'everybody.'

Jifunze kujitegemea na kwa kutofurahisha watu kwa mabaya bali kwa mema. Pata maarifa ya kupata marafiki wema, sio lazima wale mashuhuri, ila wale wa tabia njema hata wakiwa wachache au bora kukosa rafiki kuliko kuwa na rafiki wabaya.

28. ***Nina binti wa miaka kumi na saba. Anataka kuvaa sidiria ila hana maziwa; je, nifanyeje?*** (jinsi ya kushugulika na matatizo yanayopata watoto).

Kwa vile anataka kufanana na wengine, au kuwa mtu mzima na anapata hofu kwa mabadiliko ambayo hayakuja kwake haraka kama inavyotazamiwa. Hamna ubaya kumnunulia avae. Wakati huu mtoto anakuwa hajiamini, au kujipunguza thamani. Wengine wanajiona wanyonge au kujiona amekataliwa na rafiki zao, na hukata tamaa.

Mzazi afundishe watoto kujithamini maana mara nyingi watoto wana ukatili wa maneno na kucheka wengine. Mfundishe jinsi ya kujitoa kwenye moyo uliopondeka, mwonyeshe kwamba anapendwa na kuthaminiwa nyumbani. Mtoto ajue pia kwamba hawezi kufuata wengine katika kuvunja amri au kutotii. Kumbuka, kama mzazi huwezi ukawatatulia matatizo yao yote. Wajifunze kutatua shida za mazingira yao. Mtoto anakuwa na magumu kiasi fulani ambayo anaweza kutatua. Hutamrukia viunga vyake vyote!

Miaka ya viunga inaleta mtoto kukomaa, kuwa mwenye uvumilivu, huruma, ushujaa, ushindi. Mti usio na mizizi unaanguka kirahisi upepo au mafuriko yakija. Watoto waliojifunza kutatua matatizo wanakuwa na ulinzi (security). Huko kutoa matatizo yao yote, ila kuwatia moyo, kuwakinga katika madhara makubwa, kuwapa nyenzo za kuruka viunga na kuwaonyesha uko upande wao.

29. ***Nitajuaje kama mtoto wangu atumia madawa ya kulevya?***

Ataonekana kuchoka na kukosa malengo (ambition), kuzorota kwa kazi ya shuleni, kutotilia makini vitu, kutowasiliana na familia au wenzake kwa ufanisi. Kutojali hisia za wengine, sura kubadilika, kama macho kuwa mekundu, au macho

kucheza cheza, kutojali usafi wake, na kubwatika kwa kuonywa mambo madogo madogo. Pia atapendelea kukaa mwenyewe wakati wote, kuwa na marafiki ambao hataki wajulikane, kula mno, magomvi, na kuwa na harufu ya vileo. Maadili huvunjika, pia anakuwa na alama za sindano kwenye mwili, kuwa mtu wa siri kupita kiasi, kupotea kwa pesa au vitu vya thamani nyumbani na anaweza kuharisha.

Watoto wengi wameshajua madhara yake ila endelea kuwaambia tu na kuendelea kutafuta ufumbuzi. Zungumza nao kuhusu msukumo wa rika pia, na kuwa shujaa wa kusimama peke yake siku moja! Mzazi uwe mfano, ili nawe usiwe na msukumo wa rika, wa kuigaiga na kutaka kuwa na vitu kama au kuvaa kama watu wengine. Kuna watu wazima wengi ambao bado, wanataka kufanana na watu fulani. Hebu tuige mfano wa mashujaa waliosimama wenyewe, maana kuna wakati ambapo inabidi usiende na kadamnasi.

30. ***Mtoto wangu anapenda kukusanya miti, mimea, wadudu na wanyama, nifanyeje?***

Akiviweka chumbani kwake, kwa unadhifu na bila kuleta madhara au harufu mwache aendelee, kwani huu ni umri wa kukusanya vitu. Ataokota kila kitu anachopata njiani, kama makopo, waya, vifuniko vya chupa, n.k. Mpe box awe anaviweka au mwelekeze mahali pa kuviweka. Kamwe, usivitupe.

31. ***Binti yangu wa miaka kumi na sita, ambaye hajaolewa, ameniambia ni mjamzito nifanyeje?***

Binti yako anakuhitaji sana sasa kuliko awali. Uwe mwenye upendo; kaa mzungumze. Siyo wakati wa kusema "Nilikwambia;" na kugomba ovyo ovyo. Mara nyingine mahusiano yenu yaweza kujengeka baada ya hii shida kuliko awali, mkashikana zaidi. Aliyekosea mara nyingi huwa mnyenyekevu. Msaidie na mwenzi Wako (mume/mke) mambo ya kutunza mtoto na arudi shule kama anaweza, ili aweze kuwa na riziki njema zaidi baadaye. Mkae na kuzungumza kwa undani, baada ya kujifungua; kwa maana tabia hii imeonekana kujirudia kwa wasichana wengi, hata wanapataa watoto kadhaa nyumbani kwao. Akiwa mtu mzima ana uchaguzi wa usafi na kutunza amri, ila achukue majukumu ya kutunza watoto wake. Baba wengi wamekuwa na magomvi na wake zao "unanificha mambo ya binti, mlifanya

naye mipango ya kupokea mahari eh?'' Jaribu kuyaweka wazi kwa mume Wako, na muwe na rehema.

32.***Umesema kupiga mtoto wa umri wa zaidi ya miaka kumi na miwili si vyema, apewe adhabu gani basi?***

Angalia kwenye mambo kama posho ya pesa (pocket money) na mengineyo ambayo waweza kuyapunguza. Pia unaweza kumground mahali kama kwenye chumba chake, au nyumbani, umwambie asitoke kwa muda fulani. Adhabu hii ni nzuri kwa watoto wa rika hili. Angalia hata wale wadogo sana inabidi kuwaadhibu bila kuponda roho zao (damage spirit). Elezea mipaka vizuri (define boundaries). Usifoke kwa kumwaibisha; ''Mbona maksi zako mbaya kuliko za mdogo wako,'' au ''mtoto mjinga hufai kitu.''

www.ngj.org au soma gazeti la No Greater Joy.

33. ***Binti yetu amekuwa akiona aibu siku hizi; akivaa huwaambia dada zake watoke chumbani!***

Mabadiliko ya mwili yafanya atake faragha (peke yake) mpe nafasi, mara nyingi ni kitu cha muda mfupi tu.

34. ***Je, watoto wanapevuka mapema siku hizi?***

Ni kweli; kwa urefu na mabadiliko ya mwili. Katika nchi ya Marekani, miaka ya 1850, mtoto alivunja ungo akiwa na wasitani wa miaka kumi na saba. Miaka ya 1950 wastani ukawa miaka kumi na mitatu, na sasa ni wastani wa miaka kumi na miwili.

35. ***Mtoto wetu wa miaka kumi na mitatu anaona aibu kuonekana nami mzazi, nimemzaa na kumlea na kumtumikia maisha yote na sasa ananionea aibu hasa akiwa narafiki zake! Je, nikubali hili au nilipinge?***

Miaka kumi na mitatu hadi kumi na minne ndiyo migumu sana. Watoto wa umri huu wanapenda mno kuonekana kama ni watu wazima, na wanajitegemea na huona aibu kuonekana na wazazi. Lione jambo hili kama la kawaida katika kipindi hiki; labda kuwe na harari. Mahusiano yako na mtoto yatarudi. Japokuwa si kama yale ya utoto udogo.

36. ***Je, nivae na kuzungumza kama mtoto wangu teenager ili aone kwamba namwelewa?***

Hakuna ujinga kama wa kujifananisha na mtoto ili uonekane unamwelewa. Je, mtoto wa miaka miwili akijiangusha, nasi tufanye vile? Waweza kuonyesha uelewaji wako kwa kumkubali kwa njia nyingi tofauti. Kwanza yeye anataka kutofautiana nawe, awe pekee. Ukianza kumfuata ataabadilisha staili! Usimwigize, bado anahitaji mamlaka yako, na wewe ndiwe mwenye kumwongoza! Hatufuati mfano wa watoto, ila watoto ndio waige mzazi ambaye naye amwige Mzazi MKUU yaani MUNGU. Hii inamaanisha maagizo, amri, mausia na shuhuda za MUNGU.

37. ***Mtoto wangu wa miaka kumi na minne ameanza kutuonyesha wazi wazi, kuvunja sheria na kuchukia familia. Anatuchukia tukimwadabisha. Anakuja amechelewa bila kuomba udhuru, tufanyeje?***

Ni vyema umchukue kando siku tofauti na anapoanza vituko. Nenda naye kutembea, mfano, kwenye kiwanja, mgahawa n.k. Mwambie kwamba una mambo dharua ya kuongea naye. "Naona mabadiliko yanatokea nyumbani, umekuwa na hasira, ujeuri, mimi na mama yako tunajikuta pia tunafadhaika na kukemea. Huu si mpango wa Mungu kwetu au kwako. Je, kuna njia bora ya kutatua haya matatizo?, Ndiyo maana tuko hapa leo." Mweleze unajua mabadiliko ya mwili wa ujana, kuna misukumo. "Umeonja uhuru na unataka kula, kutembea, na kuvaa unavyotaka. Tunajua unataka kuwa bosi wako mwenyewe na watu wasikuingilie. Muda si mrefu utakua, utajitegemea na utaoa. Kwa sasa hujakua bado. Kwa miezi kadhaa umetaka kutuonyesha na mama yako, kwamba umekua, na hutaki kusoma, kufanya kazi au kuja wakati unaotakiwa. Ni rahisi kwetu kukuacha ufanye utakavyo, ila tunajua tutajuta nawe pia utajuta. Una wadogo zako wanaokungalia na kuiga mifano ambayo itaharibu maisha yao ikiwa tutaacha ufanye utakavyo. Sisi tu mawakili wa Mungu soma 1 Sam 12: 22, 25:27 –34. Mungu alimwadhibu Baba Eli na watoto wake kwa sababu ya tabia yao mbaya." (Angalia kwenye neno mifano mingi mingine).

"Mungu hatatuhesabia kwamba hatuna hatia kukuachilia vile. Nataka utuahidi kwamba utakuwa mwangalifu kwa mambo haya; 1, 2, 3, nasi tuendelea kuwa waangalifu kujali maslahi yako. Utakapohitaji kitu na kutuuliza tutaangalia kama umekuwa mwangalifu kuyafuata haya. Tunajua wewe ni mtu mzima na

kwamba hatuwezi kutumia kiboko, ila kuna mambo ambayo hatuwezi kuyaachilia; (cant be compromised); hata kama ukipiga kelele na kufanya ujeuri. Hutaki tukae usiku mzima tukipembua njia za kukufanya ukose raha, maana zipo!''

" Nahitaji kufanya kazi yangu kwa umakini hii miaka michache ambayo upo nyumbani. Ni juu yako sasa. Twaweza kuwa na amani ukishirikiana nasi na kufanya miaka michache uliyobakiza kuishi nasi iwe ya amani. Yabidi urudi nyumbani mapema, kujituma kazi na kumweshimu mama yako na mimi. Tunakupenda kuliko unavyoweza kufikiri. Tunataka kudumisha urafiki kwenye dunia ya machungu mengi. Hayo machungu mengi hujayafikia ila kuna siku lazima utayaona, tunahitajiana (we need each other). Tunakuhitaji, na hata nawe, amini usiamini watuhitaji hapa na pale. Tusaidie, tukusaidie tusidondoshe mpira.'' Kisha muulize;
"Je, una lolote la kutuambia?'' Mpe mtoto muda afikiri. Hata kama kijana wako awe na hasira au asijibu, umemweleza hali ya hewa na mategemeo yako. Yawezekana kuwaelekeza vijana bila kuwazungumzia kwa ujeuri. Kuwa mwema kwake, na mwelezee wigo.

42. **Kwenye mazishi ya mjomba wa watoto wangu watoto wameniuliza kuhusu mauti, niwajibuje?**

Neno la Mungu limetuonyesha kwamba mtu akifa analala kaburini kungojea ufufuo. Martha, dada yake Lazaro alisema, "najua siku ya mwisho lakini sasa ananuka yangu ". Jitahidi kumweleza mtoto ukweli , na kama hufahamu mwambie unapeleleza au hufahamu. Martha Akajibiwa na Bwana "MIMI ndiye ufufuo na uzima!'' Bwana akija na parapanda ikilia, makaburi yatafunguliwa na wafu watatoka makaburini, na wala si mbinguni, kisha watapaa kumlaki YESU mawinguni. Neno la MUNGU halisemi YESU atakuja na jeshi la wale waliokufa na kuwa huko mbinguni, bali linasema atakuja na jeshi la malaika.

Bwana Anakuja afufue, kama wako mbinguni tayari, hakungekuwa haja ya kuja. Huu ni ufufuo wa watu wenye haki. Kuna ufufuo wa wale waovu ambao wataenda jehanam kwenye adhabu ya moto uchomao na kuwateketeza. Mungu hajaahidi uzima wa milele kwa waovu kwamba wataungua milele! La hasha, wataungua na kuteketea.

Ni vyema mtoto ajue kuna mshahara wa dhambi na wema. Mtoto apewe nafasi ya kulia, umtulize ila asiambiwe usilie uwe shujaa, kwani imeleta makovu au vidonda vya muda. Atalia kwa siku kadhaa au hata baada ya miezi, hapa na pale

aruhusiwe kulia. Mtoto mdogo ni vigumu kumweleza kuhusu mauti, hata watu wengi wazima hawajui vizuri neno linasemaje kuhusu mauti. Ndiyo maana tumeamibiwa ni fumbo(mystery).

Ni vizuri mtoto aone maiti ya mzazi wake anapozikwa, japo watoto wadogo sana wanakuwa na hofu na kuota ndoto za kutisha usiku. Utapima kama mzazi. Mtoto akingwe na watu wengi wanaopiga mayowe makubwa kilioni kama inawezekana maana inajenga mfadhaiko mwingi. Mtoto aweza kuona yule aliyekufa amemtelekeza, au akasikia dhamiri inamshitaki kwamba yeye ndiye aliyemwua hasa kama alimkasirikia. Msaidie kumweleza mtoto yeye si sababisho la kifo. Mtoto ajue baada ya kifo hakuna nafasi ya kuungama ni mwisho wa maamuzi.

43. ***Mtoto wangu anakuja toka shuleni akilia kwamba amepigwa na watoto wengine. Je, nimwambie ajitetee kwa kuwapiga pia?***

Ni vyema umwambie mtoto wako asiwe na tabia ya kupigana katika mchezo. Watoto wana uchoyo na ukatili mara nyingine, kwa kuwatenga wenzao na kuwasema kwa wazi, kama wana kilema au maumbile tofauti. Watoto wanajipenda, wanalimbikiza vifaa vya kuchezea kwao. Kwa vile bado ni mdogo, mwambie vitu vingine ajihami. Na akipigwa au kuchukuliwa vitu vyake, amwambie mwalimu ili aliyefanya hilo ashugulikiwe. Watoto wenye ukatili kama wale "bullies" angalia website breakingsilencenow; ni vizuri washugulikiwe ili wasizidi kuhangaisha wengine!

Ikiwezekana watoto hawa wapigwe au kuchapwa na wanafunzi wenzao ili wakomeshe tabia hii! Na kisha mwalimu aishugulikie. Mtoto anayependa kupigana atakoma ujinga! Cha muhimu mzazi asisitize ubaya na ujinga wa kupigana ila asimwache mtoto mdogo akipigwa bila kujitetea au kutafuta haki. Watoto wengine wenye nguvu, kwa ajili ya "bullies," wamejifunza karate na mengine ili kuondoa unyanyasaji huu.

43. ***Unafikiri watoto wa miaka mitano waachwe wasikilize muziki wa rap na rock?***

Kwa kweli muziki huu ni mbaya sana kwa ye yote, hata mtu mzima asisikilize. Angalia sura ya muziki na tabia. Tabia mbovu zimezaana kutokana na rap na miziki na sampuli zake. Kwa vile shetani alikuwa mwanamuziki mbinguni, ameshugulikia binadamu wapende muziki wake wa uovu. Miziki hii hatukuwa nayo kwenye tamaduni zetu za kiafrika. Hata mambo ya dansi mengi yanakita kwenye uasherati.

Hata ngoma za kiafrika zilikuwa za heshima na si za kudansi mwanamke na mwanaume wakiwa wamekumbatiana 'milimita moja'. Je kuna mtu angependa mume wake au mke washikane na mtu namna hii?

44. ***Baada ya mambo yaliyotokea Rwanda ya ukabila ya watusi na wahutu na makabila yetu mengine, nifanyeje ili mtoto wangu asiwe na ubaguzi?***

Hakuna litakalosaidia watoto kama mfano wako unavyowatendea wa makabila mengine. Kuwabagua au kuwajali wale walioumbwa kwa mfano wa Mungu. Ubaguzi karibu wote duniani, uwe wa rangi au wa kabila unarithiwa kutoka kwa wazazi, na mara zingine unahusiana na mali, yaani kubagua masikini. Watoto wetu wanatutazama kwa makini, na kufuata nyayo zetu. Mama mmoja wa kizungu aliniambia kwamba siku moja walipoenda kuogelea kwenye bwawa, na waliporudi nyumbani, alimwuliza mtoto wake "mmeonaje kuogelea na watoto weusi" watoto walijibu "kulikuwa na watoto weusi pale?". Kwa maana nyingine watoto hawakujali rangi waliona ni marafiki tu na wakaendelea na michezo. Kwa upande mwingine watu weusi nao wanawashuku wazungu kwamba wana ubaguzi hata kama hawajakaa na mtu au kufahamu nia yake. Ni dhambi kushuku watu kwa yale usiyo hakika nayo. Mama huyu alisema alipata fundisho. Watoto wadogo waweza kuonyesha dharau kwa kutojibu watu wakiwasalimu au kuonyesha ubaguzi kutokana na wanayoona nyumbani. Hata ubaguzi wa jinsia "dada zako watakuoshea nguo zako na kusafisha vyombo, wewe ni mwanamume hapa" anaambiwa mtoto wa miaka nane. Kuna ubaguzi wa dini pia wa kuona sisi ndiyo tuna ukweli wote au wengine wanahitaji kufa sisi ndiyo tuishi maana wao ni waovu. Kuna ubaguzi kwa wazee kwa kuwasononesha na kuwatupia maneno. Moyo umejaa mengi na tunayaleta kwa matendo na maneno yetu. Tusifikiri ubaguzi wa rangi tu bali hata makabila, je tunatenga makabila fulani? Je tunawasema vibaya? Fundisho la Rwanda lilikuwa zito, na limetokea zaidi ya mara moja, hebu tujifunze kujua, tu familia ya Mungu. Somo hili ni refu,ila anzia kufuta ubaguzi nyumbani mwako maana mbali huko utafika baadaye.

***45. Nakuza watoto wawili wa kiume mwenyewe kama mama je watu wa imani yangu wawezaje kunisaidia***?

Kwa kweli kila anayempenda Mungu ni baba au mama wa kiroho. Wanaume waweza kusaidia watoto hawa kujifunza kazi, michezo na mambo ya kiume. Watoto hawa wakiwa na wajomba, baba wadogo au wakubwa pia waweza kuwa msaada. Ni wajibu wa kila mtu kwenye jumuiya ya wampendao Mungu kusaidia malezi "yachukua kijiji kulea mtoto". Mtoto si wa mtu mmoja, hata faida ya mtoto ni taifa , jumuiya na nyumba za ibada pia.

***46 Mtoto anamjuaje Mungu ?,sehemu yangu mimi mzazi ni ipi ya kumtambulisha MUNGU kwake?***

mtoto anazaliwa kama kafiri asiyejua Mungu. Nabii Yeremia anasema " moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha nani awezaye kujua? Mimi, Bwana nauchunguza moyo". Mtoto wa chini ya miaka saba anafundishwa kwa urahisi kuhusu Mungu Muumbaji. Kule Ghana na pengi afrika ni rahisi hata mtoto kumjua Mungu. jina "Mungu" ni Onyame kwame ikimaanisha "Mungu Mwumbaji" mtoto anaanza kumjua Mungu akifundishwa na wazazi toka utoto. 75% wanamjua na kumwamini Mungu kabla ya kufika miaka 10! Na 3% baada ya miaka 50. Nabii Musa alisema  Mungu Bwana ni mmoja nasi tumpende kwa mioyo, nguvu, roho na akili zetu zote. Na maneno anayotuamuru kama wazazi ni kwamba tuwafundishe watoto wetu kwa bidii na kuyanena tutembeapo njiani, tulalapo na tuondokapo, tuyafunge kwenye mkono na yawe utepe wa macho, tena tuyaandike kwenye miimo ya nyumba na malango yetu. Ni muhimu kufundisha watoto amri za Mungu na waone kama tunaishi hizo amri na kukazia kwenye mazungumzo na maisha yetu ya kila siku. Maisha yetu ndiyo mahubiri makubwa kwa watoto wetu. Tusiwe kama mafarisayo ambao waliambiwa "wanayowaambieni yote mafarisayo fuateni, maana wajua sheria mpaka takarakimu ya mwisho ila matendo yao msifuate, maana ni wanafiki". Mtoto mdogo anajua mnafiki mapema tena hata pengine kuliko sisi watu wazima. Watoto wadogo wanachoka haraka, fanya ibada na maombi yawe ya kufurahisha. Kwa vijana leta changamoto, mijadala na maswali. Mtoto akiwa miaka 9 hivi  apaswa kujua kusoma neno la Mungu kila siku na kusali mwenyewe mbali na wazazi. Aifanye imani iwe yake na si wazazi . safari ya maili 1000 huanza na moja, endelea kuomba Mungu mtoto apende vitu vya kiroho na toa Tv haisaidi katu ibada ya nyumbani. Mtoto ajue Mungu ni baba yake.  Wakatoliki wamesema "tupe mtoto kabla ya miaka sabaa atakuwa wetu". Miaka saba ya mwanzo ni muhimu mtoto ajue "amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu. Yeye amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake na moyoni mwake amemwacha Bwana, maana atakuwa kama fukara nyikani. Hataona yatakapotokea mema..Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana Ambaye Bwana ni tumaini lake, maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na mto; na hautaona hofu wakati wa hari ijapo

ni muhimu pia mtoto ahudhurie nyumba ya ibada regulary na ajue kusaidia yatima , masikini na wajane au watu wenye mahitaji ndiyo dini ya kweli, kumpenda Mungu na Jirani. Mpe mtoto majukumu ya kuongoza ibada anapoendelea kukua, mpeleke kwenye makambi ya mafundisho au semina za vijana/watoto.

***47. Napenda mke wangu akae shambani na kuishi na watoto nami nifanye kibarua mjini ili aangalie mashamba na watoto wanakua mashambani vizuri***

mke wako siyo mama yako. Ulipotaka kumwoa ilikuwa kwa kuishi naye si kibarua wa shamba kwanini nawe usilime hili shamba? . Kaeni mjini wote au shambani wote ili mfundishe watoto wenu kazi. Shamba ndiyo mwanzo wa alfabeti za Elimu. Matayarisho ya tabia njema ni rahisi mara kumi zaidi mashambani kuliko mijini. Hata kama kila mwisho wa wiki waenda haitoshi. Mtoto anasaidiwa malezi kila siku. Baba anasaidia kuboresha sana nidhamu ya watoto. Hata hivyo kuishi mwenyewe ina nafasi kubwa sana kukuingiza kwenye uasherati , kutokula vyakula bora, kuwa na maamuzi yasiyojali familia, au kuwa na marafiki wabaya au kwenda sehemu zinazofanya watu waulize maswali. "Mtu atamwacha baba yake na mama yake na kuambatana na kazi au shamba?" si sehemu ya Amri tuliyopewa na Mungu. Kwanini kuoa kama mnakaa mbali? Wengine wasema "sili silali kwa kukufikiri, nakuota", ila wakioa wanataka mke awe bibi majivu tena akae mbali nao, hivi hii ni haki kweli yeye akae mashambani na wazazi wako nawe ukae mjini?

***48. Mimi na mke wangu tunatofautiana, yeye ataka kuwanunulia watoto kila kitu, mimi nasema ni kuharibu watoto wajali vitu na mali kuliko vile muhimu, Mume wangu ataka kuwanunulia michezo ya kompyuta nami sitaki, sasa imekuwa mvutano.***

kwa kweli hata mimi naona watoto wasipewe kila kitu. Wajifunze kujali watu na Mungu na si vitu. Wapunguzie majaribu ya kupenda vitu na kutumia watu ili wapende watu na kutumia vitu. Mara zingine wazazi wananunua vitu kwa vile dhamira zao zinawashitaki kwamba hawakai na watoto ila kila mara wapo barabarani. Hata hivyo dunia yabadilika siku zikija za shida watoto waliodekeshwa na vitu watakuwa na mfadhaiko mkubwa. Matangazo ya biashara yamewekwa kuwatega watoto wetu. Wao hupata pesa ila watoto wetu hupata vitu ambavyo baadaye vyaleta tamaa na huzuni. Wazazi nao wapunguze kununua vitu ili mtoto wenu asiwafuatilize. Ukiwa na ulevi wa kununua vitu utashindwa kusema la kwa watoto wakiomba vitu. Watu wachache sana wamejenga tabia nzuri utotoni wakiwa na vitu, tabia inajengeka vyema ukiwa na vitu vichache na kukana nafsi na kufikiria kuwasaidia wengine pia. Hata babu akimpa zawadi mara zingine Ancona ni haki yake na hawashukuru. Vitu vingi vinapunguza ubunifu wa mtoto pia, apaswa ajue kutengeneza gari, mwanasesere au vitu vingine vya kucheza atafurahia muda mrefu ila kama ameletewa baada ya muda anavichoka na kuvitupa huko na kule na kufanya wewe uwe bibi majivu wa kufagia mabaki au makaratasi yaliyofungiwa toys.. Kwa upande wa chakula peremende na vingine vyafanya akose hamu ya chakula wakati ukifika. Vitu vingine mtoto anyimwe ili aweze kuvithamini! Na

vingine anapokuwa mkubwa avifanyie kazi , akitoka jasho hataviomba omba kila mara

***49 Nimeambiwa kuwanunulia watoto michezo ya bunduki au mikuki ni kufanya wawe makatili***

Kwa kweli ukatili mwingi unatoka na kuangalia Tv na vitendo vyetu wazazi au walezi, unyanyasaji au mtoto kuchagua kuongozwa na uovu. Wakati ukatili unaonyeshwa kwenye runinga unafanya moyo, uende mbio, macho yacheze cheze, midomo kukauka na viganja kutoa jasho. Watoto wadogo wakicheza mchezo wa vita ni sehemu tu ya maisha ya kuonyesha yanayoendelea kila siku. Mchezo kwa watoto ni "sehemu ya maisha ya kila siku yakiigizwa". Mara nyingi haina madhara labda mtoto huyo awe na nia ya kushugulikia hizi silaha(toys) kupita kiasi kwa hisia zisizo za kawaida.

***50 Nasikia vibaya kutoa adhabu kwa mtoto najiona kama nitakuwa dikteta au mtu mkatili.***

Ni kweli kama wazazi mara zingine tunatoa adhabu bila haki. Ila bado kama wazazi tumepewa ili jukumu na Mungu na tuna uzoefu kwani kule wanakokwenda sisi tumepitia. Ni kweli kwamba sina hekima zote wakati wote ila nina upendo mtoto wangu awe na tabia njema. Upendo wetu na adhabu zetu zapasa zitoshane. Kama una lita moja ya upendo basi na adhabu iwe lita moja. Usimpe adhabu mtoto ambaye humpendi! Labda iwe katika mazingira Fulani tofauti. Ukiwa mkali na kutoa adhabu kupita kiasi, mtoto aweza kuwa na hofu na asiwe mwenye kujitegemea kwa fikira zake na ukimwachia awe kisultani kidogo waweza kuona aibu kwenda naye mahali maana atakuaibisha. Usiruke mipaka kwa adhabu nyingi au kudekesha kwingi. Mtoto anakuwa na wigo akiwa na sheria na adhabu, na anajisikia salama. Angalia babu/bibi wasimwache mtoto wako kufanya yale ambayo yataharibu nidhamu. Mweleze mtoto tendo lake baya na kutotii kwake ndipo umpe adhabu. Usitoe adhabu au usiadilishe kwa hasira. Kama mtoto ana hasira msaidie jinsi ya kutoa hasira yake kwa njia ambayo haina madhara. Mtoto mara zingine anatingisha kibiriti kuchunguza ni nani mwenye mamlaka! Jielimishe ili utumie mamlaka yako kwa hekima na upendo

adhabu mara zingine inamwokoa mtoto wako ili mbeleni asipate adhabu mbaya zaidi, wengi wamesikia kisa cha mtoto aliyekuwa na tabia ya kuiba akimletea mama yake alichoiba. Alipokuwa mtu mzima aliiba na kuhukumiwa kifungo cha miaka

mingi, alipoulizwa kama anataka kusema kitu, alisema naombeni mumlete mama yangu hapa nizungumze naye. Mama yake alipoletwa alimwuma sikio na kusema 'mama yote haya yamenipata kwaajili yako, nilikuwa naiba nakukuletea ila hukunikanya, leo naenda jela, wewe huendi, ni haki hii?@.

**51. Je! kumpiga mtoto kiboko ni kumnyanyasa na kumponda roho kwa kumkatisha tamaa na kumfanya apungue thamani machoni pake?.**

La hasha, watoto wanatofautiana kuna wengine ukimkazia jicho tu atapata hofu, atalia na kujisahihisha na hatarudia kosa. Ila wengine ni lazima wapate kiboko. Narudia upendo wako na viboko vyako vitoshane! Moja isipite nyingine. Usipige na hasira. Kama huna upendo usifanye biashara ya kupiga mtoto! Kumpiga mtoto ni kumsaidia awe bora ni tendo la upendo si la kumalizia hasira zako. Watoto wengi wameumizwa hata kuuwawa kwa viboko. Wengine wana makovu mengi kwaajili ya watu waliowapiga kumaliza hasira zao. Watoto wengine wameulizwa "kazi ya mwalimu ni nini?" wakajibu "kupiga watu viboko, hata mimi siku moja nitakuwa mwalimu nicharaze watu".

Mtoto awe zaidi ya mwaka mmoja, na asipigwe kwa nguvu umri huu mdogo mkononi. Tabia ya kupiga watoto matakoni ni ya nadra na soma zaidi kabla hujafanya hivi. Mtoto mkubwa kuanzia miaka 12 awe na adhabu zingine na si kupigwa. Watoto wapewe nafasi ya kupumua na kukua kwa upendo. wazazi wengi wamesema usipige mtoto na mkono maana mkono wa mzazi ni wa upendo, upige na kiboko na kisiwe kikubwa. Kupiga makofi ni hatari kwa viungo vya mwili usoni au makonde ni hatari kwa kichwa. Makofi kwenye mikoni ni tofauti. Lazima vipigo vilete maumivu ili kuleta tofauti, ila maumivu yasiwe makubwa ya madhara. Mpige mtoto baada ya tukio na mweleze sababu na umpige bila hasira. Kwa wazazi wengine imewasaidia kuomba na mtoto baada ya adhabu. Mtoto mdogo aruhusiwe kulia kwa dakika chache. Mweleze unampenda hata umkumbatie ila tabia ile siyo nzuri. Neno la Mungu linasema ;"mwanangu usiyadharau mausia ya Bwana wala usizimie moyo ukikemewa naye. Maana Yeye ambaye Bwana ampenda humrudi Naye humpiga kila mwana akubaliye.. mwana yupi asiyerudiwa na babaye? Msiporudiwa mmekuwa wana haramu wala si wana halali. Kila adhabu kwa wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha bali huzuni, lakina baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani". Basi mzazi anachukua nafasi ya Mungu hapa duniani kumwadili mtoto.

### *52 Hakuna kinachoniudhi kama watoto wangu wawili wa kiume kugombana kila mara, je nifanyeje na magomvi yao*

Ni kweli inachukiza wakina mama wengi hasa kugombana gombana, kuamua. Watoto wadogo hawachukiani kwa siri, wanafanya vyote wazi wanakuwa kama wapo vitani. Waweza kuchukua chochote na kumpiga mwingine wanamnyanganya mwingine kitu. Watoto wengine wameendelea na magomvi ukubwani. Mzazi ujue jinsi ya kuamua, Kain na Abel waligombana kabla ya runinga! Haikuchukua raundi baada ya uumbaji. Wivu ndiyo kitu kikubwa. Mzazi aweza kuipunguza hii kwa kutowalinganisha watoto. Usilinganishe talanta, michezo,maumbile ,ustadi au kitu chochote.''mfano huyu hana akili darasani, hajui kupika, hajui kutunza vitu vyake, hajui kuvaa vizuri, au hapangi vitu vyake vizuri nk. Kila mtoto aheshimiwe na kama ana talanta Fulani ikisemwa, sema na ya mwingine pia, maana kila mtoto ana jambo Fulani zuri. Mara zingine watoto wanagombana ili kutaka attention (umakini wako) na kama hushuguliki nao wanaacha. Jaribu kusema "kama mnataka kuondoa furaha yenu kwa kugombana hapa kila siku nendeni kule nje mkaonyeshe ubingwa wenu siyo hapa mbele yangu. Mara nyingi wataacha. Mama asirushe mikono na kuonekana hajiwezi "magomvi yamenichosha mie, hata sijuie nifanyeje, wacha baba yao aje". Mama jifunze kuamua hata ukiwa peke yako, nawe pia una mamlaka ya uzazi. Baba akija atilie mkazo na muwe mraba mmoja. Mara zingine toa adhabu kwa magomvi haya.Weka sheria mfano: hakuna kuitana majina, kila mtu akae kwake, mkubwa asimtanie mdogo, lazima uweke mipaka. Zaidi lipeleke kwa Mungu maana likiendelea ukubwani lina madhara zaidi. Nina mama ambaye ana watoto wa kiume waliofunga ndoa na wanagombana, wala hawataki kuzungumza pamoja. Imefanya watoto na wake zao wasifahamiane kabisa. Adui ana Njia nyingi za kutuibia furaha Ambayo Mungu anataka tuwe nayo asipotuweza kwa hili anatafuta lile.

### *53 Tunataka kuwa na watoto na tunajiuliza wapishane miaka mingapi ili waweze kucheza vizuri*

Kawaida watoto wanaopishana miaka 2 hushindana sana ila wanaweza kuwa na urafiki na ushirika kuliko wengine. Watoto wanaopishana zaidi yamiaka 4 huwa hawagombani sana ni jambo la nadra na laweza kutokana na mmoja kupenda kuburuza mwingine. Ila kupanga kuwa na watoto haitokani sana na hili ila afya ya mama , hali ya maisha na nia yakuwa na mtoto mwingine.

### *54 Mtoto wetu ana wivu na mdogo wake aliyezaliwa na tunaona pengine aweza kumdhuru*

Mtoto attention kwake inapopungua anakuwa na wivu. Kaa uzungumze na mtoto wako kuhusu mtoto mpya mwambie hata yeye alipokuwa mdogo alipakatwa na kusherekewa vile alipozaliwa. Mwonyeshe kwamba upendo wako kwake haujapungua. Watoto wengi hawawezi kueleza wivu wao ila wale wakubwa zaidi ya miaka 5 wamesema " hivi sijui huyu mtoto amekuja hapa kufanya nini? Kwanini asiende akakae na watu wengine". Mwachie muda azungumze mawazo yake, maana mashuguli ni mengi baada ya mtoto kuja na kila mtu anamwacha mkubwa na kumshugulikia mzazi na mtoto. Fanya mengine anayopenda kama kutembea kwenda mjini mwambie "mtoto hawezi kwenda mjini. Mwache akus  aidie kufanya vitu vidogo kwa mtoto kujenga mahusiano. Mtoto baada ya muda atagundua maisha duniani hayana kitovu kwake  tu bali watu wengine ni wa muhimu pia. Jaribu kumlinda mtoto mchanga asidhuriwe pia.

***55 Mtoto wangu hakosi adabu wazi wazi ila hachukui majukumu nifanyeje***?

Tabia za utoto kama vile kusahau vitu, kupoteza vitu, kuharibu vitu,  kutotandika kitanda, kutopiga mswaki, kutopanga vitu vyake si njema.

Jaribu kutafuta vitu vya kusisitiza hivi vitu kufanywa. Usimwite majina kama "mjinga, mvivu au mpoteza vitu". Hautasaidia tabia. Najua hii ni ngumu hata mimi limenishinda mara nyingi, lakini siwezi nikakwambia ikitushinda basi tufanye lile ambalo ni ovu! Msifu mtoto akikumbuka kitu kama kutandika kitanda. Mweleze tabia yake ina matokeo. Mfano; Asipoenda na begi la shule atashindwa kusoma na atarudishwa nyumbani au akichelewa kibarua atafukuzwa kazi, akipoteza nauli ya basi atatembea kwa mguu. Tabia kama hivi zinapojirudia mfano anamwaga maji kwenye sakafu kila mara, je ni uasi au ni mchezo tu. Tabia inafunzwa mengi ili mtoto asisahau,yaandike kwenye ukuta, mfano chukua ufuto, kalamu na peni ukienda shule nk

***56 Nina mtoto wa miaka 4 ana tabia yakulalamika lalamika tu kila saa. Hazungumzi kwa sauti ya kawaida ni malalamishi tu (whining***).

Mwambie mtoto akifanya hili. Pengine amelizoea sana na haoni tofauti.  Pengine ameona sauti hii tofauti ndiyo inayoweza kumfanya asikilizwe.  Mwambie unashindwa kumwelewa kwaajili ya sauti ya kulalama. Mwambie azungumze sauti ya kawaida.  Rudia hili ukisikia sauti hii na utaona matokeo mazuri. Waambie na wengine wa familia wafuate nyayo zako

***57 Je, kusema asante, ni muhimu?.***

Ndiyo mtoto atakiwa ajenge tabia ya shukurani. anayofanyiwa si haki yake ila ni rehema! Hii itamfanya aweze kuwa na shukrani. Pole , asante, naomba, tafadhali, samahani na maneno ya tunu au dhahabu. Ataishi na watu vyema, kama akioa/kuolewa au akiwa na watoto, watabarikiwa na tabia njema, na aweza kuwafundisha wengine kwa mfano wake.

***58 Nina mtoto anayeogopa giza nifanyeje***

Ni kweli watoto wanaogopa giza kutokana na sisi wakubwa au kutokana na hadithi zetu. Matani yasiwe yanahusu giza, mnatembea kwenye giza na kusema "zimwi anakuja huyo" . mwambie mtoto kwamba unaenda kwenye giza ila Mungu yupo pamoja naye kama anaogopa kwamba uovu hufanyika gizani.

***59 Je, mtoto wa miaka 4 aweza kusoma.***

Ndiyo kama ni akili nyepesi kushika, aweza kusoma kwanza kiswahili ni rahisi kusoma maana a e I o u hazibadili ila wazazi wachache wako tayari kushugulika na hawa watoto bila kuonyesha hasira. Kama hautakuwa na uvumilivu acha mtoto akue kwanza ni vizuri kwa macho yake na ubongo kungoja. Usikimbizane na watu wenye mashindano "mtoto wangu asoma na miaka 3" hata akisoma na miaka 3 ataenda wapi? Mfundishe kazi, zile njia za ubongo zihusuzo kazi zinakuza mafikara kuliko masomo . Mfundishe kuvuka barabara, kwenda chooni na kujifuta vizuri, kufunga viatu vyake, kuhesabu mpaka 20 au kujibu simu. Mpatie vitabu au mpeleke maktaba na msomee. Akiwa tayari ataanza kusoma

***60 Watoto wadogo wa darasa la kwanza na la pili wapewe maksi kwenye darasa?***

Kutoa maksi ni kitu ambacho kinasaidia mtoto ila kwa mtoto mdogo wa madarasa hayo, msisitizo uwe kwenye kujitahidi kwake, hata kama kazi yake si nzuri sana ili umtie moyo. Maksi zitumiwe kujenga motisha na wala si kubomoa, na pengine ni nzuri kwa watoto wakubwa kidogo.

***61 Nimeona watoto wengi wanapenda walimu strict au "wakoloni".***

ni kweli walimu wale ambao wanaleta mpango kwenye darasa wanapendwa maana una uhakika wa mipango au kinachofuata. Haitakuwa mshangao. Mwalimu anayependa watoto na kuwa strict watoto wanajifunza zaidi. Darasa likiwa na fujo watoto wanaogopa usalama wao na watoto wengine waweza kuonea wengine. Watoto wengine hawana haki kwa wenzao na wasipokuwa na mwalimu ambaye anasimamia mambo kwa umakini wanaweza kuumizwa. Watoto wanapenda

kutendewa haki wakiwa na mwalimu anayefuata sheria watatendewa haki badala ya uharamia, makelele na uonevu. Mwalimu ambaye anachia uovu uendelee bila kukemea, au taaluma isitiliwe mkazo si mbaraka kwa watoto. Mtoto asiyefanya kazi yake, mwalimu lazima afuatilie na ikiwa zaidi ya mara moja, adhabu itolewe.

***62 Nina watoto ambao hawaleti kalamu wala karatasi wakija kusoma na nikiwaazima hawarudishi***

Nafikiri lazima utoe adhabu kwa hili. Mfano waambie kwamba wakija safari ijayo na wamechukua penseli zako wasimame kwa saa moja wakiandika. Baada ya muda kila mtu atakuja na penseli yake. Kama kuna yule anafanya hili akionekana anasimama, ataona aibu

***63 Kuna umuhimu gani kwenda shule na watoto wanasahau waliyofundishwa?***

Mbali na hesabu, mwandiko na kujua kusoma, shule ina faidi zaidi ya hapo.Ni kweli kuna kusahau ila shule inaleta nidhamu na kujikana nafsi, kukaa kwa muda na kufuata masharti, kufanya kazi, kushirikiana na wengine, kutoka jasho. Hata nyumbani mtoto apewe kazi za kujifunza. Yanayofundishwa yanabadilisha mwenendo, hisia na pia ustadi wa kujitafutia riziki. Kama asipoenda shule, mfundishe nyumbani ukitumia syllabus inayokubaliwa (homeschooling).

64. ***Mimi ni kijana wa miaka 21 nataka kuoa, niko mwaka wa pili chuo kikuu wa shahada ya kwanza na mchumba wangu tukimaliza tu twataka kuingia shahada ya pili, na kutafuta vibarua na tuanze kutafuta kiwanja kujenga nyumba***

Vijana wengi wanapigana vita vingi kwa wakati mmoja (battle with many fronts). Mama, watoto na baba wasoma. Kisha mnataka muwe na vitu vingi. Vibarua mwende na pia mtoto aweza akaja saa yoyote, ni nani atakuwa na muda na watoto? Kila mtu yuko katika high ambition ya kuwa na hiki na kila. Ningeshauri pengine mfanye harusi baada ya kumaliza shule au mkioana msiwe na watoto kwanza. Hata mahusiano ya ndoa yanaharibika kwa tamaa za kuwa na kila kitu na watu hawana muda na mwenzi wake na mwishowe kuachana. Nilitembelea mji Fulani mkubwa hapa kwetu afrika nikakuta bwana Fulani na mke wake wameachana na mama anakaa na watoto. Bwana na mke, ni madaktari wafani mbalimbali. Wamehenya kumaliza shule na nyumba nzuri, magari na vitu, ila wanagombana kwa ukatili mwingi na kuchapana mpaka kila mtu ametokwa hamu na vitu. Walichukua muda kuvipata vitu ila havina maana tena. Wote wana huzuni, kila mtu anakaa kwake, wanagombania watoto, wanafika shuleni na kumwambia mwalimu "akija mume wangu usimpe mtoto! Ningoje mimi". Mtoto akawa mgonjwa

nao wanaendelea na ugomvi. Usitake ujaze vitu vyote duniani kwenye mkono wako! kuwa na furaha ni zaidi ya elimu na vitu, ishi kwa hekima za mbingu ,usitegemee akili zao maana vitu vyote vitakuwa siku moja ubatili. Wazungu wasema "less Is more" yaanni kuwa na vichache ni kuwa na vingi. Vingi ni kama amani, uvumilivu, furaha, kuridhika nk Fikiri hili. Waweza kuonekana umeshinda kwa moja au mawili na kushindwa kwa mengi ya thamani zaidi.

**65. Tuna kijana wa miaka 21 bado anaishi nyumbani ila hakubali mamlaka yetu na hatueshimu. Anavunja sheria zetu nyumbani, anasikiliza miziki ya ajabu kwa sauti ya juu, anarudi baada ya saa saba usiku. Nahofia wadogo zake ambao ni wadogo wanaanza kumfuata na kuvunja sheria pia**

kijana huyu ni mkubwa na kwa vile ana shingo ngumu, hali hii itazidi kuwa mbaya mwaka hata mwaka. Mwiteni na mzungumze naye matakwa yenu na kutaka kwake uhuru . Kutoheshimu sheria kwake kwaonyesha amekua na inabidi mmsaidie akaishi mwenyewe kwa kupanga chumba, kumnunulia vitu vya kuanzia maisha nk. Inakuwa vigumu kumbadilisha mtu mzima au kumlazimisha. Watu wa dini ya Amish marekani mtoto wanakuwa kwenye mamlaka ya mzazi sana na kwa nguvu zote ila akifika 16 anaambiwa uko huru kunywa, kuhama na kufanya chochote unachotaka. Ila ukikaa lazima uendelee kutunza kanuni za maisha. Wanapewa fedha kwenda mjini waanze maisha yao, wanapoenda huko, Wachache sana wanatumia huo uhuru, wengi wanapenda kuendelea na urithi waliopata na wanarudi kwao (Amish wanajali maisha rahisi ya kumcha Mungu. Waishi bila umeme, magari, au vifaa vyovyote vya kisasa, wanatumia farasi, na kulima kwa plau, wanashona nguo zao na kujenga majengo yao wenyewe, wale wa mijini wanaitwa Mennonite). Sisemi kwako ufanye haraka, ila kwa waamish wamekuwa wakifunza watoto na kufanya nao mazoezi ya kuwaachia huru na kuwajengea ustadi toka utoto. Usimfuge mtoto sana unaalika uasi, labda uone mtoto mwenyewe anapenda kushirikiana nanyi vizuri

**66 Kuna watoto wa nyumba nzuri wanakuwa waovu wakikua na wengine waovu kutoka nyumba ngumu ila wakikua wanakuwa wema sana**

kweli hata mama mwingine nilimsikia akiomba "ulimbadilisha Sauli kwa nguvu kuwa Paulo na tabia yake ovu akawa mtu mwema kwanini usimlazimishe kijana wangu kama ulivyomlazimisha Sauli". Hili ni fumbo, kama wazazi tunafanya sehemu yetu, kwa nguvu zote. Kama vile maharamia walivyovunja majengo ya New York World trade center, kwa nia ovu, ndivyo ambavyo wazazi tunapaswa kuwa na nia yenye nguvu na kina ya kunuia katika malezi bora ya watoto wetu. Kama wao walinuia uovu na kuweza, je sisi tunaonuia wema ili watoto wetu wamjali Mwenyezi Mungu

na watu, Mungu hatajibu dua zetu? Usikate tamaa mwombe Roho wa Mungu akusaidia mtoto ampende Mungu sana, na kupenda watu, hata wakiwa na shida omba huruma na kuwasaidia. Mungu naye atampa njozi mtoto, na misheni ya vitu vya kufanya maishani na kisha usongo na nyenzo (Vision, Mission, Passion and Provision).

***67 Vyuo vikuu vya siku hizi, vijana wetu wa kike na kiume wanakaa vyumba vya karibu , hamna masaa ya kuwatembelea kwenye bweni, unaonaje hii tabia kwa adabu za watoto wetu***

Jambo hili linaleta shida za watoto wetu kuwa na maisha yasiyokuwa na usafi. Hasa katika enzi ya mambo ya ushoga, kumekuwa na kuchanganyakiwa, na kusema vyoo vya wasichana na wavulana viwe pamoja na hadithi za ajabu ambazo toka enzi za mababu hatukuzisikia. Siku moja tulitembelea chuo kikuu Nairobi kama chuo na tulipelekwa kwa vyumba vya wasichana tuliowafahamu. Chumba kimoja kidogo sana kama wasichana wawili wana pazia linatenganisha. Msichana wa upande wa kushoto alikuwa amelala na mwanamume wanazungumza nasi tumemtembelea msichana mwingine upande wa kulia! Na usiku wanalala vile pia. Binadamu anakuwa kama mnyama, kulala na mwanamume hapa, na wengine kando hapo. Bafu na choo wanashare . vyumba vya wasichana na wavulana vipo pamoja. Kwa kweli hata tamaduni zetu za kiafrika watoto walilindwa. Hii ni njia ya kuleta ukahaba na uovu. Karibu 70% ya wanafunzi watakuwa wameshugulika na ngono nje ya ndoa kabla ya kumaliza shule. Je unapinga msemo wa wazee "sitaki binti yangu aende chuoni atakuwa malaya, nitakosa ngombe wa mahari?!". Jambo hili limeathiri uaminifu kwa Mungu, kwa watu na hasa mume/mke. Nguvu za ashiki kwa vijana ni kubwa na tena unawaweka vyumba vya pamoja wanatembeleana, na kujamiiana na wengine na kuishi kule.. Kwa kweli ni kufanya jamii ivunjike. Huu ni uovu wa wazi. Kama tumeiga magharibi inabidi tuachane nao. Pengine maisha ya usafi si muhimu katika vitivo vya elimu ila tutavuna tunavyopanda. Napenda kusema kwamba masomo yameingiza wengi kwenye uasheratina dhambi ya ushoga. Ni vyema watu waoane kabla ya kwenda chuoni kama hawawezi kuzitawala tamaa zao. Wengine wanasema sitaoa mapema mpaka nifike miaka 30, kumbe anafanya ngono na hata kuzaa . tofauti ni nini? Kwamba huna ruksa au cheti na maana unafanya yote tayari. Uasherati umeleta mmomonyoko wa mengi katika jamii. Oa au olewa usiseme unaenda chuoni na unashugulika na maisha uasherati/uzinzi.

***67 Je,Mtoto afundishwa kuhusu ashiki(sex) akiwa na umri gani?***

Mtoto mdogo kawaida anaanza kujiuliza maumbile yake akijitazama na jinsia nyingine na kukuuliza maswali. Usishtuke. Jaribu kupembua anachojua na uongezee

hapo. Mfano mtoto wa miaka 6 alimwuliza mama yake tumetoka wapi? Mama alitumia muda kumpa semina kueleza mambo ya uzazi nk kwa muda wa dakika 15. alipomaliza mtoto alisema "nilikuwa nauliza sisi ni watu wa kabila gani, tumetoka mji gani? Wazazi ni vizuri wamjibu mtoto, si vizuri aambiwe na watoto wenzake, au vitabu akienda shule. Usipende kuficha ficha, maana shetani afanya ashiki ionekane ni kitu cha aibu wakati ilipewa kama zawadi. Anza kuzungumza na mtoto pengine uzazi kwa mimea kisha wanyama kama kuku, mbuzi. Pengine ameona haya kwa mimea hivyo uanzie pale. Kuwa wazi na mkweli. Unaanza kueleza pole mambo ya maumbile na unaendelea na somo siku zinavyoenda. Sisitiza usafi wa ngono (purity), mawazo, nia na maneno ya mdomoni. Ngono kama zawadi toka kwa Mungu kwa kuendeleza kizazi, nk. Mtoto wako asiende shule ya bweni kusikia haya kabla hujamwambia atapata hadithi zingine ambazo pengine hazitakufurahisha, labda awe na walimu wanaomcha Mungu na wenye uzoefu na jinsi ya kujibu maswali haya inavyotakiwa. Kwa maoni yangu Mtoto akifika miaka 10 ni vizuri ajue maana hata mashule ya serikali watakuwa wamejifunza mengi! Mfundishe kwa hatua. Somo hili uliendeleze, wengine wamefundisha watoto baada ya kuvunja ungo au kubalehe wakaishia pale, wakashtuka mambo mengi yametokea baada ya watoto kufika miaka 16, kumbe masomo haya yahitaji kuendelezwa kila siku zinapokwenda. Mtoto wakati wa karibu na kupevuka pia unaendelea na somo. Na kumwomba Mungu akusaidie maana siku hizi vimezuka vitu vya uchafu wa moyo vya amalaya wa mapicha na hata punyeto (masturbation) vyote hivi si dhambi tu bali hata vyaweza kuharibu akili za mtoto asiwe wa kufaa kwa jumuia au familia yake, yote haya yasome na kuyaelewa vizuri, zaidi ya yote Mwombe Mungu.

***68 Unafikiriaje kuhusu jezi au unifom mashuleni***

Inasaidia kujenga nidhamu, na watoto wote kulingana. Lazima mtoto awekewe viwango, usipoweka viwango kufeli ni rahisi hasa katika ulimwengu wa mitumba na fasheni. Angalia timu za mpira, wanariadha au wanakwaya ili wafanikiwe jambo la muhimi ni nidhamu. Kuwa na nidhamu na kujikana nafsi ni kupunguza kufanya mambo kiholela. Viwango na masharti ambayo si ya kunyanyasa ni muhimu.

***70 Nina watoto wa darasa la tano ambao saba hawana nidhamu nifanyeje***

Kwanza angalia vile vitabia yao na motisha yake, mara nyingi watoto wanapenda kujionyesha. Waweke katika mazingira ambayo hawatajionyesha. Wengine hata wanapenda wawe nyota kwa kupigwa viboko watoto wote wawangalie! Kutafuta attention, mweke nyuma ya kabati ili asionekane dawati lake likae pale. Akitoka hapo baada ya mwezi atagundua kwamba ile atensheni hapati. Waambie wazazi wafanye kazi nao pia na kutoa au kupunguza runinga. Unapoona hata badiliko dogo

wapongeze na msonge mbele. Runinga ni mwalimu wa mengi pia yasiyofaa, kwamba wanafanya watu wa magharibi aina maana ni jambo zuri.

***71 Watoto wakati wa ibada yao wanafanya fujo, na walimu hawawashugulikii inavyopasa***

Walimu wa ibada ni wa kujitolea na pengine hawajasomea saikologia na jinsi ya kushugulika watoto. Wengine wanafikiri wawafundishe kuhusu Neno la Mungu tu na sio adabu au nidhamu. Watoto waweza kufundishwa na walimu wapate semina. Haiwezekani kufundisha masomo na vurugu bila nidhamu!Hilo si shamba la wanyama (zoo). Ni sehemu ya mafunzo. Pia ni kulikejeli Jina la Mungu kuleta vurugu kwenye nyumba yake "nyumba ya Mungu itaitwa nyumba ya Sala na siyo pango lao wenye vurugu". Utaratibu ni muhimu. Hata adhabu mara zingine inabidi itolewe! Ila kabla ya adhabu jiulize je umewaeleza sheria na wamekuelewa? Je unawapenda kiasi ya kutosha? Je maisha yangu ni mfano mzuri kwao? Je upevu wa umri wao ni upi? Omba na kuzungumza na wazazi wakusaidie, maana hutaki adhabu iwe kali wakimbie nyumba ya Bwana!

***72. Tuna mtoto wa mwaka mmoja, tumesikia kwamba tunaweza kuisisimua (stimulate) akili yake na kuongeza uwezo wake wa kuelewa vitu (intelligence***).

Utafiti wa Dr burton white wa Harvard kwa watoto ulionyesha haya. Miezi 8 mpaka 18 mtoto anaweza akaongeza uwezo wake wa akili kutokana na uzoefu anaopata. Mama ndiye mwalimu mkubwa wa kuleta mazingira haya. Lugha inayozungumza ni muhimu sana. Lugha hii si ya runinga! Watoto wenye mazingira makubwa na kusogea hapa na pale wanajifunza zaidi umri huu. Toka na mtoto nje, shambani, hapa na pale nk . mawasiliano ya familia ni muhimu sana hivyo mnapozunguza nyumbani na maelewano yenu ni mali sana! Mambo matatu yalionekana kwenye utafiti kama muhimu a. Mzazi aliye na mpangilio mzuri wa mazingira, b. anayeruhusu watoto kuwauliza maswali hapa na pale na kuwaletea kuelewa, ucheshi, maarifa na faraja b. wanasimamia nidhamu dede (firm discplinarian) huku wakionyesha upendo mkubwa kwa watoto!

***73 Mtoto wangu wa miaka sita ana nishati za kuruka hapa na pale, mawazo hayako makini dakika moja yapo hapa dakika nyingine pale nilimpeleka kwa tabibu watoto akaniambia nimpe dawa za kumtuliza(hyperactive child) nifanyeje?***

Shida hizi za watoto kupewa dawa za kuwatuliza ziko magharibi zaidi ila zinakuja kwetu afrika. Mtoto aliumbwa acheze na kufurahia, na kukimbia. Ila wakina mama wengi wapo vibaruani na wanakosa uvumilivu wa kukimbia na mtoto na kucheza naye wakija toka vibarua maana wamemaliza kazi moja na wanaingia nyingine. Kazi ya mama ni full time ila haina malipo hata kwa wale wenye watoto wa miaka 10+ wanafurahi wakija nyumbani na kumkuta mama na kumweleza yaliyoendelea shuleni au katika maisha yao. Mtoto wa miaka sita pengine hajakua haraka kama wengine na bado anapenda mchezo sana, waweza hata umrudishe darasa moja nyuma au akae nyumbani akicheza apevuke vizuri. Soma kitabu cha Dr Raymond and Dorothy Moore cha homegrown kids. Mtoto aweza kusubiri asiende shule mapema ukimfundisha kazi ndogo ndogo, na atakapoanza kusoma tarakimu hata akiwa na miaka tisa atazitambua haraka na bila masumbufu. Mara nyingi watoto wakiwa shule wanachuliwa kama kikundi ila ukiwa naye nyumbani kama shule ya nyumbani uko naye peke yenu. Thomas Edison aliyegundua taa ya bulb alikuwa na uwezo mkubwa wa akili ila alionekana hatulii na msumbufu. Mwalimu alishindwa, mama yake alimchukua na kumfundisha hata jinsi ya kufanya majaribio ya sayansi nyumbani akawa mwanasayansi mkubwa anayejulikana duniani

Kuhusu watoto wenye mahitaji maalumu (special needs) pata msaada zaidi kutoka kwa walimu wake, wakuambie vizuri siku inavyokwenda darasani, na ukifika nyumbani nawe ushugulike naye, maana walimu wana watoto wengi. Usikate tama watoto wengi wamepiga hatua kwa kushugulikiwa mmoja mmoja na wazazi wao, hata wakaenda vyuoni. Watoto ambao watu walisema hawatajua hata kusoma. Endelea kumwomba Mungu, ndiye aliyeumba macho, ulimi, masikio, ubongo, na vyote. Kwa wale wenye watoto viziwi, vipofu au bubu. Siku hizi kuna shule na msaada zaidi. Mengi waweza kuyapata kwenye tovuti pia.

**73. Tuna mtoto wa miaka sita na mzito kujifunza vitu darasani tufanyeje.**

Ubaya ni kwamba shule zinaweka miaka na tunafikiri kila mtoto umri Fulani awe darasa Fulani na ajue list ya mambo haya! Kutumia miaka kupima mtoto amefika hapa, ni kurahisisha (convenient) kazi ya mzazi, au mwalimu katika shule ila haisaidii mtoto. Watu hutofautiana na atafika tu pale unapotaka, mpe nafasi. Ni kosa kubwa kumwonyesha au kumwambia mtoto ni "mjinga, hawezi au mpumbavu". Mpe muda, mfundishe vitu rahisi, na mpe uhuru kiasi Fulani. Usijiunge kwenye maonyesho "mtoto wangu ndiyo ana akili, amejua kusoma na miaka 4!". Aweza kujua kusoma mapema ila yule asiyejua kusoma wakifika darasa la saba akampita. Nafikiri mmeona mashambani vitu vingine vinakua tofauti vya kupandwa wakati mmoja! Shule mara nyingi zina paa moja kwa watoto wote, fanya kazi na mtoto

wako na umpe nafasi ya kupumua. Ukisoma zaidi kuhusu ubongo unavyokua tumboni na mtoto akitoka una hatua Fulani na mara zingine watoto wengine kuna ucheleweshe Fulani. Na kama mtoto ana shida ya kweli ya utindio wa ubongo (mentaly retarded) ambayo yaweza kupimwa na watalaam basi usimweke kwenye mashindano ya kawaida.. Endelea kusisimua akili ya mtoto. Urithi wako, mazingira na maumbile ndiyo yanachangia. Mtoto awekwe kwenye mazingira ya kujifunza, mfano atembelee uwanja wa ndege, kituo cha basi, maktaba, mbuga za wanyama au kuwa na wanyama wa kufugwa n.k. kawaida mtoto akiwa na uzito kiasi kikubwa usimweke kwenye darasa la wale watoto wanaojifunza kwa kawaida. Utamfanya awe na mifadhaiko, shida za nidhamu kama kupiga watoto wengine, na kuropoka kwa sauti kubwa au kufanya fujo. Shule za watoto wenye mahitaji tofauti na watoto wengine kwa kuwa na uzito au wepesi mno kujifunza ni adimu kwetu. Kama una uwezo peleleza hizo shule

***74. Tufanyeje na watoto wasiojiweza darasani kama walimu, niliye naye ana IQ ya 120 hawa ni watoto ambao japo wanasoma wanafeli. Na wale wana IQ (urithi wa akili) wa kutosha (zaidi ya 70)?***

Kuna pengi wanafundisha jinsi ya kufanya mitihani (how to take a test) ili kama ana woga wa mitihani umtoke. Pia mtoto afundishwe ufanisi na kasi ya kusoma. Aonyeshwe jinsi ya kusoma kwa ufanisi. Mfano asubuhi sana na si usiku. Usimkejeli mtoto, kumuumiza, na kumkimbiza kama anajitahidi. Mwalimu wa kawaida ni vigumu na watoto 100 darasani. Zungumza na mzazi pia akusaidie. Mwambie kila siku ulichofundisha ili apokee mwenge huu na kuleta nuru kwa mtoto kesho yake. Mzazi akae na mtoto na kusaidia kazi za shule (homework). Zawadi ndogo ndogo zitolewe mfano sh 50 kwa kumaliza hesabu. Mzazi inabidi awe na nidhamu na ratiba, maana mbinu za kushugulika na mtoto ni vizuri zibadilike au ziwe tofauti tofauti. Gari laenda rahisi lenyewe kuliko unapolisukumu. Tafuta motisha kwa mtoto

***75 Mtoto wangu ana shida ya macho na masikio na akisoma anaelewa vitu tofauti***

Mtoto huyu ni vizuri apelekwe kwa tabibu ili ijulikane kama shida yake yaweza kupata muafaka. Watoto wengi hawaoni au hawasikii vizuri wahitaji mawani au msaada wa afya. Kisha umweke kwenye "mstari" tofauti na watoto wa kawaida. Kama mzazi fanya naye kazi nyumbani. Mfundishe na mshugulikie. Hichi ndiyo nimeona wenzetu wa magharibi waliozaa watoto wenye udhaifu Fulani wazazi wanawashugulikia kwa nguvu hata kwenda kubadili katiba za nchi ili watoto kama hawa wapate msaada kwenye wizara ya elimu. Najua nchi zetu ni changa ila wengi wanaendelea kusoma vizuri, wana magari na nyumba kama magharibi, je

tukisimamia haya mengine dede yatatushinda? La tukiwa na kipaumbele na kumwomba Mungu ataondoa viunga hivi. Mtoto wako akiwa kiwete huwezi kumwambia ukimbie na watoto wenye miguu miwili na uwe sawa na wao. Ila akiwa na shida ya kujifunza tunataka akimbie na watoto wengine kwa usawa!. Pengine wazazi hawagundui kwa urahisi au ukamili kama ni shida ya ulema au ni uvivu na ukaidi wa mtoto. Naamini na kuthamini elimu ya shule, na kwamba imeleta tofauti kwetu Afrika, tumeona kazi na maisha wanayoishi wale walioenda shule zamani. Nathamini nidhamu kwa watoto na kutii. Ila mtoto kujithamini ni muhimu usimvunje mtoto moyo, kwa mambo ya shule akakosa kujithamini baadaye ukashindwa kukarabati shida hiyo. Siyo kila mtoto atashamiri na kufanya vizuri darasani kama kawaida ya wengi ilivyo. Kuna kesi chache tofauti. Hapo mzazi wataka upime wako ujue. Mtoto ana haki na utu wa binadamu akiwa ana uwezo wa darasani mkubwa au mdogo. Yeye bado ni mtoto wa Mungu. Ikiwa masomo ya darasani hayawezekani ni vizuri kumtafutia ustadi aweze kukabili mazingira yake. Si kila mtu duniani atafit kwenye mfumo huu. Shahada kisiwe kimungu kidogo. Bora ajue kutafuta riziki na kuwa na tabia ya Mungu.

***76 Mtoto wangu amefukuzwa shule na sijui la kufanya. Mimi mzazi ni mwalimu na nimeomba wanisaidie ili amalize shule, miezi 2 angemaliza, wamekataa. Siku ya kumchukuwa wakaniambia "mwalimu gani wewe unashindwa kumwadabisha mtoto wako" kwa kweli tumejitahidi mno na tunaogopa kuendelea kutumia nguvu mno na kumdhuru. Tunaona aibu kwa marafiki zetu na wakituuliza watoto wenu wanaendeleaje mawazo yetu yanafikiri kwamba wanatucheka. Mke wangu anafanya kwenye picha za xray hospital na ameona watoto wengi wamevunjwa mifupa kwa adhabu na wazazi, sasa naanza kuelewa hawa wazazi walipopitia. Tuna watoto wengine 3 wanatabia nzuri wamemaliza shule, wameolewa na wameenda kwenye miji yao***

Kuna pande mbili za sarafu ya hili. Pengine mzazi alikuwa na shida ndiyo maana walimu walisema vile. Hakumwambia mtoto na kuwaambia "nataka ufuate haya masharti". Au hawakuwa na muda wa mtoto walikuwa kwenye mashuguli, uovu kama pombe, uasherati au kujipenda na ubinafsi badala ya kushuguulikia watoto. Au hawakushika usukani wa malezi vizuri wakati wa udogo.

ila sidhani kesi hii ni shida ya wazazi bali maneno waliyosema walimu hawakudhamiria waliropoka au kutouwa na upendo. Wazazi wengi wamekuwa wepesi kujilaumu siku hizi kuliko zamani! Zamani mtoto akiwa na nidhamu mbaya watu walisema ni mtoto mbaya, na mzazi hakujilaumu sana.

Mawazo mengi yamekuja kwa wazazi hawa, kutoweza kutatua matatizo la mtoto huyu, dhamira kuwashitaki, kutojiamini kwamba wanaweza (lost confidence), kuona

wamemwangusha mtoto, au hawakuweka mfano mzuri, kuona wamechelewa , kuona majukumu ni mengi mno (overwhelmed), kumchukia mtoto na kutotaka kumpa usalama na mwisho Kufikiri pengine kwenye utoto wao walifanya hivi na tabia inajirudia kwenye kioo, au wanalipwa walivyosumbua wazazi wao.

Mzazi huyu asijilaumu na kujihukumu sana. Wazazi tumetwika na kulaumiwa hata na watoto wetu walio na mvi makwao! Mtoto akiwa na akili, mwanamichezo, mwasi, ana sura nzuri, mrefu, kilema, mgonjwa, mnene, mrefu, mvivu tunafikiri au wanatuambia wazazi ndiyo sababishi. Hakuna mtu ataelewa aibu hii ya mzazi aliye na mtoto mwovu! Ila Hata mtoto ana uchaguzi hasa mkubwa wa miaka 17 kama huyu. Wakati neno la Mungu linaandikwa mtoto wa miaka 12 alianza utu uzima. Wazazi hawa wasichukue kama wao ndiyo wanafanya hili mfano (mchungaji mmoja alisikitika kijana wake alipompa mimba msichana kanisani, akaandika barua ya kuacha kazi, kama ndiye yeye alizini akisema kwamba hakusimamia nyumba yake vizuri kama Tito 1:6 ilivyosema. Nafikiri fungu hili ni kwa watoto wadogo. Nafikiri hata Adam na Eva walichagua dhambi na haikuwa shida ya Mungu. Muda umeenda usiendelee kujilaumu, mwombee kwa matumaini. Watoto wengine wanaonyesha uasi waweza kubadilika na kuwa wema tu baadaye na wale walionza vizuri wakamaliza vibaya. Soma kitabu parents in pain by Dr John White au angalia website.

***77. Nilimzaa mtoto nje ya ndoa, mume wangu alipoenda vitani. Mume wangu anamchukia mtoto huyu na hii imenifanya hata mimi nimchukie***

Ukifanya uamuzi wa kumpenda mtoto utampenda ingawa umepitia hapo. Mtoto hana kosa, ni wewe ambaye ulikuwa na uamuzi zaidi ya mtoto. Kama mtoto huyu utashindwa kumpa upendo ni vizuri utafute mtu wa kukusaidia. Mara nyingi wazazi wako waweza kukusaidia ila usipotee kabisa, tuma kwa mtoto zawadi,piga simu na kujua maendeleo yake. Neno la Mungu linazungumza bibi Lois akimlea Timotheo. Ila lazima uwe na uhusiano mzuri na wazazi wako ili mtoto asaidike zaidi. mahusiano mabaya na wazazi yatamuumiza mtoto zaidi. Watoto wakisikia wazazi wako wanakusema vibaya inapunguza nafasi ya ufanisi wa kukuza tabia ya mtoto. Waambie washugulikie nidhamu. Endelea kujenga mahusiano mazuri na kama ni wale wanaokusema vibaya kwa mtoto hawatakusaidia mtoto bali kumwaribu. Angalia wazazi wako kama ni wale wanaopenda kufuata imani yako au vitu unavithamini au dada zako ndiyo mnafanana kwa maadili yenu .Ni nani ajuaye hata huyu mume aweza kukuchoka hasa baada ya kuona hata damu yako unaitelekeza na huyu mtoto akawa msaada kwako siku moja. Angalia pia kama wazazi wako wanakidhi mahitaji yake. Kuna mabibi/babu wengi hawapendi kulea watoto, wanataka kuwa huru au hawana uwezo wa kukabiliana na suala lako. Hili pia ni fundisho la kutoshiriki kwenye uasherati au uzinzi. Mwombe Mungu Msamaha

akusaidie. Usilinganishe watoto pia, wapende wote kwa usawa. Usiwe na wivu wa watoto wengine ukiwaona unasema "watoto wa wengine wazuri, ningekuwa na mtoto wa aina vile, aidha kwa maumbile, visomo, mali au chochote! Huyo ndiyo aliyekupa Mungu mtunze vizuri. Hakuna mkamilifu, na hata hivyo mambo ya dunia hugeuka na kuchuja, hebu chuki yako uiondoe, utafute ufumbuzi, Mungu ni wa rehema anasemehe, na ni fundisho kwetu kwamba dhambi inaumiza. Endapo Daudi angejua kumchukua mke wa Uria ni dhambi ambayo watu wangeisoma miaka 3000 asingeifanya,maana kwa miaka hii yote ametoa mwanya kwa adui za Mungu kulitukana Jina la Mungu.

***78 Inakuwaje watoto wadogo wanajifunza kuzungumza lugha na lafudhi wakati watu wazima twaweza kujifunza lugha ila si lafudhi?***

Wazungu waita hii phoneme contraction au kuanguka kwa sauti. Koo la mtoto mdogo linachukua shepu Fulani ya lafudhi kwa urahisi na shepu hiyo anajengeka na kuwa ngumu kubadilika. Hii inafanya kubadilika shepu ya koo kuwa ngumu na kufanya lafudhi isiweze kubadilika. Hata mamlaka ya mzazi kwa mtoto ni vile, kuna dirisha la mtoto la muda utotoni la kumthamini na kumheshimu mzazi linajengeka. Dirisha hili ni la muda mfupi, baada ya hapo inakuwa ngumu. Wazazi wengi wanatenda kosa la viwango tofauti kwa watoto tofauti. Wa kwanza akizaliwa wazazi wanaweka viwango vikubwa, baadaye wanachoka na kulipua kazi. Wana mashuguli mengi pengine, kila mtoto ana viwango vyake na wa mwisho anakuzwa vibaya kupita wote viwango vikiendelea hivi.

77. ***Nilisafiri kwenye basi na mama mmoja, mtoto wake wa miaka 3 anasumbuka na kupiga makelele, kila abiria alichoka nao. Je mtoto kama huyu asaidiwaje?***

mtoto kama huyu kama ameonekana haumwi, hana njaa wala haitaji kujisaidia, ni vyema atolewe mkazo wa jambo. Mzazi asiwe na tabia ya kurudia rudia , akisema mara moja tu ifanyike, ya pili adhabu itolewe. Mfano toa mguu wako kwenye bomba la maji. Mwambie unahesabu mpaka 3 na kama haujatoka ni adhabu. Mara nyingi wazazi tunapenda kurudia rudia, na mtoto anaona kwamba utarudia rudia ndiyo afanye. Hata hivyo mtoto wa miaka 3 mama huyu angesafiri na vitu vya kuchezea, kuandika au kuchora ili awe na kitu cha kujishugulisha kwa safari ndefu

***79. Tulilea watoto tukiishi gizani na tabia za ulevi, wizi, uasherati, uongo na mengineyo. Sasa tumerudi kwa Mungu na tunampenda Mungu, ila watoto wetu tuliowalea gizani zile tabia wanaendelea nazo na zinapita hata zile mbaya zetu,***

***tukiwaambia hawataki kusikia kama vile sisi tulivyokuwa. Hatutaki wapate shida tulizopata hivi kwanini watu hawajifunzi kutokana na uzoefu wa wengine? Wanatuambia "mnataka tuwe ambavyo hamkuwa?" tunasikitika ila tufanyeje. Tunashindwa kujisamehe***

Hali hii ni ngumu na ni fundisho kwa wengi wetu kwamba Mungu Atusaidie tuishi maisha ya mfano bora kwa watoto, maana mara zingine mzazi aweza kuacha uovu ila mtoto akamzidi kwa ule umaarufu mbaya. Ila tukumbuke Binadamu anapenda uovu hata kama angekuwa na wazazi wema namna gani! Kwa kweli hakuna mzazi ambaye hajutii jambo Fulani alilofanya kwa watoto! Hakuna mzazi mkamilifu. Hata baada ya muda tukiangalia nyuma wote tuna makosa tele. Muhimu kumkabidhi Mungu Atuongoze. Jifunze kujisamehe, na pia mfundishe mtoto kujisamehe na kukusamehe. Dunia ina mazito mno. Mkutano mmoja nilikwenda baba mmoja Steve Chapman alisema alirudisha gari nyuma akamgonga mtoto wake kwa bahati mbaya". Dunia ni ngumu. Jifunze kusahau yaliyopita si ndwele.''Natenda neno moja tu, nayasahau yaliyo nyuma nikiyachuchumilia yaliyo mbele, nakaza mwendo niifikilie ile medali ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu''umkabidhi

mwombe Mungu msamaha maana YeYe ni mwenye rehema " binadamu wote tumefanya dhambi, tumeoza hakuna mwema". Zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni. Chukua muda kufanya tofauti kwa wajukuu wako au watoto wa jumuiya kwa yale mema unayojua ya kusaidia watoto. Kile kilicholiwa na mchwa Mungu Atakurudishia kwa mapenzi yake maana anasikia kilio chako "nitakurudishia watoto wako". Ila usiwe mtu mwenye wivu, malumbano au jazba. Nimeona wazazi wengi waliopata shida hii wakiona watu wengine wenye watoto ambao wamesoma vizuri na tabia njema wanafurahi sana wakianguka na kusema "tumelingana", huu ni uovu. Maana hata wao wakiwa "wabaya" haitasaidia wako wawe "wazuri" bali kuongeza mbegu za uovu duniani. watu wakizungumza watoto wako usiwe na haraka kujibu "wananicheka na watoto wangu, hata wao watakuwa kama wangu tena wabaya zaidi", hii ni roho ya adui na si ya Mungu ya kutaka watoto wa wengine waharibikiwe kwasababu wako waliharibikiwa. Ili Mungu asikie sauti yako kuwa mnyenyekevu anayewaombea watu mema ! "Ukae kimya mbele za Bwana Nawe umngojee kwa saburi usimkasirikie yeye afanikiwaye". ". Mungu ni mwenye huruma, haki na rehema hata Samson mnadhiri alipoteza muda kwa uovu, au mfalme Manase saa ya mwisho walipata kubadilika, ila angalia bahati ya mwenzako usilalie mlango wazi , leo ndiyo nafasi ya kumwamini Mungu ukipata nafasi, na pia ukimwamini toka ujanani utafanya usiwapeleke wengi Jehanam.

***80. Je, waweza kumruhusu kijana wako kiume na rafiki yake wa kike wasiyefunga ndoa waje kulala kwako?***

La. Itakuwa kumvunjia Mungu heshima na kanuni ambazo mimi na mke wangu tumeziwekea msingi. Nitachukuliana na watoto ila si kiasi hicho cha kumhuzunisha Mungu wangu. Pengine naweza kuwatafutia mahali pa kulala kama nyumba ya wageni.

***81. Je kuna wakati wazazi hawapendi watoto wao ?***

Ndiyo ni kama maisha ya ndoa, tabia na vitu vingine vinafanya upendo wetu upungue. Kuna wakati mwingine mtoto anafanya vituko vikubwa, mama mmoja aliniita akasema nifanyeje "sina upendo na mtoto tena". Alikuwa ni mtoto wa miaka 10, aligundulia amefanya vituko vikubwa shuleni. Ila upendo ni kanuni si hisia zinazokuja na kutoka. Angalia jinsi ya kufanya mahusiano yawe mazuri. Mshauri kwa mambo, inategemea na shida yenyewe. Siku za mbeleni tabia zingine huondoka. Uwe na uvumilivu wanapokua, utashumshukuru Mungu kwa uvumilivu huo

***82. Tuna mtoto wa miaka 2 ana dada wa miaka 4, 6 na 8 anawapiga na kuwafanyia fujo mpaka wanalia tufanyeje?***

Mwambie vizuri na aelewe kwa vile mtoto wa miaka anajua vyema maumivu na kupigwa waambie dada zake kwamba akiwapiga nao wampige miguuni au mapaja. Hii inaitwa nidhamu ya upendo (loving discpline)

***83 Ni matatizo gani yanatokea wazazi wanapoachana na watoto wao waliokuwa watu wazima?***

Watu wengi walifikiri ni matatizo ya wakwe! Kumbe siyo, ni matatizo ya mahusiano na wazazi! Hata wengine wanafikiri kwamba wanaishi na wakwe vizuri kuzidi wazazi wao. Tatizo ambalo limechukua karibu nusu ya zote ni wazazi kutopenda watoto waende "mama hakupenda niwe huru, hakugundua kwamba sikumhitaji kwa namna ile tena. Alitaka niwe chini yake na anitawale kwenye maisha yangu". Wengine wamesema wazazi wanawaona kama watoto na wanataka yale waliyokuwa wanawafanyia wakiwa wadogo waendelee, hawafurahi tukisaidia wengine au kufanya vitu vya jumuiya. Mwingine alisema nina miaka 54 na bado nikimtembelea mama yangu haniruhusu nimenye viazi au kupika, anasema sifanyi vitu anavyotaka. Kila mara ananikosoa kosoa tu hata akija kunitembelea kwangu. Kila saa anataka kunishushua, hata kwa vitu vidogo vidogo. Mwingine alisema "nilikuwa kitinda mimba wa watoto 5 na msichana peke yangu, na nikirudi kutembelea wazazi mama anasema ingekuwa heri ningekuza watoto wa kiume 4 kuliko binti mmoja, na naomba Mungu anisaidie na kunipa nguvu za kumsamehe mdogo wake ni

malumbano kila saa, "hata najiwazia kuna haja ya kumtembelea kweli? Yaonekana haridhiki na kila kitu japo amebarikiwa sana ni mtu wa kunikosoa kosoa tu. Nampenda na kumheshimu ila nataka aache sumu zake". Mwingine alisema mama yangu ana wivu na kujilinganisha nami kila mara kwa nguo , kwa uzuri wa uso "nywele zako siyo kama zangu, nashangaa mzazi kujilinganisha vile kama mke mwenza, hivi kwani tuna mashindano gani!?".

**84 Mtoto mtu mzima au mzazi akiwa na maneno ya kashifa, malumbano, kukosoa na ya kuumiza ufanyeje? (toxic people)au watu wenye sumu wanaitwa kwa kingereza**

hili ni jambo la kutia huzuni, ila kuna watu wa namna hii hawana furaha na wanapenda kutia wengine huzuni. Wengi wanapenda kucontrol watu na wanataka vitu viende watakavyo, yote ni kuhusu wao (it is about them). Nafikiri umekutana nao wengi au wewe ni mmoja wao! Nilihudhuria mkutano wa "women of faith" na kuna washauri wanaoependa Mungu wengi (counselors) wao walitoa ushauri wakiwa kwenye panel (jopo) ambalo Sandi Pati alikuwa mwenyekiti. Mmoja alisema wakimbie watu kama hao! Ila utawakimbiaje wakija kukutembelea nyumbani pako, kukupigia simu na kukuandikia barua mara kwa mara? Watu wenye sumu "toxic people" wamo duniani hata nyumba za ibada tunapata mioshi yao. Jaribu kufanya wema na kuwasamehe, maana usipowasamehe ni wewe ndiye unapata shida, wao wenyewe mara nyingi hawajijui, ni hodari, wana nguvu, hawana kazi ya kufanya (idle) na wengine wana maradhi ya hisia. Kuwafikiria mno ni kama kunywa sumu, ukitegemea wao ndiyo watakufa. Yabidi uwasamehe, kisha usonge mbele. Nabii mwenye hekima Ibrahim alikuwa na hii shida na mpwa wake aliyeishi naye kama mtoto wake baada ya kaka yake kufa. Kulikuwepo magomvi na malumbano 'basi usiwepo ugomvi nakusihi kati ya mimi na wewe, wala kati ya wachungaji wangu na wachungaji wako maana sisi tu ndugu.. Je nchi hii yote haiko mbele yako? Basi ujitenge nami, nakusihi ukienda upande wa kushoto, nitakwenda upande wa kuume, ukienda upande wa kuume nitakwenda upande wa kushoto". Mwanzo 18 yaelezea Ibrahim alijua kutawala watoto wake vyema.

Tujitahidi tuwe wapatanishi, kwa watu wanaopiga simu kugombana au kuandika mabarua ya sumu ni rahisi usijibu! Nilijifunza hili baada ya miaka mingi, kwa vishawishi vya kujibu nyaraka za watu kama hawa, haikusaidia!. Hautawaridhisha na majibu yako bali utaongeza mafuta kwenye moto. Pengine uwashauri waandike kitabu kusitransfer hizi nguvu zao kwenye jambo la manufaa! Wanaweza kuandika mpaka peni au computer ikatoa moshi!. Ila kwa yule anayekuja kwenye nyumba mwambie vizuri tu kama Ibrahim. Hakuna atakayemwona Mungu Anayependa kulumbana lumbana, ni tabia ya mwovu si ya Mungu. Akiendelea kukufuata fuata

niandikie!. kwa wanawake angalia kwenye computer huduma za mama Beth Moore usikie mashauri, na washauri wengine kama vile au Reviveourhearts Internet radio au blog ya one without words.

Dr Dobson anazungumzkia Tough love principles (kanuni za upendo mgumu?) zisome. Phyllis and David York, wanasema wazazi kuna wakati wa kumwonyesha mtoto awe mahali pake. Mama mmoja alipigwa kisu na mtoto wake na bado anatolea udhuru kwamba "hakudhamiria kufanya vile" na bado wanaendelea kuishi nyumba moja na mtoto wa miaka 19. Jaribu kuondoka na mahusiano ya ya sumu (toxic). Kumsamhe, mwelewe, ila anapovuka mipaka mwambie mfano, hutatumia hii simu, hauruhusiwi kutumia baiskeli yangu. Wazazi hawa wa tough love wana chama chao cha kusaidiana mawazo. Yaweza mbinu zisifanye kazi mara zote ila zitafanya mara nyingi. Yawezekana wewe mzazi ndiyo sumu kwa watoto! Kama ni vile, omba Mungu akusaidie uache jazba hiyo yenye sumu.

**85 Namwonea wivu jirani yangu ana mtoto anayetii, anashika sheria na kufanya anayoambiwa**

Ni kweli mara nyingi sote tunapenda tuwe na mtoto kama huyu (compliant child). Ila mara zingine watoto kama hawa wanategemea wazazi mno kiasi kwamba hawafikiri kwa mawazo yao (long dependence relationship). Mtoto akipevuka yatakiwa awe huru na kufikiria na kujitegemea. Watoto wale wanaopenda na nia yao ni ngumu kubadili (strong willed) wanakuwa tayari wakati wowote kuondoka na kuwa huru.

Mtoto wa kupendeza wakati wote, mara nyingi hawezi kueleza hasira yake na anakuwa na hasira ya ndani ambayo anaitoa kwa njia nyingine yenye madhara zaidi. Mara nyingi inakuwa kazi kushirikiana na ndugu zake na kuwa na chuki, hadithi ya mwana mpotevu yatufundisha zaidi kwamba yule aliyebaki na kufuata sheria alikuwa ndani ya moyo wake amechukia. Yawezekana si mara zote ila ni mfano kwamba anayeshika sheria anaona wengine wanaachiwa tu hata wakifanya mabaya au ndiyo wanaishi (mfano wa kaini na Abel). Mtoto wa namna hivi akiwa mkubwa aweza kuugua vidonda vya tumbo, vichwa au shinikizo la damu. Watoto wa namna hii wanahitaji tuwajali na kuwauliza maswali wazungumze ya moyoni, na kuwafanyia haki ukilinganisha na wengine. Wape uamuzi wa kuchagua nguo au shule n.k washikilie ila waache pia waende wasikutegemee sana. Hakuna kitu kama mtoto rahisi, kulea kila sample ya tabia ina shida yake. Maana akiwa rahisi kupendeza marafiki wabaya aweza kuigiza vile Ambavyo ni vibovu kirahisi ili atunze amani nao. Kwa kifupi, hata akiwa ni rahisi kulea, awe na uti wa mgongo (back bone) na mabadiliko ya moyo na si matendo tu.

***86 Je, mtoto kurudia darasa ni kitu kizuri?.***

*Mara zingine mtoto ni vizuri arudie darasa si kwaajili ya taaluma tu bali kupevuka kiakili na kijamii. Mtoto akiwa mgonjwa kwa muda mrefu ni vizuri arudie, ila mtoto ambaye anakuwa mzito sana kujifunza haitasaidia sana. Wazazi wengine wanaona kwamba wakati wa likizo mtoto afanye tuition imsaidie ili aweze kuwa na wengine na hii pengine ikawa msaada au isiwe. Mtoto atafaidika zaidi kama nyumbani atasaidiwa hasa kwa vile unamsaidia mmoja kwa wakati mmoja. Ni vizuri mtoto afundishwe kujua kusoma akiwa nyumbani, maana shuleni kuna watoto wengi ili awafikie wenzake. Wazazi fanyeni kazi na watoto wenu*

***87 Je! watoto ambao wamezaliwa na uzito wa kujifunza wana mahitaji kama wengine****?*

*Ndiyo! wote wanahitaji kupendwa na kuthaminiwa. Mara nyingi kuwatenganisha madarasa na kuwaitia majina imeleta huzuni na makovu mengi. Mwalimu aangalie atawezaje kuwa wa upendo na msaada kwa watoto hawa. Ila mzazi ajibidishe naye kuendeleza kazi ya mwalimu nyumbani, apate maarifa kwa wataalamu na hata kwenye tovuti siku hizi kuna mengi ya watoto wenye mahitaji maalumu (special needs children). Watoto wengi wamemaliza sekondari na kwenda hata vyuoni, ambao wengi walifikiri hawataenda kokote. Si wanaoenda kwa kazi tu wanaowezea maisha bali hata wale waendao pole pole, wamekuwa mbaraka kwa wengi, angalia mengine kwenye tovuti na kwa watalaamu kuhusu watoto wenye mahitaji maalumu na jinsi ya kushugulikia hilo.*

***88 Nina mtoto anayetaka kuonyesha mamlaka yake na kukataa kila anachomwambia afanye. Ana miaka 7***

*Shida hii ipo kwa binadamu wote, toka mtoto anazaliwa anataka awe anatawala (manipulate). Watu wazima wameandika vitabu vingi kuhusu hii tabia mfano emotional tafsiri"blackmail, do what I want, shut up and do what I tell you, do what I want and I will be nice to your sweet mother, don't upset me, can't you see I am sick?, do what I want or I wont pay the bills".*

*Have a new Kid by Friday na Dr Lehman, ni kitabu kizuri cha kuonyesha kwamba mtoto ajue kwamba kuna matokeo ya tabia mbovu au kuwa mtawala. Mfano akija nyumbani na kusema "mama mbona saa saba na chakula sijala". Mama aseme "ni kweli ila nilipokwambia ufagie ulisema kwamba hutaki, hata mama hajisikii kupika leo"*

*Mtoto mdogo wa mwaka anaanza kukataa kulala akiwekwa kitandani, anakataa chakula anachopewa anataka kingine, hataki nguo aliyonunuliwa, hataki kuosha*

vyombo au shuguli za nyumbani, hata kukaa kwenye gari kila mtu anagombania dirisha n.k

tabia hizi zakutaka utawala zanaendelea ukubwani na kufanya mtu asijitawale nafsi. Mtoto akiwa mdogo anakuwa chini ya mamlaka ila anapokuwa mkubwa akiwa na tabia ya kutojitawala nafsi ataingia pabaya sana mfano: Sulemani kama mfalme alishindwa kuwa na uzio, akaoa anavyotaka, kula anavyotaka na kwenda anakotaka. Hitler na Stalin walikuwa na mamlaka haya na kutumia vibaya. Mfano Stalin alisemekana aliua 25 milioni. Siku moja alisema polisi waende kwa walimu wake waliomfundisha msingi na sekondari kuwaua

Je mtoto aweza kufanya anavyotaka? Je ni nani mwenye mamlaka katika nyumba? mzazi akiondolewa mamlaka ya kuadhibu mtoto mara zingine madhara mengi zaidi yanafanyika kwa mtoto. Mzazi asikubali mtoto amwite majina yoyote ya kashfa hata akiwa mdogo ni njia ya mtoto kukalia kiti cha mamlaka. Akisema kitu cha kukasirisha, ukakarisirika ameshinda mchezo wa kuwa mtawala

Mamlaka na kusifiwa mno, yamefanya wengi wajenge kiburi na kuwa watu ambao wana udikteta. Na hata si madikteta wa uongozi wa chi tu, ila hata madaktari ,wanamuziki, wachungaji, mashehe, marabi, wanasheria, wanajeshi waliopata kuonyesha utawala au kusifiwa wamekuwa watu wasiojikana nafsi na kujifikiria wao kuliko wengine. Ni kweli mtu hujaribiwa na sifa zake. Ila anapoanguka akajinyenyekeza huweza kufanya huduma nzuri kwa watu. "Ambaye ni mdogo kwenu ndiye mkuu katika ufalme wa Mungu". Chuck Colson aliyekuwa kwenye wizara ya ulinzi wa marekani wakati wa kashifa ya Watergate na kwenda jela. Alipenda mamlaka na kuyatumia vibaya. Ila alipofika jela ilimfanya aweze kuishi maisha ya huduma na kusaidia watu waliokuwa jela. Mtoto akipata mamlaka mapema ana risk ya uasi, kutoheshimu mamlaka (mzazi, mwalimu, polisi na hata Mungu). Mzazi asimpe mamlaka mtoto akiwa mdogo ayatoe pole pole mtoto akiwa anakua na kumwacha awe huru akienda kujitegemea

***89 Tufanye nini kama wazazi kwa kweli tumechoka na hii kazi ya kulea?***

kuna kitabu kilichaondikwa na Dr Joseph Procaccini "parent burnout".Wazazi wanaochoka sana ni wale wanaojali watoto wao na kujitahidi kutafuta kila njia ya kuwasaidia maana hakuna kuungua kama hakuna moto. Wanakuwa kafara kwa watoto, wanaacha mambo mengine yote kama marafiki na muda wao kama mke na mume wa kuongea na kufurahiana. Kila "mwali" wa jua unaenda kwa watoto. Hawawezi kupeleka hata watoto kwa mtu awangalilie watoto hata kama ni mother Teresa!. Kila mara wanakuwa na watoto. Hawaamini hata wazazi wao kwamba japo wana uzoefu zaidi ya wao, na wanaweza kuwasadia wakati mwingine. Wanajiweka katika hali ya upweke.

pengine bibi na babu waishi mbali au hawajali kusaidia wajukuu zao ila wamejiingiza kwenye kazi nyingi, kufanya mazoezi, kutalii na rika zao, nk. Ni kweli mabibi mababu wengi si msaada siku hizi. mke pia aweza kuchukulia kulea watoto ni muhimu hata kumsahau mume wake. Mume naye akachukia watoto kwamba yeye hajaliwi. Hatukatai usiwe mzazi bora (superparenting). Ila usiwe mtu ambaye unashugulikia watoto mno na kujisahau au akafikiri ni wewe tu waweza uzazi mzuri kiasi cha kuchoka na kuungua.

Nguvu za mwanadamu ni muhimu na zina kipimo zinafikia, na mtu huanza kuchoka. Wazazi wanaotaka kuwasaidia watoto waangalie nguvu zao zisiende kwa yasiyo muhimu. Hata Yesu alichukua muda na kwenda mbali kupumzika na kuomba. Angalia mwili wako utunze vizuri. Najua makanisa, mashule, marafiki, ukoo, misikiti, na jumuiya pia zataka tufanye vitu Fulani na tunachoka kabisa maana tuna shuguli zetu pia. Watoto wanapata shida tukiwa tumechoka hivi. Maana kuchoka baadaye kunajileta kwa magonjwa mwilini, kama vile shingo, presha au sonona n.k

Mara zingine wazazi walifikiri wakizaa itasaidia mahitaji yao ya upendo ila kuchoka, hasira na kuchukia kumeibuka. Wazazi watambue hii shida. Mzazi aweza kujitoa kwenye jukumu la kulea kihisia au kusema "nimechoka na hawa watoto siwezi kulea sasa hivi, ni kama waniondokee usoni mwangu. " I just can't deal with the kids right now". Mzazi na hasa mama wa namna hii anaweza kujisikia vibaya ila hajui jinsi ya kupata msaada. Mara nyingi anakuwa mpweke na hana wa kumshauri. Anafikiria ila anachanganyikiwa, na mahusiano yake ya ndoa yanaharibika. Baadaye watoto wanaharibikiwa.

Si wengi wanafikia hatua hizi Ila wapo na anza kuangalia dalili hizi

Ufanyeje ili maisha yako ya kulea yawe mazuri bila kufoka foka, kugomba gomba, kutishia , kukosoa kosoa, kuchoka. Lazima kuna njia nzuri. Usipende kufanya vitu vingi kwa wakati mmoja. Kusoma. Kuolewa, kupata mtoto, kufanya kibarua, kujenga nyumba nk. Mara nyingi hata ni vyema mngoje angalau miaka 2 baada ya ndoa ndiyo mpate watoto. Kuna mengi ya kuadjust kwanza. Mwili wa binadamu hauhitaji presha nyingi hivi. Mwili ukichoka na hisia pia zinafyatuka. Mwili, akili na roho zafanya kazi pamoja. Utajiletea huzuni kama si wazimu. Lazima uwe na balansi ya hizi ili usibomoke! Tumia mwili wako vizuri kama kukimbia marathon, usimalize nguvu zote mara moja kama mkimbiaji wa mbio fupi na ukifika wakati watoto wanaanza kupevuka nguvu inapungua kumaliza mbio. Uzazi ni mbio za marathon kimbia pole pole ni miaka mingi pengine 20 hata 30, ndiyo siri ya ushindi. Ishi maisha yenye balance na kumlilia Mungu ni wa rehema maana binadamu hatujiwezi

**90. Wazazi wengi wanashitakiwa na dhamira zao kwaajili ya matunzo ya watoto, tufanyeje?**

Ni kweli kila mzazi anadhamiri inamshitaki kwaajili ya malezi, hata mtoto akiwa mdogo, mfano "unasikitika kwamba tunamwachia yaya badala ya kushugulikia watoto wetu". Dhamira kutushitaki ni kufikiri kwamba kuna kitu tunakifanya kibaya. Kama ni kitu cha kuomba msamaha tuombe msamaha na kuamini tumesamehewa. Ila kama kiko nje ya uwezo wetu hakuna haja ya kujichapa viboko. Ila ni vizuri kuzijua hisia hizi, usizifungie kwenye chupa mwishowe zilipuke kama bomu. Angalia pale pa kusahihisha. Usifanye dhamira kukushitaki na kukuharibia malezi. Wazazi wengi wamedeka watoto kwa dhamira kuwashitaki kwamba wanaenda vibaruani au mtoto anaumwa naye yupo kazini. Wengine watoa mazawadi kwa watoto kupita mpaka, wanafanya kazi zote nyumbani na kuacha watoto wawe huru, hawakemei tabia Fulani, au wampa mtoto chochote atakacho,kwa vile wanaona kwamba hawako na watoto wakati wote, au wanataka watoto wampende yeye kuliko mwenzi wake.

Toa dhamira kukushitaki na jaribu kuishi kwa furaha na maisha ya imani na matumaini. Huwezi kuwa mkamilifu na tambua hivyo. Angalia kama kuna njia zingine za kufanya mambo kuwa mazuri, omba msamaha pale wa panapotakiwa na songa mbele.

***91 Nina watoto wakambo nifanyeje?.***

Kulea watoto wakambo ina changamoto zake nyingi hasa wakiwa wakubwa. Ulipomwoa au olewa na huyu mtu ulijua hali hii na ulikubali kwamba utaishi na watoto wake kwa upendo. Watoto wengi wana ndoto kwamba wazazi wao watarudiana na mtu anapooa, yafanya wale watoto wamchukie yule mke au mume mgeni.. ni vyema kabla ya ndoa, kuweka wazi na kuzungumza na watoto pia mategemeo yao ni yapi. Wazazi solemba wanakuwa karibu na watoto wao hata pengine kulala chumba kimoja, zungumza na mtoto kile ambacho kitaenda kutokea. Mfano " tumekuwa karibu nawe ila sasa naenda kuolewa. Kama ndoa yangu itakuwa kama Mungu anavyotaka, napaswa kuwa kitu kimoja na mume wangu. nampenda mume wangu ila upendo wangu kwako hautabadilika.

'Mara zingine utafikiri kwamba "uko nje"nikiwa nimeolewa, sipendi udhanie hivi kwani nakupenda na unahitajika katika maisha yangu. Endapo mawazo haya yatakuja "hawanihitaji nami siwahitaji" naomba uniambie ili tuzungumze. Watoto wengi hufikiri hivi na si jambo linalosaidia familia kuwa na upendo na furaha. Lazima uniambie ukiwa na lolote moyoni tuzungumze pale kwenye maumivu na kujaribu kutatua'.

Mara zingine watoto hawapendi kushirikiana vyumba au vifaa na watoto wa yule mume/mke. Ni vizuri mzungumze na kuafikiana mambo Fulani, ili msilete vurugu na ugomvi. Jaribu kuwa mwema na mwenye upendo pande zote. Jaribu kuwa wa haki

pande zote, hata upande wa mtoto wako usipende kuwafurahisha sana wale wa mume wako waliokuja ili kununua upendo wao na kumtelekeza wako nayo pia ni shida yabidi kubalance. Watoto wengi husema "usiniambie kufanya lolote wewe si mzazi wangu". Yabidi mzungumze na mzazi wake ili muafikiane kwenye mambo ya nidhamu na kazi za nyumbani mtafanyeje. Muwe timu moja. Mara zingine watoto wakubwa wa jinsia tofauti wana hofu kuishi karibu au kutumia vyoo pamoja. Pengine ni vizuri milango ifungwe na angalia hali kwamba ni watoto wa namna gani, waweza kuingia katika shida katika nyanja hii. Watoto wengine dhamira zao zinawashitaki wakipenda mama wakambo au baba wakambo wanafikiri wamewatelekeza wazazi wao.  Na wazazi wengine ambao wako nje waleta ugomvi kule waliko kuharibu ndoa hii mpya.

Watoto wengine wanalinganisha wazazi wao na wale wakambo mbele yako "mama yangu ana mapishi mazuri si kama yako" " baba yangu ana kazi nzuri siyo kubeba magunia kama wewe" n.k. Jaribu usirudishe maneno ya kulipizia. Watoto wana hasira kwamba nafasi ya mzazi wao imechukuliwa, zungumza nao na kuwaambia kwamba "najua kwamba ni vigumu kuwa na mzazi mwingine, na mngependa muwe na baba au mama yenu mzazi na si mgeni kama mimi ila najitahidi tuishi kwa furaha na kuwa timu moja ya kupata ushindi".  kisha waambie " hata mimi moyoni mwangu naumizwa na kupata huzuni mkinipakazia vitu, nami nataka tuishi kwa urafiki na kusaidiana pamoja". Ukiona kwamba magomvi yanakuwa makubwa zaidi ni vyema ujitoe na kwenda mahali kimya si wakati wa kufokeana na kupaza sauti,na kusoma zaburi 37.

Japo uzazi wa kambo si rahisi waweza kufanikiwa kwa kuzungumza nao na kuwa na mikutano ya familia ya kutatua matatizo. Je mnataka mwendelee kuishi pamoja na kusaidiana maishani kama kusoma na mengineyo au kuna njia zingine pengine za kuishi kumudu ili tatizo. Endapo kila mmoja ataka kutuma mikuki kwa mwingine hamtafika mbali. Niliona familia moja mama mmoja alipenda kurusha mikuki , hata yule mtoto akisema yametosha tuache na kwenda chumbani mwake, yule mama alimfuata yule mtoto na kufungua mlango na kuendelea. Endapo mmeamua kuishi pamoja kama mke na mume muwe timu moja ya upendo kwenu na watoto. Muwe tayari kupenda watoto wote na kuwahudumia bila ubaguzi.

Mara zingine watoto, au jamaa  au wageni wenu wanaweza kuwa na wivu na kutaka mwachane mwahitaji kuzungumza nao na kuelewa nia zao na kuja na suluhu ili uhusiano wenu uendelee. Je ni kwenda shule ya bweni? Je ni kutafuta wakae na mama yao au jamaa mwingine wa karibu na kuwasaidia huko. Kumbuka kwamba hata mkiachana na kuoa/olewa mwingine haya yatalipuka tena. Watoto wanakaa muda mfupi na mzazi,  ila mtu na mke wanakaa mpaka kifo kiwatenganishe

Ingawa shida za watoto wakambo ni nyingi nimekutana na wengi walioshukuru kwa kulelewana na mama au baba wakambo vyema na wana urafiki na wanathamini mzazi huyo. Hata mama mmoja wa mombasa aliniambia "mama yangu mzazi alikuwa mbaya kwangu kuliko mama wakambo alikimbia kwenda kwa wanaume mbali mbali mara nyingi! Hata hakutujali". Mungu bado ana watu wake japo wakambo wazuri sana kwa watoto. Najua mara nyigi kuwa mama wa kambo ni ngumu zaidi kuliko baba wakambo. Pengine ni kwasababu mama ndiye anayekaa na watoto, anawapa Chakula na mahitaji mengine. Kama una changamoto hii mwambie Mungu akupe msaada wa siku kwa siku

***92 watoto wengi wakizungumzia ndugu zao wanasema maneno ya kufurahisha marafiki mfano "nina dada mkoloni sana na kaka yangu kila mara vitu vyake akiviweka nataka nivipige teke" je hii ni hali ya kawaida?***

Inaonekana kitu cha kawaida kwa watoto wengi wa umri wa teenage 12+ kuwasema ndugu zao hivi ili wapate kuwa timu moja na marafiki au rika zao, ni msukumo Fulani wa rika. Pengine ni kutaka kuiga wenzao au ni wivu kwa ndugu zao. Nafikiri tabia hii si nzuri maana kila mtu ni "mlinzi wa ndugu yake". Waeleze watoto wako kwamba mko timu moja na msifikiri watu wa nje watawapenda sana kwa kuonekana hamko timu moja. Jenga tabia ya kutozungumza mambo mabaya kwa wenzako shuleni, nyumba ya ibada au katika jumuiya. Ukimshika mtoto akizungumza mabaya kuhusu Fulani mwambie akwambie mawili mazuri ya mtu huyo. Usizungumze mume, mke au watoto wako vibaya kwa watu wengine. Jaribuni kufanya vitu vyenu pamoja. Fundisha watoto kumshukuru mwenzao au kumpongeza akifanya jema. Mtu akifanya kosa angalia jinsi ya kumsaidia kama ndugu na si kumlaumu laumu. Kuwa mwanatimu wa familia inasaidia kuwa mwanatimu kwenye familia ya Mungu pia katika jumuiya. Wote tunajisikia na nguvu tukiwa na timu inatusapoti na kuwa na mategemeo mazuri nasi.

Nasi wazazi tujaze vikombe vya upendo vya watoto wetu, chukua muda kuwasikiliza na kujenga timu bora. Wapende bila kamba yoyote au vizuizi (unconditionally). Itawasaidia kuwa wanajumuiya bora.

**93 Nawezaje kusaidia watoto watii mamlaka**

'na sasa Bwana Mungu wako anataka nini kwako? Ila umche BwanaMungu wako na kewnda katika njia zake zote na kumpenda na kumtumikia Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kuzishika amri za Bwana na sheria zake ninazokuamuru''

wazazi wana jukumu la kuwafundisha watoto wao wampende Mungu na mamlaka yake. Kujifunza kumpenda Mungu mzazi wetu mkuu na mamlaka ya juu ni muhimu

na hii mtoto atajifunza toka kwako. Mtoto aweza kuogopa mamlaka au kupenda na kuheshimu. Mamlaka ya dunia kama polisi, jaji, mwalimu. Wafundishe watoto wako kukuheshimu na kukupenda. Mwambie mtoto kwamba usingependa kuishi pale pasipo na mfumo au mamlaka "je ingekuwaje kama tusingekuwa na polisi au jeshi?". Mwulize mtoto. Waeleze watoto mamlaka ya dunia kwa kawaida yamewekwa kututumikia sisi , au kwa faida yetu.

Usipokuwa mwangalifu utafundisha watoto wako kuogopa mamlaka ya dunia au kukuogopa na kumtumikia Mungu kwa woga wa adhabu au kuasi wazi wazi na kutelekeza karama ya Mungu ya wokovu.

Usipende kutumia nguvu au udikteta "sijali unafikiri nini fanya hili nalokwambia" watoto wakiwa wanapigwa, fokewa, laumiwa, kosolewa kila mara na kunyimwa uchaguzi au uhuru kabisa wanajenga hari mbaya na mamlaka. Wazazi wengine wanaweka sheria nyingi ambazo wenyewe hawazifuati mfano " usiangalie runinga zaidi ya saa moja". Ikija soka wanaangalia kwa saa tatu.

mzazi awe na mamlaka ya serikali ya nyumbani ila atumie demokrasia hii itafanya watoto wafuate ambazo wanajua sababu au wamesaidia kutunga. Mfano hakuna kuvuka barabara –waulize sababu kisha watoe na uandike wajue sababu. Kwa mtoto mdogo waweza kuweka sheria bila kueleza vitu vingi. Ila mzazi jifunze kufurahi na watoto wako hata kucheza nao siyo kila saa unatafuta mbinu za kuwakimbia na kufanya vitu vyako. Waongoze watoto kutii mamlaka yako. Mara zinginei onyesha rehema, si kila kosa lahitaji adhabu kali, mara zingine watoto hufanya kitu kwa bahati mbaya. Mfano kumwaga maji, siyo kila kitu unatoa adhabu. Utafanya watoto wasikwambie ukweli wote na kuwa waongo , dhamira kuwashitaki na kutaka usikae karibu nao

***94 Nilikwenda kutembea kwa rafiki na watoto wangu. wakaanza kufuatisha watoto wa ile nyumba kupiga makelele na kuzomea nifanyeje na mama yao hawagombezi wale watoto.***

Napotembelea familia nyngine najaribu kuangalia watoto wangu wasikose adabu "usiguse hiki au kile, angalia miguu yako usikanyage hiki au kile" ila mara zingine yule mzazi wa ile nyumba anasema "ni sawa tu wacha waguse au wakanyage!". Nafikiri ingekuwa rahisi mwenyeji kuweka viwango "tukiwa tunatembelea hapa hii itafanya nisiwe na tashishwi wakati nafanya ugeni hapa". Nikiwaambia watoto wangu sheria au watoto wa mwenyeji yaonekana mimi ndiyo "mzazi mbaya" . napenda watoto wangu wajue yule mwenyeji wetu hapendi hizi ghasia pia ila anataka asitukoseshe raha. Wazazi wengi hawapendi watoto wao kuambiwa wakiwa wanakosa, wanaona ni kama wamekosolewa mbinu zao za kulea.

Endapo kwenye jumuiya tungekuwa tunasapoti mzazi mwingine akiwa anatusaidia na watoto wetu tungepiga hatua kubwa kwa malezi ya watoto. Wazazi wajifunze kuona kwamba wazazi wengi tu wana nia njema kwa tabia ya watoto wao. Mtu anayependa watoto akiwaambia watoto wetu, wanaweza kujifunza toka kwake vizuri tu, na tukawa timu moja na mzazi huyo. Mfano mzazi aweza kusema "tawi la mti huu laonekana dogo ni hatari kwenu wote kupanda huu mti, labda mmoja mmoja". Badala ya kusema "shukeni haraka kwenye mti wangu mtajutia mkipanda". Mtoto anajifunza kumpenda na kumheshimu mlezi mwingine ambaye si mzazi kutokana na upendo wake. Mtoto anajua si mzee mbaya tu ila ni mtu anayejali mema yao. Mfano ukimwona mtoto anapiga kelele kanisani badala ya kumngoja mzazi wake baada ya ibada umwambie, mwambie mtoto ukitabasamu " sisikii mahubiri mkizungumza kwa sauti kubwa" au ukisikia mtoto mmoja anamzungumzia mwenzake vibaya "maneno hayo yatamhuzunisha mwenzako, jambo la upendo ni kumwomba msamaha". Ukiona watoto wangu wanaharibu vifaa, usingoje mpaka vimeharibika uniambie baadaye waambie " hili si jambo jema la kufanya litawaweka kwenye tatizo kubwa". Napenda watoto wangu wampende na kumweshimu Mungu na kupenda watu, na siwezi kuwa kila mahali, au mara zingine waweza kumsikiliza mwingine vyema zaidi, naomba kwa kujali waambie ili uwasaidie. Nami nafanya vile kwa watoto wa wengine

***95 nitamsaidiaje mtoto wangu ajue talanta zake?***

kila mtoto ana talanta spesheli na akizitumia vizuri zinazidi kujengeka kwa kumtumika Mungu na kuhudumia watu. Mwambie mtoto hakupewa talanta ajivune au ajisifu, ila kwa utukufu wa Mungu. msaidie mtoto kujenga talanta kwa kumpa ujasiri, uhuru , kujiamini ili zitokeze. Mungu anatoa talanta na mtoto anakuwa na shauku ya kuitumia. Unamjua mtoto kuliko yoyote, je anapenda nini, ana maumbile gani. Usifanye kosa la kuendeleza talanta yako kwa mtoto kwa vile uliizika (hasa kama mtoto hana hiyo). Mwonyeshe mtoto mambo mbali mbali yatakayofanya talanta yake kutokeza, kama vyombo vya muziki, fasihi, michezo, taaluma. Mfano waweza kununua darubini telescope na kuona kama mtoto apenda kusoma mambo ya fizikia yahusuyo nyota. Vingine hata si ghali mfano filimbi yawesa isifikie dola 10, ila mtoto aweza kujifundisha mwenyewe nyimbo ukashangaa. Ukuze udadisi na shauku ya mtoto katika vile vizuri anavyovipenda. Itamsaidia pia matatizo ya kuingia kwenye ukorofi!. Lazima uwe na magoli na hata watoto waishi kwa magoli. Mambo mengine yaonekana hayawezekani ila kama Mungu ametoa talanta itashamiri tu. Beethoven wa ujerumani alikuwa kiziwi akatunga nyimbo nzuri sana na kucheza piano, ni nani angetegemea hayo? Mungu ametoa vipaji, hataki tuvipoteze au tuwe wavivu. Umashuhuri si lazima kujulikana au kuwa na cheo ila

kutumia talanta Mungu ametupa. Edison alisema kuwa na akili nyingi au intelligence ni "2% ubongo na 98% mitulinga". Kingereza twasema 2% brains na 98% hard work. Kuweka magoli ni muhimu, mwambie mtoto wako aweke magoli na kuanza kuyatekeleza kama kuranda na kutengeneza viti kila siku, kufanyia mazoezi mashine ya kushona au vyombo vya muziki kwa dakika 20 kila siku nk. Msimulie mtoto wako watu mashuhuri waliotumia talanta zao kama vile Mzee Morris na ngoma zake kumi, Kambarage Nyerere, Jomo Kenyata, Patrick Lumumba, Mandela n.k. Mwambie azifikie nyota au vito juu. Fikia nyota moja kwa wakati mmoja, na zile za karibu na endelea kufikia zingine. Mpongeze akifikia nyota, na kuna zingine pengine asifikie ila asikate tamaa na aendelee kufikia zile zinazoweka kushikika. Kuna maswali dodoso (questioneer) zaweza kuwa msaada kudadisi pia, nilituma kwa watoto wangu nikapata mwanga kidogo.

***96 nawezaje kuwapa watoto wangu motisha?.***

Kuwatia watoto moyo ni muhimu sana. Mara zingine tukimwona mtoto anachezea tiara au pia (kite or top) tunamgombeza ila watu wengine kama Benjamin Franklini wamevumbua mambo ya umeme kwenye michezo ya aina hii. Majaribio mengi ya sayansi na ugudunzi yalianza watoto wakiwa wadogo na wazazi wao wakiwatia moyo kufanya majaribio, kukuza talanta au kucheza michezo Fulani. Pengine kwaajili ya umasikini waweza kufoka "usitumie cherehani yangu au msumeno". Hili ni kosa ambalo wengi tunafanya. Mtoto wako anakupima namna gani katika kipimo cha kumtia moyo? Jaribu kumwuliza! Kukosoa, kutaka mtoto awe mkamilifu katika ustadi au kuwa na mawazo chanya kunafanya mtoto akate tamaa na kujifikiria hawezi au ni duni. Ujasiri wako wa kumtia moyo unajenga mtoto kujiamini kwamba anaweza (confidence). Mwahikikishie mtoto wako ana talanta kumi au zaidi! utamweka kwenye mahali pa kufanya mengi ukimwongoza. Kuna mtu anaitwa Barnabas ambaye maana yake ni mwana wa matumaini –encourager. Ni tabia nzuri Ambato wote tumlilie Mungu tuwe nayo. Jifunze tabia hii kwa watoto hata kwa wengine ukiwatia moyo. Kwa wale wenye maofisi au biashara mweke mtoto wako katika shuguli, hata wa miaka 8 utashangaa anavyojifunza na siku hizi mambo ya computa marafiki wameniambia watoto wao baada ya kufundishwa wamewasaidia mengi na kujiamini kufanya mengi ya kusaidia wengine. Akikosea mpe moyo "jaribu tena".. tia moyo, tia moyo tia moyo. Kamwe usiseme "najua ungeshindwa".watoto wana udadisi na kuuliza maswali ya "kwanini". Mahali pa usalama usiogope watoto kuchafuka wakijifunza. Wakitengeneza vitu kwa kuvumbua wanavithamini zaidi ya kununua. waache watoto wagundue, watajifunza zaidi ya kuwaambia. Kuza udadisi wao

***97 Nitawasaidiaje watoto wangu kutofautisha baya au jema?***

*Mtoto akiwa mdogo ni rahisi unamwambia hili baya hapana usifanye na hili zuri. Ila anapokua inakuwa kazi. Yaani nyeusi na nyeupe inakuwa rahisi kutofautisha, ila kijivu ni ngumu kidogo. "inabidi tufundishe watoto wetu toka udogo, wakiamka, wakitembea na kwenda kulala" neno la Mungu.. ila watoto mara nyingi wana nia ya kufanya mema ila wanajikuta wamefanya makosa. Je inakutokea nawe pia? Mtume Paulo kwenye matendo saba alisema anapata shida hii. Ikiwa wameiona, waeleze kuhusu tatizo la dhambi lilivyoingia duniani. Watoto wanajitahidi kuwa wema wakifanya makosa wanaomba msamaha na kusema hawatafanya ikifika usiku wameshafanya na kukata tamaa. Shetani ana nguvu na ujanja, watoto kwa nguvu zao wenyewe hawawezi pambano hili. Ila Mungu ameshatupa ushindi kwa Mwana wake.wafundishe wamwombe Mungu aingie mioyoni mwao na kuwasaidia kushinda hii vita. Tunaokolewa kwa neema na Haki ya Mungu. "ombeni nanyi mtapewa, tafuteni nanyi mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa" wape ahadi hii waidai. Mtoto akiwa mdogo anaona ubaya na wema kwa rangi nyeusi na nyeupe tu ila anapokua anaanza kuona mambo mengine kama nia (will) iko kwenye ubaya uliotokea au kama ni bahati mbaya na si kudhamiria. Watoto hawajajua kanuni na nia (principles na motives) vyema. Waambie kwamba kutii bila kujua sababu unavyozidi kukua haisaidii sana. Mara zingine waweza kufikiri akipewa adhabu sana kwenye jambo Fulani, basi ndiyo kosa kubwa na si kweli. Wazazi wamsaidie mtoto kufikiri baya na zuri anapoendelea kukua, isiwe ni udikteta wa wazazi ila moyo na nia yake isiwe na uasi. Jadiliana nao kuhusu kanuni. Hata wasipoonyesha wanajali maadili yako waweza kushangaa wakiwa na wengine wanasimamia kile ulichowaambia, na Kutoa ushuhuda wa maagizo yako! Hautaki wawe wanafiki au mafarisayo, ila waweke sheria hizi kwenye mioyo yao. Mfano kudansi au kuangalia filamu mbaya kuna ubaya gani? Kwa kifupi haileti mahusiano mazuri na muumba kwani itakuingiza kwenye uharamia au uzinzi n.k waulize je kwenda mbinguni na kuishi milele na Mungu ndiyo safari yao? Basi lazima wapange na kuishi kutokana na mahali wanataka kufika, magoli yao yawe pale.*

**98.Je ni muhimu watoto waende ibada?"**

Daudi katika Zaburi amesema "njooni tuabudu, tusujudu, tupige magoti mbele ya Mungu aliyetuumba. Kwa maana ndiye Mungu wetu, na sisi tu watu wa malisho yake". Kuabudu kunapaswa kuwa kitu cha kuleta furaha. "mtumikieni Mungu kwa furaha , njoni mbele zake kwa kuimba". Ukiwa katika nyumba ya ibada chunguza watoto wako, je wanajifunza kuabudu? Je wanampenda Mungu na kuwa kwenye nyumba yake? Au wanazungumza, kulala ,kusoma na kucheza? Je watu wazima wanatoa mfano mzuri. Je wanakuwa na mawazo gani kuhusu kuabudu? Kuabudu

yapasa kutoke kwenye mioyo yetu na kububujika bila kulazimishwa. Ni kupenda kuwa karibu na Muumba wetu. Kile ambacho watoto wako wanaona watu wengine wakifanya kanisani kisiwe ndiyo viwango watoto wako wanapenda wawe navyo. Jaribuni kufanya kiwe kitu ambacho mtoto wako hapendi kukosa kwa 'kina' ya thamani yake.. Endapo una watoto wadogo na wanashindwa kutia makini waweza kwenda nao nje na kuwasomea kitabu au mambo ya asili yahusianayo na kuabudu. Fanya nyumba ya kuabudu kiwe kitu cha furaha na si mahali pa kufoka na adhabu. Jinsi watoto wanavyokua, washirikishe katika kuchagua nyimbo, mafungu, kuandika. Weka viwango vyako vya kuabudu, la sivyo utaona wanakopi watoto wengine kanisani na kuanza kufanya yasiyo ya kuabudu. Kabla ya kwenda kanisani chukua muda msiende mkiwa na kukosoana, kukasirika na kuharakishana!. Watayarishe watoto kimawazo, fikeni mapema. Hata waweza kutoka mapema na kuchukua muda na kuzungumza hata kula kifungua kinywa kwenye viwanja kabla ya kuja kanisani (picnic). Pengine hata kabla ya mahubiri watoe watoto nje mzungumze na kutembea kidogo ili mawazo yao yawe tulivu. Mkitoka waulize pia kwamba wamejifunza nini?: na wanawezaje kutumia kwa maisha ya kila siku?. Kama ibada haipangwi kwa kujali mahitaji ya watoto waambie viongozi. Programu ziwe na hadithi za watoto, mafungu, ushuhuda, kwaya ya watoto, wakaribishaji watoto, maswali kwa watoto, ibada ya watoto mara moja kwa mwezi, au watoto wawe na huduma yao, au watoto wakubwa kuhubiri mara moja kwa miezi miwili n.k
kuimba nyimbo, kukariri maandiko na, kusali, hata kusoma ni elimu kubwa kupita zote dunani, hivi vyamsaidia mtu kuliko kitu kingine.

### 99 kazi gani nimpe mtoto wangu napata shida kuamaa, ana miaka 6?

kazi ni muhimu kwa tabia ya mtoto sana. Inafanya mzazi atawale nia ya mtoto (willful transgression not to be overlooked)-" kutotii kwa kunuia kusiachwe kiholela " alisema Susan Wesley mama wa watoto 19 kutoka Uingereza. Tumia adhabu kama mtoto analeta uasi wa wazi wazi au anapiga mamlaka ya mzazi. Angalia list kwenye sura ya kazi na website ya "401 ways to get your kids to work at home by Mc cullough". Njia 401 za kufanya watoto wako wafanye kazi za nyumbani. Nimetoa muhtasari wake kidogo. Kando na kumweheshimu Mungu kama Mwenye Enzi, linalofuatia ni kujua na kupenda kazi. Watu husoma ili wapate kazi. Mtoto apasa afundishe ustadi, Nimepata shida kufundisha watoto, ila mara zingine nikiwapeleka kwa mtu mwingine wafanye kazi kwake hufanya. Fanya juu chini, na kuomba hekima, mtoto asiyejua na kuthamini kazi ni mzigo kwake, jumuiya na kwa yule atakayemwoa au atakayeolea naye. Uvivu si tabia ya mbinguni. Biblia inasema

asiyefanya kazi asile! Agizo zito. Je waweza kusema asipokula itakuwaje? Hebu tuangalie chungu chungu na siafu walivyo na bidii!

### *100. kubariki nyumba au mtoto kuna maana gani?*

Watu wengi mtoto akizaliwa wanaita watu wanaompenda Mungu na kumtoa wakfu mtoto ili aweze kumtumikia Mungu na kuhudumia watu. Jambo hili ni la muhimu sana. Na ni vizuri sadaka itolewe. Watu wengi wametumia pesa nyingi kufanya sherehe za siku ya kuzaliwa ila wamesahau kutoa sadaka kwa masikini, wajane au yatima. Ni vizuri kwenye sherehe hii ya kumkakabidhi Mungu mtoto wetu, tupate kufikiria wengine wenye mahitaji. Waumini wengine pia watoe ahadi za kusaidia watoto katika jumuiya hiyo. Inachukua kijiji kulea mtoto awe mwadilifu. Watu wengine pia hutoa nyumba zao wakfu. Mungu ana kusudi maalum kwa kila nyumba. Familia yaweza kufanya vingi vizuri kwa watu na kwa Mungu, na shetani anawasukuma kwenye mengi maovu hivyo ni muhimu kuwa na maombi maalum ya kuweka wafku nyumba ili mfanye kazi pamoja kwa furaha na upendo. Familia moja iliamua kuiweka nyumba yao wakfu kumtumikia Bwana na kuita mchungaji wao na wageni kufanya karamu ndogo. Waliandika kwenye ukuta "Nyumba hii ya Masaka Momadi imewekwa wakfu tarehe 20/11/2001 ili kumtumikia Bwana na kuhudumia watu". Unaonaje leo uanze kupanga karamu hii na kuandika ukutani mwako maneno haya ambayo yatakuwa ushuhuda kwa wageni wako na kwako, na utaposahau magoli yako ya maisha utajikumbusha ukiyaangalia tena na tena na kupata tochi kumulika hata siku ile ya asubuhi njema.

Au waweza kuandika "chagueni leo ni nani mtakayemtumikia, ila mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana"

chukua muda kuwabariki watoto wako kila siku, upatapo nafasi wawekee mikono vichwani na wape baraka.

### *101. nifanyeje mtoto wangu ajue anamhitaji Mungu na inabidi amfahamu*

kujua sheria za mpira haziwezi kumfanya awe mchezaji bora. Ila maarifa anayopata ya sheria ayatumie yeye mwenyewe. Kujua kuhusu Mungu ni muhimu , ila uzoefu wa kuwa na mahusiano naye wahitaji mazoezi. Waambie watoto ushuhuda wako na waulize maswali katika hatua zote za ibada ya familia. Maombi yenu yaandikeni na yaliyojibiwa shukuruni mkiwa wote. Mtoto wako ajue unaomba na kujaribu kuishi maisha ya kumtegemea Mungu. Wape nafasi watoto kwa mzunguko kuongoza ibada. Personal responsibility ni muhimu, kila mtoto hata wa miaka 4 afundishwe kuomba mwenyewe na kujenga imani yake, maana ukiwa haupo nani atamsaidia? Mtoto hatafika mbinguni kwa wewe kumpenda Mungu. Mungu hana wajukuu ni watoto tu. Imani yabidi itoke kwake mwenyewe si mtumba wa imani yako!. Amtegemee,

amwamini na kumtumaini Mungu. Aone uzuri na upendo wa Mungu upitao kina, marefu  na mapana kwake. Kwamba hata wewe au yeye humependi vile kama Mungu wa mbinguni.  Mwambie twamwitaji Mungu ila hatujui mpaka tusipojiweza na njia zote zimefungwa kama Naamani aliyekuwa na ukoma! Mtoto asifikiri kwamba anaweza bila Mungu. Nadharia zingine mtoto hawezi kuelewa ila ya upendo wa Mungu, watoto wengi wanaelewa vyema kuzidi watu wazima na ndiyo maana 75% ya watoto humpokea Mungu mioyoni mwao kabla ya kufika miaka 10. tuonyeshe watoto kwamba Mungu ni halisi katika maisha yetu. Toka mtoto anapozaliwa usikazanie hadithi zisizo halisi kama za superman, zimwi. Mwambie wokovu ni bure ukiupokea, toa mifano mfano chukua hii sh 100 ni zawadi, je yabidi urudishe au ulipie? La. Hitaji kubwa la mtoto ni kuokolewa, na Mungu anasema "Niangalie mimi mkaokolewe,enyi ncha zote za dunia, maana mimi ni Mungu na hapana mwingine". Kila mtoto anazaliwa pagani au kafiri, mpaka afundishwe imani, na kisha aipokee na kuifanya kuwa yake mwenyewe.

**102. tunafundishaje watoto wetu kusali?**

Tunaambiwa kuomba bila kukoma. Mara nyingi watoto wetu wanasali kama desturi bila kufikiri, wakila au wakienda kulala. Walisema maajabu 7 ya wanaompenda Mungu ni kama "kuombea chakula kupita maisha yao, kuangalia TV kwa muda mkubwa kuliko kusoma Neno la Mungu nk). Sidhani kama tungekuwa na marafiki kama tungezungumza nao wakati mambo yameenda vibaya tu. Ili kujenga mahusiano yapasa tujadili, tuambiane habari, kuhusu yanayotokea katika maisha yetu ya kila siku. Mfundishe mtoto wako azungumze na Mungu kama rafiki, amweleze yale ambayo yanaendelea maishani mwake " leo asubuhi nilicheza mdako au , mama alinipiga viboko bila haki nami nilishangaa je Baba wa mbinguni nawe ulionaje pale ? nafikiri rafiki yangu alifunga goli zuri leo' . Wafundishe watoto wako kuwaombea wengine pia, wakiona matokeo mazuri imani yao itajengekea na kupenda kuomba zaidi.  kusali ni kuzungumza na Mungu kama rafiki, kunaleta faraja na matokeo ambayo yanatufanya tukaribie na Mungu na kuwa na furaha. Kama mzazi nimejikuta napenda kuongea mno, na marafiki na watoto n.k. Bali sina muda wa kuomba, na wakati kuomba ni kuongea na Mungu. Nimejiuliza inakuwaje nina maneno mengi ya kuongea, blah blah ila ikija kuomba au kuongea na Muumba wangu, maneno yanakauka?!! Je hili limekutokea wewe pia? Tuombe Mungu atuhurumie kwani mambo yote ya kimbingu ni mpando, lazima tukiamka twende magotini, asubuhi mchana na usiku, na zaidi ya hapo. Tujifunze 'kupiga porojo na Mungu'' kama vile marafiki zetu.

### 102. Twawezaje kuwamotisha watoto wetu kuona kwamba mbinguni ni mahali ambapo ni muhimu kuliko kote kufika?

maandiko matakatifu yanaonyesha mbingu, ahera au paradiso ni mahali pazuri sana. Uzuri wake wameshindwa kusimulia binadamu "macho hayajaona, wala masikio hayajasikia, wala hayajaingia katika masikio ya binadamu mambo ambayo Mungu ametayarishia watu wake". Baadhi ya mambo yaliyosemwa ni hakuna maumivu, vilio wala kifo. Majengo ya vito, barabara za dhahabu, vyakula vya kupendeza macho na ladha vya pekee. Mito ya kupendeza, moyo kupata raha na kuridhika , urafiki, kucheza na wanyama kama simba na amani ipitayo akili yote. Ni sehemu ya lazima kufika! Mahali pa ajabu. Mbinguni ni mahali, si hali, mahali panapofurahisha watoto. kutakuwa na michezo na mengine mengi. Usimfanye mtoto afikiri mbinguni ni kuishi kwenye majumba makubwa bila anaowapenda au kiupweke, au mbinguni kutakuwa na watu tu na si wanyama au utakuwa unaelea mawinguni ukipiga vinanda masaa 24! Ila jipe moyo katika ulezi, usihofu wala usiogope kwani pambano ni la Bwana.

Mbinguni ni mahali kila mtoto au mtu ataridhika kwani kila mmoja atakuwa na uhuru anaoupenda usiokuwa na dhambi.
Endelea kuzungumza na watoto wako kuhusu mbingu, ni tumaini la baraka hautajuta kuwa kule na kila mtu atapata vitu vya kufanya na kufurahia au kufurahiana na wengine! Onyesha mbingu kuwa nzuuri sana kulinganisha na dunia yetu ambayo imekuwa kama tambara bovu lililochoka. Wewe na watoto wako njozi zenu mziweke kule, na mnuie na kufanya matayarisho kwamba siku moja mtakutana kule kwenye kiti cha enzi cha Mungu! Jambo la kufurahia kukutana kwenye mto wa uzima au mti wa uzima. Tukilenga mbingu tutapata mbingu, ila tukilenga sifuri tutapata sifuri. Hivi kuna cha kulinganisha hapa duniani kweli. Basi utii wetu na watoto wetu unaanza hapa maana mbinguni Dhambi haitainua kichwa chake tena Nah 1:9. Maana hakuna anayetaka kustarehe mbinguni kisha mtu akaja kumpiga konde, au akamwibia kiatu chake!

### 103. Nimpeleke mtoto wangu wa miaka 6 shule gani kusoma?

Zamani tulipeleka watoto wetu shule za serikali bila kujali sana. Ila tabia za jumuiya yanazidi kupotoka. Ni muhimu sana uamue kwamba jambo muhimu katika maisha yako ni nini? Kwa upande wangu kama mtoto atasoma nyumbani na kukaa na mama mpaka darasa la nne, itakuwa kitu chema sana. Vitabu vyaweza kununuliwa na mtoto akajifunza nyumbani na kuwa na mwalimu mmoja mwanafunzi mmoja, kwa kawaida mtoto anajifunza vizuri kuliko mazingira mengine! Ila kwa sababu

wakina mama wengi wameingia vibaruani, na wengine hawajapata fununu kumfundisha mtoto wao nyumbani, hapo ndiyo shule za kuchagua zinakuja. Kwangu ni muhimu mtoto afunidishwe imani, kusoma na kulitii neno la Mungu aamkapo na aendapo kulala. Hivyo, kama familia ina uwezo ipeleke mtoto kwenye shule inayofundisha imani ya kumpenda Mungu. Sipendi kupeleka mtoto wangu shule yoyote. Najua shule nyingi zenye ushindani ni nzuri mtoto asiwe mvivu. Mtoto anapasa kujali matokeo yake ya mtihani. Mzazi apeleleze vizuri kwenye wizara ya elimu, kwa wazazi wengine na kadhalika kujua shule nzuri kwa tabia na taaluma. Kuna wengi ambao itabidi wapeleke mtoto wao kwenye shule ya jumuiya kwa vile hawana uwezo ila mzazi mfundishe mtoto wako nyumbani pia. Niliona watoto 100 kwenye darasa moja. Na pia kuna shule mama Fulani aliniambia mvomero miaka ya nyuma, ilikuwa na watoto kama 700 na mwalimu mmoja!. Je mzazi aweza kununua vitabu na kuanza kufundisha mtoto wake hesabu na kusoma darasa la kwanza na la Pili? Wazazi wengi wajua kusoma. Kitabu cha kujifunza kusoma mwaka huu nimeona ni kama dola mbili au tatu. Watu wengi wanapesa ya kununua vocha/credit za simu , je vitabu si muhimu zaidi? mtoto wako asifike darasa la pili hajui kusoma na kufanya hesabu rahisi, mtoto anayekumbuka kwa wepesi huchukua miezi 3 tu kujua kusoma!

### *105 Watoto wangu wanagombana mno nifanyeje?*

Wanandugu kugombana imekuwapo toka wakati wa Kaini na Habili hata kabla ya runinga! Chanzo kikubwa ni mashindano na wivu, kwa kifupi ni mimi . mimi, mimi (me, myself and I). Kitu kikubwa usiwalinganishe, kwa na kuwa na upendeleo. Usilinganishe tabia, maumbile, taaluma au talanta. Hili limekwaza wazazi wengi. Endelea kufuwafundisha tabia au kanuni ya kuishi pamoja, wengi wanapokua tabia hii hupungua, na kupendana sana. Wanasema watoto wanaofuatana ndiyo wanaoneana wivu sana. Kitabu cha Warumi saba kinaeleza msingi wetu wa kufanya maovu "kile tupendacho kufanya hatufanyi, bali tusichopenda cha dhambi twajikuta tumefanya! Ole wangu mimi, ni nani atakayeniokoa katika mwili huu". Mkumbushe mtoto kwamba ibilisi apenda awe analumbana na kuwa kama bisi, ajitahidi kumpinga, ni mafundisho ya kila siku, na kuomba Mwenyezi rehema zake. Nimeona maombi tu ndiyo silaha. Spurgeon Mhubiri alieyeanza kuhubiri akiwa na miaka 16, na akiwa na miaka 20 alikuwa na kanisa la zaidi ya watu 2000 alisema "Ni afadhali nifundishe mtu mmoja kuomba kuliko kumi kuhubiri". Maombi ni nguvu nyingi katika maisha ya ulezi, waombee watoto.

***106. Nina mtoto ambaye ana uzuri wa uso, ana miaka 8 na kila mtu anamsifia, je hili ni jambo zuri.***

Kwenye dunia yaleo ambayo watoto wengi wanaanza kutojiamini na kutojithamini, itamsaidia kujikubali. Uzuri imekuwa kama nguvu (power) hasa kwaajili ya runinga na mambo ya maonyesho mengine. Ila hili laweza kuwa hatari, kwa mfano kwa msichana wa miaka 14 ambaye ana uzuri wa uso na shepu nzuri, aweza kupata attention ya wavulana nyingi na kumwingiza kwenye majaribu ya ukahaba na kuharibu maisha yake. Hivyo mzazi ni vyema amwambie japo kuna macho yanakutazama, wewe ni nani na malengo yako duniani ni gani. Kushugulikia usafi wa moyo, taaluma aambiwe ni muhimu. Maana hayo hayatakimbia, yana siku zake yanakuja tu. Utafiti ulifanywa wa wasichana na wavulana wazuri baada ya miaka 25 waliona kwamba wengi walikuwa na ndoa zisizo na furaha. Hii ilitokana pengine na mashindano ya watu wa tabia mbovu kuwakimbilia. Wa wastani au mtu mwenye sura ya kawaida anapata wale watu wanaompenda kwaajili yake na si sura au talanta. Na pia uzuri unapoisha uzeeni, kwa wale wanaoingiza uzuri kichwani kupita kipimo wanachanganyikiwa kwamba sasa hakuna anayewatazama au kuwathamini sana. Wamekuwa wa kawaida na hili laweza kuwaletea shida. Kazania tabia ya kicho kwa Mungu, ndiyo Uzuri bora lupita wote. Mcheza filamu Marilyn Monroe ni mfano wa watu waliopata hiyo shida. Mara nyingi ukiweka uzuri kwanza kuharibikiwa ni kwingi. Kupima mtu kutokana na uzuri wa sura au talanta ni makosa. Mmeona hili limetokea kwa wacheza muziki wakikimbiliwa na watu ila maisha yanalemea pande moja. Wazazi hapa epukeni kulinganisha watoto, na kusema maneno bila kufikiri kwa watoto wengine "nywele zako mbaya, kipilipili cha kutisha" ni nani alikuambia kwamba nywele fulani ni mbaya au nzuri? Muumba wetu hajaandika hayo kwenye Neno lake?.

Mtoto anathamini tathmini yako. Usimfanye apondeke moyo bila sababu. Watoto wanahitaji kupendwa na kukukubaliwa. Kaka Restrapo alisema kwamba shangazi yake mmoja alipendwa kuliko wengine kwasababu alikuwa na rangi ya kahawia, na nywele zilizonyooka, na akaruhusiwa kufanya vile ndugu zake hawakuruhusiwa, hii ilimfanya asikomae (immaturity), hata leo ana miaka 70 bali ana mazungumzo ya kitoto na kila alipoolewa aliachika kwa kutoheshimu watu kule. Hichi ni kilema kibaya Kumpa mtoto

106. ***Madoli ya kampuni ya Barbie yana wanasesere watu wazima warembo sana wenye maziwa, wengine hata wana mimba. Watu wengi wamesema si mazuri unafikiriaje?***

Kwa upande wangu hata mimi madoli ya namna hii sipendi mtoto wangu awe nayo. Kwa namna fulani yanakuza uzuri wa sura, uasherati na pesa. Mtoto anaanza

kujipima na madoli hayo. Mtoto anapocheza anahitaji sanamu za watoto wadogo si watu wazima. Watoto hawa ni wadogo, wasikuzwe kushugulikia mambo ya watu wazima hata upevu wao wa mambo ya kiutu uzima utakuja mapema bila kupanga. Chagua wanasesere wako vizuri, chunguza. Wengine wana majitu ya kutisha tisha ya mazimwi kama Ninja, ndiyo wanasesere. Macho kama ya nyoka n.k. Unajenga mvuto wa aina fulani pia na hayo. Watoto wadogo wachezee vitu vya kawaida visipeleke mawazo yao pale ambapo haisaidii kimaadili, kijamii au kiroho. Wasipende kufanana kwa nguo, rangi, miziki au maneno na hawa wanasesere. Mtoto wa kike aliyekuwa na sura ya kawaida akijilinganisha na hawa ataona kama ameachwa na basi na si kweli. Thamani yake si kuonekana kama hawa wanasesere. Mungu anamthamini kama yeye. Mungu ameumba watu tofauti kwa utukufu wake.

104. ***Nimesikia mtoto wa katikati ana shida ya kujiona hana nafasi maalum kwenye familia ?***

Nni kweli , mtoto wa kwanza au wa mwisho, au mtoto wa kwanza wa kike au wa mwisho wa kiume wanaona wana sehemu maalumu katika familia kuliko mfano msichana wa tatu na wane katika familia ya watoto 5. Anakuwa amezaliwa pia wakati amekuta wengine. Na wengine baadaye wanamfuata anakuwa katikati. Wazazi wachukue muda wa kuwaonyesha watoto wao kwamba wanawathamini, na hasa watoto wa katikati. Mama na baba wachukue muda wa kutembea na mtoto mmoja mmoja, kwenda mahali hata kama ni karibu sokoni, ili wajue wao si namba tu. Au wapewe nafasi ya kuchagua mahali au kitu mara ya kwanza ili wajue wanathaminiwa kama wao. Dr Lehman ameandika mengi kuhusu nafasi hizi, ila si kanuni ambazo hazibadiliki, ni general information.

***Nnawaachiaje watoto wangu uhuru waende makwao wakiwa watu wazima?***

Hili ni jambo gumu sana maana kwanza tunafikiri hawako tayari na watapata shida ulimwenguni na watu hawatawafanyia mema kama sisi. Pengine tunaona wapo hatarini kiasi Fulani. Jambo jema kupita yote kwa mtoto wako ni kumfundisha aishi bila wewe! Kuwa tayari kuwa huru ni kwamba umewafundisha majukumu! Tumefanya kazi ya upendo, na sasa imeisha! Tuko ukingoni hatujui kama tulie, tufurahi au tuendanaje na upweke. Tuna tiara mkononi tuiachie? Ila mara zingine tunaona ugumu kuwaachia kwa vile thamani yetu ya maisha ilikuwa imeganda kwa watoto hawa, na tunaogopa watakuwa huru na hatutakuwa na nguvu nao tena. Au tulikuwa hatutajenga mahusiano na wake au waume zetu, na sasa hatuna cha kuzungumza pamoja (empty nest syndrome). Kuna wakati kwa kila kitu, wakati wa kutupa jiwe na wakati wa kuokota. Umefika wakati wa kuiachia tiara iende, umeshafanya kazi yako. Iachie tiara iende ili muwe na mahusiano ya urafiki mapya

yenye zawadi zake. Tiara itajiachia kwenda yenyewe hata usipoaichia ila wewe iachie wakati ufikapo ili iende kwa namna nzuri. Msiachene kwa magomvi na malumbano achaneni kwa upendo mkifurahiana

### *105. Je niwalipe watoto wangu kufanya kazi za nyumbani?*

La hasha! Watandike vitanda vyao, maana ni wao wanavilalia. Wasafishe vyombo maana ni wao wanakula! Usizoeshe kulipa watoto kwa kazi. Waweza kuwalipa kwa kuwapa motisha kazi chache mno. Mfano kusafisha baiskeli ya baba, kulima bustani zaidi ya mpango wa kulima wa kila siku n.k wakumbushe, matumizi ya pesa ni mahitaji na si matakwa. Watoto wanapenda wanunuliwe hiki na kile kama sisi watu wazima tu. Pesa yenyewe ni ndogo hata kwa mume na mke sasa watoto wakitaka itakuwa ngumu. Ukiwa na uwezo kuwapa pesa ya posho kidogo mara moja kwa mwezi si vibaya , ila wabuni miradi yao. Waweza kuuza mayai ya kuchemsha, au magazeti au maji. Wasaidie kubuni na wape mtaji wafanye masaa Fulani kwa wiki. Zaidi wapaswa kuwasaidia kwenda chuoni, kupata ardhi, mitaji au ustadi wajitegemee. Huo ndiyo urithi wao. Ila wasitegemee kwamba utawapa mali. Jaribu mali usaidie watu wenye mahitaji kama yatima, wajane, masikini na kazi ya kuongeza ufalme wa Mungu. Hata kwenye hati ya mirathi usisahau ukiwapa watoto wako kitu kumega fungu la kusaidia kazi ya Mwenyezi Mungu. Ni haki hata mimbo mingi ya taifa yaomba Baraka toka kwa Mungu hivyo najua waafrika wengi Mungu ni ngao na baraka kubwa.

### **106. Nitajuaje watoto walio kata tamaa, wasiojithamini au walio na huzuni? Discouraged or depressed**

Dalili za watoto hawa ni kutotulia mahali pamoja, kujitenga pembeni na wengine (withdraw), wanakuwa wazito na kutofautiana na ratiba ya watoto wenzao, wanakuwa wakaidi, wenye uvumilivu mdogo, wanafikiri wanahitaji hiki au kile kama marafiki zao. Wanakuwa wakali na wana tabia ya kuvunja sheria. Vya kuangalia hapa ni kama tabia yako! kwanza je unafoka foka, na kumkejeli bidii zake? Unazungumza na mke au mume wako kwa adabu mbele ya mtoto?. Mara zingine ni kumpeleka kwa tabibu aende kumwangalia kama kuna shida ya afya kama matezi n.k. mtoto mshugulishe na kumfundisha nyumbani kwa mpango na ratiba na pia asiwe anakula vitu vya sukari, mafuta, kukobolewa au chumvi nyingi. Mtoto afundishwe kujikana nafsi na kuhudumia wengine nyumbani, kwenye jumuiya au kwa wagonjwa. Angalia kama ana lishe bora, na mazingira ya kufaa, waombe wataalamu pia wakusaidie.

Nitatoa mfano mmoja wa Ninapoishi: waligundua wavulana wadogo weusi (Black americans) walikuwa na shida za hisia kuliko wengine. Mwalimu mmoja alisema

*ilitokana na kuishi na mama tu bila baba, na mama wengine walikuwa wana tabia ya kuleta marafiki wa kiume nyumbani, na kumkemea kemea mtoto. Mtoto alijiona ametengwa, na kuishi kwa hofu. Watoto hawa walizaliwa na urithi mkubwa wa akili, ila baadaye hisia zao zilikawa nzito na kuwafanya wasijisomee, na kujiachia kimasomo*

107. ***Nina mtoto kilema je nifanyeje naye ili aweze kujenga ustadi?***

Watoto wengi vilema wanaachiwa wajifunze na kupata maarifa wenyewe hasa kwenye nchi zetu za kiafrika. Upendo ndiyo hitaji lao kubwa na kisha peleleza habari za watoto kama hawa na jinsi ya kuwasaidia. Wawe vipofu, viwete, viziwi, bubu, wanaojifunza pole pole n.k. wanaweza kuwa na upungufu kwenye hiyo nyanja moja ya maumbile ila wana talanta nyingine tu. Mungu anawapenda kuliko sisi. Mzazi anza kuzifanyia kazi hizo kwa mpangilio na ratiba. Wengine wameweza kutumia vyombo vya muziki. Usiruhusu mtoto kuitwa majina nawe au wengine. Mpatie nafasi ya mazingira mbali mbali ya viasili, miti au maua. Wengi waweza kufundishwa bustani, kusuka vikapu, au kusoma kwa tarakimu tofauti za kugusa na vidole (braille). Fanya nao kazi na kuwashugulisha, usikae tu na kuwaonea huruma na kuwalemaza maana wengi wanaishi maisha ya kawaida hata kuwa na miji yao. Wale wanaosikia wasomee kila siku. Hata kama una kitabu kimoja tu cha neno la Mungu kinatosha. Uwe na utajiri wa uvumilivu, upendo na uelewaji. Kwa wale wenye shida ya viungo, uliza ushauri wa mazoezi ya viungo. Wafundishe thamani ya huruma, kupewa majukumu, uaminifu n.k, Zaidi omba nao na kuimba nao toka wakiwa wadogo wamwelewe Mungu kama rafiki, na wajifunze kumtukuza. Naomba uangalia maisha ya kijana Nick vujevic kijana aliyezaliwa Australia bila mikono, miguu, ila alikuwa anaona hana tabú au hakutahayari (Google tovuti -no hands, no legs, no worries). Huyu alitaka hata kujiua maana watoto walimcheka sana akiwa shule toka utoto. Mungu alimsaidia kupata wazazi wanaompenda Mungu na kumpa faraja ya Mungu, hii ilimfanya ajithamini. Amezungumza kwa watu milioni 4, ameoa na ana mke na mtoto. Anatembea dunia nzima kutia watu wazima na watoto moyo. Amekutana na vile wengi sana. Anasema hata hawezi kumkumbatia mkewe au mtoto wake, ila mbinguni ataweza kufanya vile, hata kuweka mikono mifukoni. Hebu mzazi apeleke kutindikiwa kwake kwa Mwenyezi Mungu atafarijiwa siku kwa siku na kushinda.

***111 Sipendi kurudia rudia mambo na kuonekana kama nafuatilia sana mtoto,*** nataka niwe Mwema (sweet) kwa mtoto.

mtoto anahitaji kufuatiliwa, na kuambiwa mambo Fulani akifanya vibaya inabidi uzoee hili akilini mwako. Ukiacha kufuatilia ufanisi unakuwa mdogo. Jitahidi kutawala sauti yako isiwe ya kufoka, uwe na uvumilivu, na mtoto aone uko upande wake (best interest). Ukisema uachilie tu, na hasa wakati ukiona mambo yameharibika utakuwa na hasira kali zisizoweza kutawaliwa (lose control). Hiki nimekiona kimetokea, hasa kwa wakina baba. Wakina mama wanaonekana wanambana mtoto na hawamwachii nafasi, mpaka mtoto anaona kwamba baba ni afadhali, baadaye baba ambaye amejiziuka akiona mambo yameharibika na alikuwa hana hata fununu, anapoteza uthibiti, na kuanza kugomba na kutoa adhabu nzito nzito, pahali ambapo angekuwa amefuatilia asingefikia stage ya kufanya kitu ambacho hata baadaye akajutia.

Zaidi ya yote, mtoto ajue kila kitu kina matokeo (consequence), mfano usipotoa magugu kwenye bustani leo, basi sitakuchukua kwenda mjini na wewe. Saa ikifika ya kwenda mjini mwage uende. Jaribu Kutna matokeo (consequence) zile anazozipenda. Mfano maliza kupiga deki, ndipo utakula Chakula cha mchana. Sipendi Kutoa adhabu na Chakula, ila ukiona mtoto ameshakula kifungua kinywa, basi aweza kuvumilia, adeki ndiyo ale Chakula cha mchana. Marafiki zangu wanaofundisha watoto vyombo vya muziki, watoto wanaochukia mazoezi, waliona ni vyema wabadilishane na mama wengine, ili waendelee kuwa na urafiki na watoto. Mungu atakapa hekima. Nami sijafuzu nipo bado msituni kwa hili, tuombeane!

Ila Narudia, kwaajili yang una kwako, upendo Wako kwa mtoto ulingane na adhabu, kama unamchukia mtoto, usimpe adhabu,

### 108. mtoto alitishia kujiua nikaona ni maneno tu na akajiua, nasikia dhamira inanishitaki pengine ningefanya kitu Fulani angekuwapo leo

kwa kweli swali hili ni gumu na hakuna anayeweza kulijibu maana sisi hatujui mtoto anafikiri nini, ameumia au kuumizwa kiasi gani, anasoma au kushirikiana na nani au kwa kifupi ni nini kimetendeka?. Mzazi mmoja mtu mzima alienda Marekani na mke wake kusomea uchungaji, akasema akamwacha mtoto wake wa form 3 boarding na walezi pia wa kuangalia mambo. Mtoto alitishia kujiua wasipokwenda naye Marekani. Baba alimwita mtoto akasema "ukijiua sisi tutasikitika sana, kwani tunakupenda mno. Ila wewe una uamuzi. Sisi tunaenda kwa muda wa miaka 3 na mama yako na tunatafuta njia mpate visa mjiunge nasi, ila sasa bado mambo hayajulikana kwani hata sisi tumechangiwa tiketi na watu. Wewe vumilia. Mtoto aliendelea kutishia, walikwenda shule marekani mwaka wakarudi kuhubiri nyumbani Tanzania mtoto akiendelea kutishia . walimwita wakamwambia wewe sasa ni mkubwa wa miaka 17, tunakupenda mno. Wakamweleza kwa undani zaidi thamani yake kwao na kwa Mungu "ila kama unataka kujiua, sisi hatuna uwezo wa

kukubadilisha usifanye. Ila tutamwomba askofu x afanye mazishi yako maana tunaenda na hatuna uwezo, tuko mbali kuja tena, tutalia sana kwa uchungu, ila wewe ndiye mwenye usukani wa uhai wako''. Mtoto huyu hakujiua alingoja wazazi wakamaliza ile miaka 3. ila chunga sana! watoto wengine huwezi kuwaaambia haya, wataendelea mbele na kujiumiza. Ila soma masomo ya afya kidogo wanasema, mtu akitishia uichukulie maanani, uliza maswali kama, watatumia njia gani, na sababu gani, na utafute msaada wa kisaikologia kushauri, Maana jambo hili ni zito, na huliwezi mwenyewe. Na zaidi ya yote mwombe Mungu Akusaidie, maana hata wao wa saikologia wanaweza chembe ndogo na wao makubwa na mazito yamewatokea wakashindwa kuyahimili. Ni Mungu tu, ndiyo Atakutoa kwenye shimo hilo. Uwe mtu wa kusali ukikikesha

113. ***Jitahidi kumkumbusha mtoto wangu kila mara na sasa ana miaka 11 ''piga mswaki, paka mafuta, kumbuka daftari la kwaya " n.k. ni lini nitapumzika nisiongee ongee***. Ana adabu ila ni mvivu na ni goigoi wa mambo fulani.

kwa kweli watoto wengi wahitaji kukumbushwa! Ila yaonekana yale wanayopenda hawayasahau!. Niliuliza watoto wangu mbona mnasahau kupiga mswaki ila hamsahau kula? Kwa kweli uzazi ni kazi ya kujifunza na pata potea nyakati fulani! (guess work) unajaribu kinachofaa kwa watoto kisipowezekana unajaribu kingine alimradi wakumbuke. Watoto wa zamani kwenye neno la Mungu akifika miaka 12 alihesabika kupewa majukumu mengi. Ila Mtoto akiishi kwako bado una jukumu kumkumbusha meno. Andika na ratiba kwenye chumba chao. Mwambie anawakilisha familia yako, hivyo akitoka na chakula kimemwagika kwenye nguo ni wewe unapata aibu. Mara zingine mwambie lazima uache demokrasi na kuamrisha kitu Fulani kifanyike! Kuna haja ya kutii sheria za nyumba. Watoto wanajifunza kuwa watu wazima. Hawajaota mizizi. Tukisoma maisha ya Ezekiel na hata ya Yesu alitoka nyumbani na miaka 30. Mara nyingi kabla ya hapo makosa mengi yafanyika. Uzoefu waja mtu akifika 30 hivi! Pengine mapema kidogo kwa wasichana. Na ndiyo maana wengi waliofanya ndoa baada ya miaka 30 wanavumilia kidogo kuliko waliooa mapema.

Lakini mtoto ajue matokeo ya kutochukua majukumu, mfano hatutakula Chamula cha usiku mpaka nguo zako zimefuliwa, hutapata posho yako ya mwezi huu mpaka umepanda ile miche ya maembe niliyoleta.

114. ***Mtoto alale masaa mangapi?***

mtoto aliyezaliwa kuanzia masaa 18 hivi, mtoto wa miaka miwili masaa 12-13, mtoto wa miaka miwili mpaka sita masaa 12 hivi, mtoto wa darasa la kwanza

mpaka la tano masaa kumi mpaka kumi na moja, mtoto wa miaka 12 na kuendelea masaa tisa mpaka kumi. Watoto wale wa miaka kumi na wanachelewa kulala waambiwe walale mapema na wasilale zaidi ya saa nne asubuhi. Watu wazima hata watoto wanaolala sana pia ni shida. Mfano mtu mzima anayelala zaidi ya masaa 9 kila siku aweza kupata magonjwa Fulani. Angalia umri wako na masaa ya kulala iwe masaa 2 kabla ya saa sita ya usiku. Watoto wadogo wa wakilala baada ya saa tatu wanaongeza riski ya kuugua kisukari. upungufu wa saa moja la usingizi kila siku kwa wiki moja ni sawa na kukosa usingizi kwa siku moja nzima, na kuongeza rsiki za ajali. Na deni la usingizi halilipiki! Linauchosha mwili.

***116. nilipeleka watoto wakiwa wadogo Amerika kusoma na wananiita niende kuwatembelea ila sina nafasi. Mzee ni mtumishi wa serikali nami nafuga ng'ombe na hakuna wa kumwachia.***

Ni muhimu kutembelea watoto. Watoto wanakuwa na ukiwa hasa wale walienda kusoma wakiwa wadogo wa miaka kumi na, mpaka ishirini na. Hawana uongozi, mashauri na marafiki wanaowajali kama wazazi. Wengi hawamalizi shule na wazazi wangejua wangewatembelea mara kwa mara bila kujali pesa. Watoto wengi wameachia shule katikati. Hata baada ya miaka 10 hawana shahada, na mara zingine wazazi wanaendelea kutoa msaada. Nachoelewa hapa kwamba shida si pesa ila muda. Wengine hata hawawezi kuhudhuria arusi za watoto au kuwapa mashauri ya wachumba. hii imefanya watoto wengi waishi na watu tu bila ndoa. Na kujiletea maumivu mengi. Mara zingine waoe mtu mkatili ili kupata makaratasi ( uraia).

Watoto wamekosa watu wa kuwashauri na kupima watu hawa. Wengi ya watu ni wale ambao hawajulikani walipozaliwa, makuzi yao au kama hata waliacha wake/waume nchi walizotoka. Mtoto anakutana na milima, wakati wazazi wanajali ngombe au kibarua!. Nafikiri ni vyema watoto wetu tuwalete wakiwa wamepevuka kidogo, kama shahada ya pili, Marekani si mbinguni, mtoto anahitaji msaada wa mzazi bado ili akabili maisha. Watoto wengi wameacha kumwabudu Mungu, kuingia kwenye ulevi, au maisha ya anasa ambayo familia haiafikiani nayo. Kuna wengi saana wanaokabili maisha vizuri bila kuja kusoma magharibi, fanya utafiti na kuona lile linalokuwa msada kwako na kumpa Mungu utukufu.

Kuna wazazi pia wanaoenda nje ya nchi kwa muda mrefu kwa kusoma au kibarua na kutelekeza watoto. Wengine huandika barua, hupiga simu na kutuma vitu ila hili si mbadala wa kuwa na mtoto. Watoto wengi wamepata hasira na kuchukia wazazi, wengine wamefanya maamuzi mabovu kwa kutokuwa na uongozi. Baba fulani wa malawi aliyekuja Tanzania kwa vibarua, nilikutana na binti yake Marekani, aliyeniambia kwa hasira baba alivyowatelekeza akiwa na miaka 6. Nilijaribu kumtafuta mzazi huyu Dar na kumpata, alikuwa na hali nzuri, makanika mwenye

gereji yake, ila hakuwasiliana na watoto na mke kwa miaka zaidi ya 30. Mama mwingine wa Botswana (daktari) aliyetelekezwa na mume (daktari wa meno), alimwachia mtoto dada yake amtunze mpaka alipokuwa na miaka 16, alienda kumwona, mtoto ili amlete. Mtoto alikuwa na jazba, alimleta mtoto na kuishi naye Washington, na mtoto alimhuzunisha mama kila mara kwa kusema kwamba ametelekezwa mpaka mama alijinyonga mwaka huu. Hii ni habari ya kweli, maana rafiki yangu ambaye alikuwa dada wa huyu mama aliniambia siku moja kwamba anaenda kwenye mazishi ya mdogo wake aliyepatwa na huzuni hii, mpaka hakujua jinsi ya kusonga mbele. Niliwaza, baba na mama walikuwa na uwezo na makazi makubwa makubwa waliyopokea angalau dola 20,000 kwa mwezi, ila mtoto hawakuchukua hatua nzuri na akawa msumari wa moto kwao. Walikuwa na mtoto mmoja tu! Mara zingine sidhani kama kuna nafasi bora kuishi na watoto! Kama ni Wako, ishi nao tu, kwa shida na furaha.

***117. huwa nachukia sana mtoto akiropoka kwangu maneno mabaya. Mfano "sikupendi, mzazi gani wewe", au "nakuchukia sana mama"***

Kwa kweli maneno haya ni mazito kwa mzazi, na hakuna mzazi ambaye anaweza kuyastahimili. wasemavyo wahenga, ni kweli "mzazi ni jalala" ni kweli. Angalia maneno haya mtoto anayatoa wapi, na ana maana gani nayo. Jaribu kutafuta moyo wake "mwanangu nipe moyo Wako" zungumza na mtoto sababu ya hasira hizi , na kusema maneno bila ya kufikiri, maneno haya yaweza kuendelea ukubwani kwa walimu, mabosi, mke au hata watoto wake. Mtoto afundishwe jinsi ya kuzungumza hata kama hakupendezwa na kile anachokanywa. Mzazi pia asichokoze, au kumkasirisha mtoto bila sababu. Mzazi aepuke hasira na harara ya kumjibisha mtoto akizungumza haya. Atulie kabla ya kuzumza na mtoto, maana aweza kumdhuru mtoto kwa kauli zake au laana. Mtoto ni mtoto, na tembo hachoki mkonga wake, mwombe Mungu na kujua sasa una wakati wa kumkunja samaki akiwa mbichi.

Wazazi hapa nasi ni wakati mzuri wa kujua kwamba hasira ni dhambi na si msaada kwa tabia ya mtoto. Hasira ni Pepo, kama tulivyoona wakati Yakobo na Yohana wana wa Ngurumo wakiomba wapewe mamlaka ya kuleta moto uangamize sehemu Kubwa kwa vile walikataa kuamini au kuwakaribisha Luka 9:51-56. Hasira ni chukizo, na ni roho ya chukizo. Twakataza watoto wetu wasiangalie vipindi vibaya, wasiabudu sanamu au wasiseme uongo au kufanya uasherati bali tunaingiza ndani ya nyumba hasira.

Mzazi mmoja alijisifu kwamba yeye hana vipindi vibaya vya TV nyumbani, watoto anawasimamia vizuri, ila alikuwa akipatwa na hasira watoto wanakimbia. Aliposema

kwa mshauri kwamba anashangaa watoto wake wana tabia mbovu, aliulizwa "je una hasira?", alijibu

"mara moja kwa miezi miwili", Yule mshauri alimwuliza, je ukiwa unaishi karibú na volcano ambayo inalipuka kila miezi miwili utakaa hapo?" au "ukiwa na mbwa anayeuma watu mara moja baada ya miezi miwili, utaendelea kumfuga?". Hasira na lugha mbaya, wizi, uongo, uchawi na dhambi zingine, ni sawa. Hakuna binadamu ambaye ana hasira akayafanya mapenzi ya Mungu sawa. Yalimkuta Musa, kwa hasira yake alijikuta kwenye shida nyingi.wengine wamefikiri kwamba kuna hasira takatifu (righteous indignation). Nafikiri hii ni Mungu tu Ambaye anaiweza, sisi hatuwezi kuwa na utakatifu na hasira.

Neno la Mungu limetaja hasira mara 585, na mara 470 inazungumzia hasira ya Mungu, mfano kwa Akani, Uza, Joram, Manase n.k. Wazazi tumwombe Mungu tuache hasira, nimeingia mara nyingi kwenye mtego huu na ninamwomba Mungu. Hasira inahusiana sana na kisasi, ukiwa na hasira kwa mtoto, chukua muda kupoza hasira ili hata ukitoa adhabu usifanye kwa kisasi, na mtoto asirithi hasira yako, maana nimeona kwa mifano halisi ikienda kizazi hadi kizazi. Kuna tofauti kati ya hasira na kukazia, wahubiri wengi wamehubiri kwa hasira wakifikiri ni mkazo au ni maadili ya kumsahihisha mtu ila ni hasira.

Basi mtoto anayelipuka na hasira nakusema ovyo ovyo, anabidi asaidiwe, maana Pepo la hasira limeleta maovu au madhara mengi.

maswali haya yamejibiwa kwa fikara au maoni ya mwandishi ambaye anaamini kumcha Mungu ndiyo chanzo cha maarifa. Mwandishi anaamini kwamba kulea mtoto bila msaada wa Mungu ni kitu kisichowezekana. hatuwezi kuishi bila Mwenyezi Mungu na ni lazima tuwaeleze watoto wetu ili wamwabudu na kumjali katika maisha yao ndipo mema yatakaowajia. Watoto bora na wazazi au walimu bora ni wale wanaochukua muda kumtafuta Mungu. Yote yatapita ila Yeye ni wa milele. Yeye ndiye anayetatua matatizo yetu siku kwa siku. Binadamu atakusaidia kidogo tu, ila mkabidhi Mungu atakutatulia yote na Atakupa faraja na kisha uzima wa Milele.

***118. Je kuna tofauti gani kati ya malezi ya magharibi na kwetu afrika?***

Mengi yanategemea na nyumba au familia, ila magharibi mtoto akifanya kitu anaachwa, hakanywi na majirani au yoyote. Pengine tofauti ni maisha ya kileo na zamani. Kijiji hakihusishwi. Sheria zingine za serikali zinamlinda mtoto mpaka,

mzazi anakosa la kufanya, ila akiharibu mambo akifika miaka 18 polisi aweza kumchukua.

Ila mfumo wa elimu unasaidia watoto vizuri magharibi, hata wenye uwezo mdogo wa D wanaweza kumaliza polepole kutokana na kasi yao hata kama ni miaka kumi wamalize shahada. Elimu ya magharibi ina project na vitendo, vitu vinavyohusu maisha ya kila siku, ila elimu yetu haikuwa na project, ila kukariri na nadharia. Mahali pengine watoto wengine wengine ukiwakanya wanasema wananyanyaswa. Kuadabishwa magharibi mara nyingi kiboko kinapungua kuliko kwetu afrika. Na kule afrika huwezi kumwambia mtoto utachukua michezo yake au wanasesele, kwa vile anatengeneza mwenyewe.   Pia kumwambia mtoto adhabu ya 'kakae kwenye kona' haina maana maana, hata hiyo nyumba haina kona vile. Watoto hawaulizwi unataka kula nini, bali twawapa tulicho nacho, mambo ya kulala kwa watu wasio jamaa hayapo. Pia kusifia watoto mpaka kuwapa zawadi wenzetu wanatuzidi.

Watoto afrika wanajiunga kucheza pamoja bila ya kusema 'Je mimi ni rafiki yako au nicheze na wewe' mnacheza pamoja bila sheria au urasmi. Afrika watoto wakiwa wanacheza pamoja, mzazi ukienda dukani unaenda nao, ila hapa unawaambia waende nyumbani kwao, na mara nyingi wakati wa chakula wanaenda kwao. Kuwafundisha watoto maumbile na ngono si wazi, ni kama siri na hayafundishwi wazi labda kwenye jando na unyago. Watoto huambiwa shangazi atawafundisha. Sehemu za siri kwa kingereza ni darasa   la sayansi ila lugha zingine za afrika inachukuliwa kama matusi.

Ukiishi na watoto wa kike wa jamaa wanakusaidia kazi za nyumbani, na wanapaswa kuja mapema nyumbani. Kweli mambo ya kileo yana upungufu mwingi wa kiroho ila unene wa miili.

Ila watoto wote ni sawa kwa kucheza, kuchora kwenye udongo, yaani ulimwengu wa mtoto ni sawa kote.

***119. kwanini watoto hawaalikwi arusini siku hizi wakati arusi kilikuwa kitu cha wote? Watoto wanaona kwa matendo, kama hawaendi arusini watafanya arusi kweli? Ni kama mahafali ni muhimu kuhudhuria ili waone ni kizuri nao wafanye***

***(wamechangia watu watatu (Ndugu Essaba, Lima, Mavanza na Odung**a*)

Kwanza tuanze kwa kuelezea aina zenyewe za Arusi. Kwa arusi za siku hizi hata za wampendao Mungu twaona afadhali watoto wabaki majumbani na wasiyaone hayo yanayofanyika.

Arusi zetu siku hizi zinaisha usiku wa manane sio tena kama enzi hizo arusi inafungwa asubihi na ikifika saa 12 jioni kila mtu anaelekezea au anakaribia kuelekea nyumbani. Maarusi mengi yameondoa sura ya arusi na imebaki sura ya sherehe, mashindano, kujionyesha, fahari na hata uovu mara zingine.

Kumbi zinazotumika nyingi ni kumbi za starehe zisizoruhusu watoto kuingia kutokana na umri wao hata kwa siku za kawaida. Wakiingizwa kwenye arusi watagundua makubwa. Utukufu wa arusi unaachwa ibadani,na ukumbini ni sherehe, nderemo, Yesu nibebe nibembeleze nibebe . . . . .na nyimbo kama kwaito
watoto pia hawaachwi wacheze au wakae kwao na kufurahia bali wanagombezwa wakikimbia kumbini na kukoseshwa raha kwa muda mrefu wagande mahali fulani kuangalia watu wanaozungumza.
watoto wengi wamesoma kadi 'watoto tunawapenda ila usiwalete' wakashangaa tunawapenda nini?.
Mida yapotea kwa ngoma za kila kabila, babu seya,

Arusi tunamaliza muda mfupi kabla ya asubuhi, haina maana yoyote kwa watoto bali usumbufu.

Arusi zetu tumewakabidhi watu wanaitwa ma-MC, wengine wanawaita "Msema Chochote". Ni kweli hawa watu wanasema chochote. Wakianza kumsifia bibi arusi sisi wakubwa tunashangilia lakini watoto wanaona tusivyo wakweli. Bibi arusi anaambiwa ana macho ya aina fulani mara hivi mara vile, lakini watoto hawaoni hayo anayosema MC! Sisi tunaonekama kama waongo mbele ya watoto.
hata watu wanaokuja kushugulikia wanashangaa mbona arusi hii imejaa uovu?

Leo arusi ni kama deni! Usipo changia hata wewe mwenyewe hualikwi, na kipo kiwango cha fedha ambacho usipofikisha hualikwi achilia mbali na mtoto wako. Ikitokea hujamchangia mtu hata salamu zinapungua, yani kwa ujumla arusi zimechukuwa sura tofauti kabisa na ilivyokuwa. Hayo sio duniani tu, hata kanisani. Arusi hazina kiasi na sura yake inabadilika kutoka kanisani kwenye ukumbini.

Tuwaache watoto wawe salama majumbani au tubadilike kwanza turudi kwenye arusi za asubuhi, zisizo na mbembwe nyingi, MC awe mwongozaji wa arusi mwenye maadili, ukumbi utangaze utukufu wa Mungu na watu wote wajue hivyo.
hebu turudie mapito ya zamani arusi kama ile ya Kana mwujiza wa kwanza ulipotokea. Japo tunawabagua watoto wetu watakuwa madada na makaka mbinguni na si watoto wetu tena. Binafsi sisi tunaona ni jambo baya kutoalika watoto kwenye arusi, na tunashauri turudi mapito ya zamani. Mambo kama ni mabaya japo ya kileo, basi yamepitwa na wakati

1. Katika familia nyingi watoto wengi huwekwa mwishoni kwa kila jambo linalotaka kufanyika unaweza kuona mzazi anavaa suti nzuri sana na ya gharama kubwa lakini watoto wanavaa nguo za mitumba.
2. Sherehe za siku hizi ni biashara kamili kwa hiyo watoto wengi hawana kitu cha kulipia ili wawe na uwezo kushiriki katika biashara hiyo.
3. Sherehe za siku hizi ni sherehe za kidhambi:

Lazima pawe na muziki wa isiyo na minuto ya kusaidia au unaosisimua watu.
Lazima pawe na pombe.
Lazima ifanyike usiku wa manane ili watu wasiwe na aibu.
Lazima ifanyikie kwenye kumbi za starehe ili watu wa kila namna wahudhurie.

4. Wazazi wengi kwa sababu ni waovu hasa uzinzi wanawaona watoto ni wasumbufu sana na wanawanyima uhuru wa kufanya kile wanachotaka kufanya.
5. Siku hizi watoto wanathamani sana wanapokosekana lakini wakipatikana hawana thamani ndiyo maana leo utakuta watoto wanaitwa majina ya ajabu mfano Sikutumaini, Matatizo, Shida, Masumbuko, majina kama haya tayari yanaondoa thamani ya watoto hata mzazi ukimwuliza kwa nini ulimwita mwanao jina hilo anakujibu nilimzaa kwa bahati mbaya!

Maswali haya yamejibiwa kwa mafikara au maoni ya mwandishi ambaye anaamini kumcha Mungu ndiyo chanzo cha maarifa. Mwandishi anaamini kwamba kulea mtoto bila msaada wa Mungu ni kitu kisichowezekana. hatuwezi kuishi bila Mwenyezi Mungu na ni lazima tuwaeleze watoto wetu ili wamwabudu na kumjali katika maisha yao ndipo mema yatakaowajia. Watoto bora na wazazi au walimu bora ni wale wanaochukua muda kumtafuta Mungu. Yote yatapita ila Yeye ni wa milele. Yeye ndiye anayetatua matatizo yetu siku kwa siku. Binadamu atakusaidia kidogo tu, ila mkabidhi Mungu atakutatulia yote na Atakupa faraja na kisha uzima wa Milele.

***120. Napenda kupata mwangaza kuhusu teknolojia kwenye nyumba zetu za ibada leo. Pale naishi watoto hata wa miaka 6 wanakuja na vyombo vya teknolojia kama tablet, smart phone, I pod, Nintendo. Wanaleta hivi vyombo kanisa na kusikiilza muziki hata wakati huduma inaendelea, au mhubiri anatoa somo. Kitu kizuri ni kwamba kinawafanya wawe kimya au inapunguza fujo. Ila sijui kama hili ni sawa. Wengi wao wana ukarimu sana wa kushirikia hivi vyombo na wenzao. Utashangaa hata mtoto wa miaka miwili anayoweza kufanya kwenye vyombo hivyo. naelewa wakati wa kuwapa watoto kalamu, rangi na karatasi umepita. Mabadiliko haya yamekuwa haraka mno. Nami kama mama wa watoto wawili, ningependa wakue wakielewa utukufu wa nyumba ya ibda kwa macho yao, hata zaidi yakuwambiwa. Mawazo yamegawanyika sehemu mbili, kuja na Biblia kanisani na vitu vichache vya watoto kasha kuwaambia wasikilize mhubiri au kuwapa vyombo vya kisasa wajishugulishe navyo.***
***(majibu toka kwa watu kadhaa).***

(a)Nafikiri hii ni shida yetu sote wenye watoto. Kama kuna pa kusaidiana ni hapa kwa mashauri ya upendo. msukumo wa rika, na matengenezo ya moyo ndiyo shida. wewe kama mzazi ndiyo unafanya maamuzi. Mambo yakikuharibikia hakuna atakusaidia. hivyo ni vyema kuamua vizuri. Technology ni udhuru tu ila matengenezo ya moyo na kutokuwa na shauku ya vitu vya kiroho ni kwetu wote binadamu, 24/7 tunaandamwa na hili. mzee wetu wa kanisa alisema kama mama watu wazima 5 tu kati ya 100 wataenda mbinguni kwenye nyumba ya ibada, basi ni 5 tu kati ya watoto 1000 wataenda mbinguni. Hata Nuhu alinishangaza kweli hakuwa na wajukuu? Vijana wote watatu hamna mtoto! Sulemani asema mtoto ana ujinga mwingi. Watoto wana majaribu ya kuzama mengi mnooo.

na sasa imekuja kama ulevi hii I pod. Na sisi ndiyo tunanunua! Naona wazungu wengi wa matengenezo wanakiepa hichi kifaa. Tukimwona mlevi na pombe ibadani tutastuka na kuanza kumshambulia, ila sisi watu wazima na watoto, hatujiwezik tu hoi bin taabani. Tunatembea na hivi vitu saa yote, hata kukosa adabu. Siku hizi ukizungumza na mtu mara simu yake imelia hata kama si ya maana, hasemi hata samahani anakuacha kwenye mataa. mtoto wangu wa miaka sita sita aliniambia 'mama unaiependa hii simu kuliko vyote duniani, hata nyumba ikiungua moto tukikuita utakuwa kwenye halo halo tu'.
ni ulevi, hakuna ambaye ataangamia nisipopokea simu ibadani, eti mimi ndiyo najidai namwokoa au nashika zamu niko kwenye simu au gadget Fulani saa zote, najidanganya tu. Mungu wake na watu wa karibu ndiyo watamsadia; au mtu akiwa na dharura hiyo ataita ambulance apelekwe hospitali. Hata watu wazima hawaji na Biblia kanisani bali na simu ya mkononi, na wanatuma sms wao kwa wao humo humo nyumba ya ibada.
Nafikiri vyombo hivi watoto siku ya ibada waviache kutumia . Au itafanya wachukie ibada? Hata kila siku watoto wengi hasa wa shule ya msingi wawe wanatumia labda kwa saa moja tu, chini ya uangalizi, maana sasa tunavitumia kama yaya, ila mara nyingi hatujui wanaangalia nini. hata kama si vibaya wanavyoangaliaadui anawatoa kwa mema, wanasema adui wa mazuri sana mazuri kidogo. Adui aona bora awashugulishe wao nasi tu saa yote nikiamika kabla hata ya kusoma Neno la Mungu nipo kwenye mtandao, ni sawa hiyo kweli? Ni ulevi! .Sasa mimi mama mzee nikifanya vile mtoto ambaye mimi ndiye nimempa I pod ataweza kusoma neno la Mungu kweli?
mtoto akiwa kwenye I pod nikimwita maombi, anachukia, na mawazo hayawi hapo. tumestruggle na hilo, jamani kumbe wale 144,000 kwenye neno la Mungu ufunuo 7/14 ni wengi mno Ee?
Lazima tuombe usiku na mchana. maana mapigano yetu si ya nyama na damu...... bali hayo hayo tunayoyajua ambayo yako kwenye 'kipaji cha uso ;frontal lobe ' 24/7
kama kuna watoto wanajishugulisha na I pod na vitu vya kuwasaidia kiroho basi watakuwa 1% ,punguza hicho chombo sana.ninajikaza kwangu maana sikuona sababu ya kuwa na hicho chombo, ila mtu mwingine alikileta na mtoto wangu mdogo wa msingi nikasikia anacheka saa nane

ya usiku, kumbe yuko kwenye I pod. siku nyingine aliamka asubuhi kama anaumwa, baba yake akasema aende hospitali , kumbe alikuwa kwenye ipod mpaka kunakucha 11 yr old. wapendwa, hivi vifaa kama vina mazuri, nangoja kuona. maana mimi ni mtu wa zamani na ushamba wangu ni mwingi. nachojua tumlilie Mungu. mtoto hutampa kazi anachukia ataka awe kwenye chombo. washiriki wengi naowatembelea ni vile vile. tufanyeje na hivi vyombo? wazazi waweza kuonekana ni waumini, ila wote hakuna anamiliki hivi vyombo kwa hekima, labda tusiwe navyo, ila tukiwa navyo, nani anajua wanachoona kweli?
hata sodoma na gomora ilikuwa nchi ya kisasa na kileo, ila watu waliangamia. tusifikiri sisi ndiyo tofauti na tunajua sana kuliko wale wa Sodoma. Walikuwa majitu yenye akili na nguvu kupita sisi. dhambi yao ilikuwa hawakusaidia masikini, waliishi kwa ubatili, chakula kilikuwa kingi, hawakuwa na la kufanya hivyo vitu vya ovyo ovyo vikawashugulisha. Nasi watoto wetu hawana kazi za kutosha, tunawakinga na kazi za kulima, kupika na kufua, hivyo watafanya nini kam si vyombo hivi?
tusaidiane mawazo na maombi

- (*b*) Mzee Mukangara: Ni hakika sisi sote tunahitaji kueliemishwa. '*Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia; basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru*'. Warumi 13:12
- **Technology** *iletwayo makanisani leo ni utimilifu wa unabii katika* Daniel 12:4 isemwapo kuwa "Maarifa yataongezeka." Linatimia machoni petu.
- Kila baada ya miezi mitatu kuna mabadiliko. Tutafikia ambapo kila baada ya nusu saa ni technolojia mpya!
- **"Kuongezeka kwa Maarifa"** **ni ishara** kwamba, ule mwisho umekaribia. Ni kusema, kaeni 'chonjo'. Kaeni tayari.
- **Kwa wana wa nuru**, maarifa hayo kuongezeka, **ni kwa utukufu wa Mungu**. Habakuki 2:14 *"Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa BWANA, kama maji yaifunikayo bahari."*
- **Tusiiogope technolojia.** Ndiyo imetuletea **vitabu**
na **simu** tuzitumiazo, na **ndege** tupandazo, na **viwanda** vya uchapishaji vinavyochapisha **Biblia**

**zetu**, **nguo** tuvaazo, **magari** tuyatumiayo kwendea ibadani na kazini, majengo ya nyumba zetu, **fedha zetu, ATM nk** name it.

- **Walio wa nuru** hawababaiki juu ya tekinolojia.
- **Yale Shetani** ayawekayo humo, wana wa nuru hujiepusha nayo.
- **Shetani ataleta ponografia (umalaya wa picha)**, walio wa nuru hawatajishughulisha nayo. Ataleta kila aina na udanganyifu, lakini Roho wa Mungu atawawezesha kutambua hila na mitego ya Shetani.
- **Shetani asipewe utukufu wa Technolojia.** Si ya kwake. Utukufu huo ni wa Mungu Mwenyezi. Yeye ni 'mkwazaji' tu mwenye hila, akijua muda wake uliosalia **kuswekwa jehanum**, ni mchache. Anatafuta aende na vitoto vyetu na wazazi wao jehanum.
- **Shetani asipewe utukufu** wa mwanadamu kumtii kumwasi Mungu. Mwanadamu huyo ameumbwa na Mungu. Shetani hakuumba hata nzi. Yeye si muumbaji, bali kiumbe. Kazi yake - according to Jesus - ni muuaji tangu mwanzo, na baba wa uongo. Yohana 8:44
- **Tuyapinge na kuyazuia yaliyo ya Shetani** ndani ya technolojia, lakini tusiipinge technolojia. Ni utukufu wa Mungu.

- Watoto hao hununuliwa gadgets hizo na wazazi wao.
- Pale ambapo Shetani atakwaza akili za watoto hao, athari zake ni kubwa. Watoto watajifunza kuwa na miungu mingine.
- Wazazi wao "watalipa" mbele ya Atakayewahukumu wote wenye mwili.

. kuleta vitu hivi ibadani ndiyo twaita

- Hicho twaita mitego ya shetani "the snares of Satan."
- Watoto hufuata wapewacho na wazazi wao.. Wakikatazwa, wataacha. Wakipewa, watapokea.
- Wazazi wa watoto hao hawataiepuka ghadhabu ya Mungu iwapo hawatalitambua hili mapema na kuchukua hatua.
- Siku ibada ni ya Mungu wako!!!!! Tii, uishi, asi ufe. Si siku ya michezo na miziki ya duniani. Kama ni lazima, ni siku ya kutumia gadgets zote kujifunza Biblia ili watoto hao wamjue Mungu na Makusudi yake kuwaleta ulimwenguni. Mwisho wa siku wazazi

wanao wajibu wa kuwauliza watoto: leo umejifunza nini? Leo umekariri nini?

Hata kama wanatulia eti hawapigi kelele bado kuna shida maana hawafanyi wanayotakiwa katika mahali pale/

1.. Mtoto akililia wembe, na ukampa, utakuwa umemtuliza. Nakumbuka sheria za Mungunilizozikia kwa baba wa taifa, Mwalimu Nyerere, wakati wa uhai wake. Alisema, "Sheria za Mwenyezi Mungu ziko hivi: Mtoto akichezea moto, utamchoma palepale. Akichezea utelezi, ataanguka palepale. Akichezea wembe, utamkata palepale." Nini kimetokea? Wazazi wa mtoto waliona njia ya kumtuliza huyu kiumbe aombaye shari kana kwamba anaomba heri ni kumkubalia, ili awe 'calmed'. Is that positive wakati mtoto ameungua moto, au amekatwa na wembe, au ameanguka katika utelezi na kuvunjika mkono au mguu?
2.. Nabii **Habakuki** anauambia ulimwengu wote akisema, "*Lakini BWANA yumo ndani ya Hekalu lake takatifu; dunia yote na inyamaze kimya mbele zake.*" Habakuki 2:20 SWALI: Ni kwa vipi wakati BWANA yumo katika hekalu lake, wazazi peke yao ndiyo wawe humo, badala ya kuwa na watoto wao, wakafundishwa kuwa kimya mbele za BWANA? (2) Ikiwa Wazazi wamo katika hekalu na watoto wamo katika "Gadgets", je, gadgets hizo ndilo hekalu la Mungu? (3) Kama ndivyo, ni kwa nini wazazi nao wasiwe katika hekalu hilo? (4) Kama sivyo, ni mungu gani aliye katikagadgets hizo? These are rhetorical questions. Kila mmoja ajijibu mwenyewe moyoni mwake.

Kwamba wana ukarimu wa kuwapa wengine:

- Kuna Neno hili la kuaminika kutoka kwenye kinywa cha Yesu katika Mathayo 5:46-47 lisemalo hivi: *"Maana mkiwapenda wanaowapenda ninyi mwapata thawabu gani? Hata watoza ushuru, je! Nao hawafanyi yayo hayo? Tena mkiwaamkia ndugu zenu tu, mnatenda tendo gani la ziada? Hata watu wa mataifa, je! Nao hawafanyi kama hayo?"*
- "ukarimu" wafanya watu wanaotafuta haki ya Mungu na wale wanaompenda adui. Waulize wavuta- bangi: watakwambia wanavyosaidiana 'misokoto'. Waulize wavuta-sigara: watakwambia wanavyoisaidiana hata 'vichungi'. Waulize wanywaji wa "Chibuku"

wakwambie 'wanavyotikisa' jug na kunywa kwa kushirikiana - mmoja baada ya mwingine.

- Ndivyo Shetani awezavyo kuwatumia watoto wetu, na ukarimu kwa vitu ambavyo si vya msingi "vyema'

- (c) Profesa Bisanda: shida si watoto bali wazazi wanaonunua vitu hivyo. kumbukeni kwamba tunashugulika na kizazi cha Y (generation Y, ambacho ni digital, na wazazi ni Analogue! Teknologia tunayoiona hapa huwezi kulinganisha na vile ambavyo tutavikuta mbinguni. Hebu fikiria Mwenyezi Mungu atapitia rekodi za matendo ya watu wote bilioni nne, walioishi zamani na waliopo leo kwa sekunde au pungufu ya hapo. Je archive yake itakuwa kubwa kiasi gani? Naamini rekodi kule zitakuwa superior (BORA MNO? ) kuliko hizi za DVD, USB, n.k

124. Nawezaje kumsaidia mtoto wangu awe na mapungufu mengi!- bonasi!

**KANUNI 12 ZA KULEA WATOTO ILI WAWE WATUKUTU**

1. Anza tangu utotoni kumpa mtoto kila kitu akitakacho. Kwa njia hii atakuwa akiamini kuwa anapaswa kuishi duniani.

2. Anapojifunza maneno machafu mchekee. Hivyo atajidhania yu mwerevu.
3. Usimpe mafunzo yoyote ya kiroho. Subiri hadi awe na umri wa miaka 21 halafu mwache "ajiamlie mambo yake mwenyewe".
4. Epuka matumizi ya "hilo ni kosa", atajisikia hatia. Hili litamfanya aamini baadae kuwa, atakapotiwa mbaroni, jamii haimpendi na anateswa.

5. Okota kila kitu anachoacha ovyo. Mfanyie kila kitu ili azoee kuwatupia wengine kila wajibu.

6. Mtetee dhidi ya majirani, walimu na Polisi. Hao wote wanamchukia mwanao.
7. Gombaneni mara kwa mara mbele ya watoto wenu. Hivyo hawatastuka nyumba itakapovunjika baadae.

8. Mpatie mtoto fedha zote za matumizi anazotaka. Usimwache azalishe za kwake mwenyewe. 3
9. Timiza haja yake ya kila anachotamani, chakula,vinywaji na raha. Hakikisha kila jambo mwili wake unalotamani linapatikana.

10. Mwache asome kila kilichochapishwa, na asikilize kila wimbo ambao mikono yake itaufikia. Uwe mwangalifu kuhakikisha kuwa vyombo vya chakula na bilauri zote ni safi isipokuwa ubongo wake ulishwe takataka.

11. Anapokuwa ameingia matatani, jifariji kuwa "nisingeweza kumsaidia lolote".
12. Jiandae kwa maisha ya huzuni. Hakika utayapata.

Yametwaliwa kutoka jarida linaloitwa, '*Kanuni 12 za kulea mtoto awe mtukutu*' linalosambazwa na Polisi wa Houston Texas

125.Mume wangu husafiri safari sana, hii linatuwia vigumu na watoto.

Ni changamoto kubwa, mzazi anaposafiri safari, iwe ni baba au mama. WAtoto wetu tunao muda mfupi, ikiwezekana basi mzazi atafute kazi ya karibu, japo hailipi sana. Ila kuna kazi fulani lazima zifanywe. Basi mzazi aweza kupata maarifa ya kuboresha wakati anaokuwa na watoto. Mfano akirudi watoto waweze kumpokea kwenye kituo cha basi au uwanja wa ndege na kuchukua muda kuzungumza naye. Awapigie simu mara kwa mara, na kuwaandikia barua. Ajitahidi

kuwaona walimu wa watoto wake hata kama ni mara chache kwa mwaka. Apate muda wa likizo na kupanga na watoto waende mahali pamoja.

Kwa kweli ni mengi mzazi aweza kufanya akiwa mbali, na kuna vitabu vimeandikwa kwa haya. Na Tovuti itakusaidia mawazo zaidi toka kwa wazazi wengine ambao wanakabiliana na changamoto hii.

126. Njia gani ni nzuri kujenga mahusiano na watoto wangu?

Njia nyepesi 13 za kujenga uhusiano na watoto wako.

1. **Mchukue mtoto pamoja nawe kila mara unapokwenda mahali Fulani kwa gari**. Hii itakupa muda wa kuongea pamoja. Watoto wako watajifunza kutoka kwako wakati unaponunua, unapohudumu, unapoendesha, na watajifunza kutumika pamoja nawe.

2. **Fanya kazi pamoja**. Katika bustani, jikoni na nyumbani. Siyo tu kwamba hii itakupa muda zaidi wa kuongea na kuwafundisha watoto wako katika kazi unazozifanya, lakini pia itaokoa muda wako na kukuachia muda zaidi wa kuwa pamoja nao katika mambo mengine.

3. **Soma vitabu na kuangalia picha pamoja kama familia.** Hata mtoto mdogo kabisa anaweza kufurahia kuangalia picha za kitabuni na kukusikiliza unaposoma kwa sauti. Mbali na kuweka kumbukumbu za pamoja utakuza upendo wa wakujifunza na kujenga fursa kubwa za majadiliano, kuangalia na kujadili picha zinazofaa pamoja pia husaidia watoto wako kukuza stadi muhimu za kufikiri na utambuzi wa kiroho.

4. **Ongea nao – na usikilize!** Chukua muda unapowaingiza kitandani, na waulize siku ilivyoenda au wasimlie hadithi fupi. Wasikilize kwa uvumilivu wanapotaka kukuelezea jambo fulani. Anza hili mapema, na watoto wako wanaopenda kuongea nawe watakapopevuka bado watapenda kuongea nawe.

5. **Onyesha ukarimu na mjumuike pamoja kama familia.** Punguza muda ambao wanao wanautumia na wenzao wa rika moja, na tumieni muda zaidi pamoja kama familia, katika shughuli pamoja, katika kukaribisha familia nyingine nyumbani kwenu, na kuwakaribisha marafiki wa watoto wako nyumbani kwako.

6. **Tafuta miradi ya kufanya kama familia.** Kushiriki malengo ya pamoja mnapoendelea kufanya kazi na kutoa huduma pamoja vitaivuta familia yenu pamoja. Tafuta njia ya kutoa huduma pamoja kupitia kanisa lako, kuwahudumia waliozuiwa na mazingira au katika nyumba za wazee kwa pamoja, anzisheni biashara ndogondogo pamoja, iweni wenyeji wa matukio ya familia nyingine, wasaidieni bibi na babu, anzisheni mifugo, pigeni chombo cha muziki pamoja!
Imetolewa bure na Pam Forster, © Doorposts- www.doorposts.com

7. **Onyesha kuvutiwa na vitu vinavyowavutia wanao.** Baba yangu aliliweza sana hili. Usalama nilioupata katika upendo wake na mwelekeo wa maisha yangu vyote vimepata msingi mkubwa kutoka katika karama hii kubwa ambayo ni baba yangu peke yake angeweza kunipa! Kaa usikilize binti yako anapopiga kinanda, nenda kwenye mchezo wa mpira, wewe na kijana wako, jengeni nyumba ya kuchezea pamoja, choreni picha pamoja, furahieni ujenzi wa jengo kubwa, wasikilize hasa.

8. **Waonyeshe watoto wako upendo wa kimwili.** Washike mikono,wakumbatie, sema,"Ninakupenda," na kuwakumbatia tena! Ulimwengu umebadilika eti usipowaleta karibu mwingine atawaleta karibu!

9. **Panga ratiba ya kukutana na mtoto mmoja mmoja.** Ombeni pamoja! Shughulikieni mambo yanayohusu majaribu na dhambi, waambie kuwa uko upande wao, ombeaneni. Jifunze Biblia pamoja. Wafundishe wanao jinsi ya kujifunza Biblia mnapojifunza mada zinazofaa pamoja. Soma vitabu na kujadili pamoja (Mazungumzo kwa msichana, Mungu kazini, Watu wa baadae, Kuvunja ngome na Mawazo kwa vijana ni mifano michache ya vitabu tulivyokwisha soma. Pia tulisoma pamoja vitabu kwa ajili tu ya burudani). Tokeni nje kwa ajili ya matembezi pamoja. Hili tumeligundua kuwa jema hasa kwa vijana wetu wa kiume! Wakiwa njiani huongea zaidi kuliko tukiwa tumekaa nao kwenye viti vya sofa. Tokeni nje mkale pamoja. Si lazima kiwe chakula cha kupendeza sana. Hata koni tu inaweza kuwapatia muda mzuri kama vile chakula cha gharama. Nendeni nje mkapige kambi! Kila mmoja alipokuwa mdogo, sote "tulipiga kambi nje" pamoja sebuleni kila Ijumaa jioni! Pia tulipiga kambi nje usiku sakafuni pamoja na watoto na makambi ya dharura wakati wa kiangazi juu ya sitaha. Inashangaza ni kiasi gani zaidi watoto wanavyoongea tunapokuwa tumelala pale gizani! Iweni na "kutoka alasiri kwa wasichana" kila mwezi au "kutoka alasiri kwa wavulana". Hili ni wazo

ambalo nilitiwa shime kulitekeleza baada ya kusoma kitabu bora kabisa cha Carolyn Mahaney's, Maongezi ya Msichana. Mara moja kila mwezi wasichana pamoja nami tulitoka tu alasiri (au wakati mwingine kwa siku nzima) tukafurahi pamoja. Tulitembelea bustani za maua ya Tulip, Iris, bustani za Mawaridi, migahawa ya chai, maduka ya vitabu, maegesho, na zaidi, na kila mara tulikuwa na wakati mzuri sana. Kila mara iweni na wakati wa kujadili na kuweka malengo. Tulijaribu kulifanya hili angalau mara moja kila mwaka. Ilionekana kuwa ni utaratibu wa msaada mkubwa, na siku zote tulitiwa moyo, tulipoangalia nyuma na kuona ni malengo mangapi yaliyotimizwa mwishoni mwa mwaka uliopita. Angalia ibara ya Pam Foster, © Doorposts – [www.doorposts.com](http://www.doorposts.com)

**10. Waadhibu wanao.** Mojawapo ya njia bora kabisa za kuwasilisha upendo kwa watoto wetu ni kuwaadhibu kwa dhati, kwa upendo na pasipo kukoma. Mithali 13:24 inasema, " Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe, Bali yeye ampendaye humrudi mapema". Mtoto aliye huru kufanya lolote apendalo hatajisikia salama katika pendo la wazazi wake. Akiachiwa peke yake, pia atakuwa mtoto mgumu kuonyesha upendo. Karibisha mazingira ya adhabu kama fursa za kuwa karibu zaidi na wanao. Kwa unyenyekevu tukiikabili mioyo yetu yenye dhambi, tukifurahi katika neema ya Mungu na Injili ifunikayo dhambi yetu, tukiomba msamaha nasi tukisamehe – haya yote yatawavuta watoto na wazazi pamoja kama kaka na dada katika Bwana. Karibisha mazingira ya adhabu kama fursa za mafundisho. Tuna mengi ya kuwafundisha watoto wetu katika miaka michache tuliyo nao majumbani mwetu. Kila tabia mbaya, kila dhambi, ni fursa ya ziada ya kuwafundisha toka neno la Mungu.

**11. Sema wazi wazi kazi unayoiona Bwana akiifanya katika maisha ya watoto wako.** Wakia moja ya neno zuri la kutia shime ni bora kuliko ratili ya matengenezo. Tazamia ukuwaji na uwaaambie wanao unavyoona Bwana akitenda katika maisha yao. Unaweza usitambue hili litawatia moyo kiasi gani.

**12. Usijiondoe kupita kiasi.** Wanao wanapohitimu chuo au kufikia umri wa miaka 18, inawezekana kujiengua sana pale ambapo watoto wanafikia umri wa kufanya mabadiliko makubwa maishani (kazi, mwenzi wa maisha, n.k.). Baki ukiwa umeungana na watoto wako ambao sasa wanafikia utu uzima. Fahamu juu ya marafiki zao. Wahamasishe kukaa nyumbani hadi Mungu atakapowaongoza kufikia ndoa. Endelea kutoa miongozo na ushauri, ukitambua kuwa mahusiano yanabadilika wanao wanapofikia utu uzima. Baada ya umri wa kupevuka, tunapasa kubadili

majukumu yetu kutoka wenye mamlaka na badala yake kuwa walezi nwashauri wanaotumainiwa.

13. **Mshukuru Mungu kwa ajili ya watoto wako na waombee kila siku.**

**131. Ungemshauri mtoto wako nini ambaye amemaliza shule naye anaenda kujitegemea?**

Mpendwa Mwanangu Daudi. Sasa unamaliza shule, na hili linatuletea furaha na barka kwetu wazazi. Ni wachache wanamaliza shule ya sekondari na ni asilimia moja tu wanamaliza shahada ya.Kitu kikubwa katika maisha ni kujitambua wewe ni nani, uko hapa duniani kwaajili gani, na unakwenda wapi? Jiulize swali hili mara kwa mara! Mfano wake ni Mimi ni Daudi, Nipo hapa duniani kwa vile niliumbwa na Mungu ila mambo yaliharibika Edeni kwaajili ya dhambi na sasa ukarabati unaendelea ila Naenda mbinguni. Hii itakupa dira katika mambo ya maisha mengi ili usipoteze nafasi nzuri ya kufanya yale yatakayoleta tofauti.

Maisha na uwakili ni kitu kimoja! (Uwakili ni jinsi tunavyotumia maisha yetu)

Hebu YEYE Mweza akupe njozi, utume, usongo na nyenzo (vision, Mission, Passion and provision) unapoendelea kufanya kazi. Wachina wasema ukitaka kufanya tofauti kwa siku moja kula chakula kwenye hoteli nzuri. Ukitaka kufanya tofauti kwa mwezi mmoja oa/olewa (mfano mbaya). Ukitaka kufanya tofauti kwa mwaka mmoja panda bustani. Na ukitaka kufanya tofauti maishani 'panda mtu;' yaani saidia watoto kupata elimu, au peleka watoto shule. Utakuwa umemkwamua mtu.

Nilipofika Marekani zaidi ya miaka 26 iliyopita nilimwomba Mungu nikisema akinisaidia kupata kazi nitatoa asilimia fulani baada ya zaka, ya kufanya tofauti katika maisha ya watu nilio na undugu nao na wale ambao sina undugu nao. kwa vile niliona shida daima zinakuja, na pesa inaingia mikononi na kutoka, ila kama unaomba Mungu akuwezeshe kufanya hili baada ya miaka mingi italeta tofauti. Ni vyema unapoanza kazi kufanya hivi, maana sasa utakuwa na mshahara wa kila mwezi usipopanga mambo mengi yatakuja na yatafanya yale ya muhimu yasifanyike (Differentiate between the urgent and the important). Ndugu wengine wa upande wa baba na mama pia usiwasahau. Hata bibi, babu, baba wakubwa/wadogo, binamu au mama wakubwa/wadogo kutuma pesa au zawadi, hata ikiwa ni dola 30 kwa miezi sita, atakukumbuka na kukuombea. Angalial jinsi ya kuinua maisha yao. Ila sisemi wewe mwenyewe ujisahau, La! Panga mambo kama haya na nunua daftari uyaandike, na baada ya miaka mingi ukisoma utatabasamu mwenyewe.

Watoto wengi waliozaliwa hapa Marekani na kukua hawajui jamaa na huo ni umasikini wa aina fulani kwa vile hawawezi kufanya tofauti kwa jamaa. Wewe una bahati kwa vile unawajua wengi wa nyumbani. Hebu katika maisha yako uwakumbuke, si kwamba unawiwa ila kwaajili ya upendo kama jina lako linavyosema "aliyependwa" ili ubarikiwe na pia uwasaidie kimaisha. Albert Schweizer mmishonari alisema daima tukumbuke duniani hatuishi wenyewe bali tuna kaka na dada wakiwemo watu wa nchi hii wanaohitaji msaada wetu wa hali au hata mali yaani si waafrika peke yao wenye mahitaji. Naomba Mungu atakuonyesha kipaumbele.

Wachina wasema ukitaka kufanya tofauti kwa siku moja kula chakula kwenye hoteli nzuri. Ukitaka kufanya tofauti kwa mwezi mmoja oa/olewa (mfano mbaya). Ukitaka kufanya tofauti kwa mwaka mmoja panda bustani. Na ukitaka kufanya tofauti maishani 'panda mtu;' yaani saidia watu kupata elimu, au peleka watoto shule. Utakuwa umemkwamua mtu. Maisha ni vita kubwa, kila siku ina pambano lake, ila kumbuka kwamba katika njia zako zote umkiri naye atakuwezesha katika mapito yako yote. Mhubiri alikuwa akikumbuka ujana wake kwamba alijaribu kutafuta furaha katika vitu, wanyama, bustani, wake, chakula, na fahari zote alihitimisha kwa kusema "Mche Mungu na kumtukuza ndiyo jumla ya mambo yote". Akizungumzia mara 38 kwamba mengine ni kujilisha upepo chini ya jua. Mizania yake inahitaji hekima, hebu omba akupe hekima katika kila hatua.

Ukipata kitabu cha do Hard things na Harris or I kissed dating goodbye ni vitabu vizuri kwa young man, hata hivyo anza na messages to young people. Tofauti ya Daudi na Yusufu ni Yusufu alikimbia, na Daudi alikodoa macho, si anayekimbia ni mwoga ila shetani huwezi ukaanza kujadiliana naye. Kuna vitu vinavyofanya mtu wa Mungu aanguke navyo ni wanawake, mamlala, na pes. Kama kuna mtu anayefikiri hawezi kuangushwa basi atakuwa na hekima kuzidi sulemani, atakuwa na nguvu kuliko Samsoni au atakuwa anampenda Mungu kuliko Daudi.

Maisha yetu duniani tukizaliwa tunasema wacha ngoja niende shule nitakuwa na raha na kuridhika, kisha tunasema wacha nipate kibarua au nichume hela nitakuwa na raha, kisha wacha ngoja nioe/niolewe na kuwa na watoto nitakuwa na raha, kisha wacha nistaafu nitakuwa na raha, kisha wacha nipate wajukuu nitakuwa na raha, kisha wacha watoto wajitegemee basi nitakuwa na raha, mwishowe uzee unaingia na tunasema mimi sina raha na siku hizi mara magonjwa na udhaifu, kisha kuwategemea watu kunaingia. Bibi yangu mzaa mama mwaka wa 1969 alikuja kututembelea tukiwa Arusha, alikuwa na miaka 48, nilimwona ni mzee sana, nikasema bibi wewe ni mzee hivi. Alinijibu 'Grace nilitazama tu upande huu

nikigeuka nikajikuta ni mzee!, haikuchukua muda, hata wewe utazeeka na utashangaa miaka imeenda wapi! Mwombe Mungu uwe wakili mwema najua siku moja atakwambia "vyema mtumishi mwema ulikuwa mwaminifu kwa madogo, ingia katika raha yangu ya milele".

Vitu vya dunia vinapungua thamani, leo **nanunua kitu kipya na kesho huwa najiuliza**. "kwa nini nilipoteza pesa zangu na kitu **hiki** kibaya au kibovu, mbona hakivutii". Ila vile vya milele vinavyoleta tofauti hautasikitika.

Kumbuka mambo matano muhimu kwa kila binadamu

1. Mwamini Mungu, na ungama dhambi zako, na Mpende sana
2. Soma Neno la Mungu kila siku
3. Omba bila kukoma kila siku
4. Tafuta ushirika utakaokusaidia kukua na kuishi katika kweli
5. Waambie watu wengine kuhusu habari njema na hukumu inayoujia ulimwengu kwa uhakika
6. Ishi mtindo wa maisha unaoendana na Maandiko
7. Huduma za jamii, yatima, wajane, wazee, wapweke, masikini

Mungu anatupenda sana kuliko tunavyojipenda, naye anataka tukae naye milele kuliko shauku yetu ilivyo

ubarikiwe sana na angalia hatua hizi 7 katika maisha yako ya kila siku

Mama yako

**<u>Hatua saba za kuelekea kileleni:</u>**

Hatua ya 1:Amka masaa mawili au moja! kabla ya miadi yako ya kwanza au kabla ya kufika kazini. Wekeza masaa ya mwanzo kwa kusoma vitabu vya kiroho, Elimu na vya kutia hamasa. "Masaa ya kwanza ndio gurudumu la kuendesha siku" Unapoamka, jiongezee mwenyewe maarifa ya kiakili ili uwe na siku njema. Utakuwa na mtazamo sahihi, makini, mbunifu na mwenye tija kazini kwa siku yote kama utafanya hivi. Kama utawekeza katika fani yako saa moja tu kwa siku, hiyo itakuwa ni sawa na kusoma kitabu kimoja kwa juma, na vitabu hamsini kwa mwaka. Mtu mzima kwa kawaida anasoma kitabu kimoja kisicho cha hadithi kwa mwaka. Endapo unasoma kitabu kimoja kwa juma unafikiri utakuwa mkuu katika taaluma yako na kusonga mbele katika hekima dhidi ya watu wengine wote kwenye biashara yako? Ni hakika ndivyo itakavyokuwa! Hiyo itakuwa ni sawa na vitabu 500 kwa mwaka, utahitaji nyumba kubwa ya kuhifadhi vitabu vyako! Hii itakufanya uwe mtu

mwenye mamlaka katika taifa lako kuhusiana na taaluma yako kwa miaka mitatu hadi mitano.

Hatua ya 2: Andika tena malengo yako makuu kila siku katika daftari katika wakati uliopo kila asubuhi kabla ya kuondoka, bila kuangalia kile ulichoandika jana. Kitendo cha kuandika na kurudia ni cha kuunda kanuni ya uundwaji wa taarifa katika mfumo wa kuongoza akili yako. Unaporudia kuandika malengo kumi kila asubuhi unataendelea kuona na kufikiri juu ya fursa za kufikia malengo hayo hatimaye. Utakuwa makini, mwenye mwelekeo sahihi na usiyeyumbishwa, utakuwa mtu mwenye malengo na nia thabiti. Na utafanikiwa katika malengo yako kwa haraka zaidi kuliko kama yangekuwa ni mawazo tu yanayoelea katika akili yako.

Hatua ya 3: Kila siku weka mipango mapema. Andaa orodha na panga vipaumbele katika kazi yako kabla ya kuondoka nyumbani. Uwezo wako wa kuona vipaumbele na kuchagua kile ambacho ni cha muhimu zaidi ambacho utakuwa ukifanya kila wakati ni ufunguo wa kupangilia maisha yako na kuzidisha matokeo yake.

Hatua ya 4: Jenga nidhamu ya kushughulisha akili yako yote katika jambo MOJA. Chagua kitu ambacho ni cha muhimu kuliko vyote ambacho unaweza kufanya kila siku. Halafu anza nacho kwanza na kifanyie kazi mpaka kimekamilika kwa 100%. Uwezo wako wa kuwa makini na kufanya kazi, wakati unaendelea na na zoezi la kujijengea hiyo kuwa tabia, yenyewe, itakuwezesha kukuza uzalishaji wako, ufanisi, na matokeo mazuri katika mwezi unaofuata.

Hatua ya 5: Sikiliza vipindi vya kuelimisha katika gari lako: mfanyabiashara wa kawaida anayeendesha gari anatumia masaa 500 – 1000 kwa mwaka akiwa katika usukani wa gari. Unapogeuza gari lako kuwa jingo la chuo kikuu ama darasa la simu ya mkononi unapata elimu sawasawa na kuhudhuria mihula miwili ya masomo ya chuo kikuu wakati unapokuwa unaendesha gari. Watu wengi wamebadilika toka katika ufukara hadi kuwa matajiri kwa kusikiliza vipindi mbalimbali vya sauti kwenye magari yao.

Hatua 6: Uliza maswali mawili ya tafakuri kila baada ya kupiga simu, kuhudhuria sherehe au kukutana na mtu fulani: swali la kwanza ni "Je ni jambo gani nimefanya vyema?" swali la pili "ni kitu gani naweza kufanya tofauti?" Swali la kwanza linakulazimisha kufikiri kwa kina na kukumbuka mambo yote sahihi uliyoyafanya

*mara ya mwisho ulipokutana na mtu fulani, katika mkutano, ulipofanya uwasilishaji ama sherehe: hata kama haikufanikiwa. Swali la pili linakulazimisha kufikiri juu ya njia mbalimbali tofauti unazoweza kutumia kuongeza ufanisi katika mazingira yaleyale. Andika mawazo haya mahali fulani pia. Njia hii ndiyo ya haraka na zoezi la muhimu zaidi katika ukuaji binafsi na kuendelea kwa mtu.*

*Hatua ya 7: Mchukulie kila mtu unayekutana naye kama lulu ama thamani kubwa ya fedha: kote nyumbani na ofisini, unapotembelea watu nyumbani kwao na kila unayekutana naye. Unapowachukulia watu kuwa wa muhimu na wa thamani, watarejesha fadhila kwa kukuchukulia kama mtu wa thamani pia. Watatamani kuhusiana nawe, kufanya kazi nawe, na kununua vitu kutoka kwako na kukutambulisha kwa marafiki zao. Anza kwa watu wa nyumbani kwako unapoamka asubuhi, washukuru, kuwa na mtizamo sahihi utajikuta una amani na furaha siku nzima. 85% ya mafanikio yako yanategemea mahusiano yako na watu, usiwe mtu wa kukasirika kasirika.*

Contents

1.Sijatafuta title ya kitabu ila pengine: ............................................................................................1

2.–ALFABETI ZA MALEZI YA WATOTO au mzazi wa karne ya 21 au nini? Najaribu kutoa penye Yesu niweke Mungu iwe universal hata kwa waislamu.........................................................1

3.(The main thing, is to keep the main thing, the main thing).........................................................1

5.Eli alikuwa amekosa mawasiliano muda mrefu hakujua kinachoendelea. Alishakuwa mzee nno na kukosa kueleweka na watoto ambao ni kizazi tofauti. Alikuwa amepoteza mamlaka yake juu ya wanawe. Watoto wake walikuwa wameharibika sana kitabia kusaidika. .................................43

1.Mbingu na dunia ndiyo vitabu vya mtoto wa kiume, kabla hajaanza kujua kusoma au kuandika, kama Zaburi 19 inavyosema. Zaburi 144: 12-15 yasema, 'Wana wetu na wawe kama miche waliokua ujanani. Binti zetu kama nguzo za pembeni zilizonakishiwa kwa kupamba hekalu. Ghala zetu na zijae akiba za jinsi zote. Kondoo zetu na wazae elfu na makumi elfu, mashambani mwetu ngombe zetu na wachukue mizigo, kusiwe kushambuliwa. Wala kusiwe kuhamishwa. Wala malalamiko katika njia zetu. Heri watu wenye hali hiyo. Heri watu wenye Bwana kuwa Mungu wao.” ..............................................................................................................94

The Eagle does not fight the snake on the ground. It picks it up into the sky and changes the battle ground, and then it releases the snake into the sky.
The snake has no stamina, no power and no balance in the air. It is useless, weak and vulnerable unlike on the ground where it is powerful wise and deadly.
Take your fight into the spiritual realm by praying and when you are in the spiritual realm God takes over your battles.
Don't fight the enemy in his comfort zone, change the battle grounds like the Eagle and let God take charge through your earnest prayer. You'll be assured of clean victory.
Pray without ceasing. The Eagle does not fight the snake on the ground. It picks it up into the sky

and changes the battle ground, and then it releases the snake into the sky.
The snake has no stamina, no power and no balance in the air. It is useless, weak and vulnerable unlike on the ground where it is powerful wise and deadly.
Take your fight into the spiritual realm by praying and when you are in the spiritual realm God takes over your battles.
Don't fight the enemy in his comfort zone, change the battle grounds like the Eagle and let God take charge through your earnest prayer. You'll be assured of clean victory.

Pray without ceasing. ....................................................................................................132
Contents....................................................................................................132
7.ASSIGN 05
=========================================================== ..........................132
8.ASSIGN 06
=========================================================== ..........................133
9.ASSIGN 07
============================================================ ........................135
10.ASSIGN 09
==============================================================....................135
11.ASSIGN 10
=============================================================......................137
12.ASSIGN 11
============================================================== ..................137
13.
ASSIGN 12
================================================
KANUNI 12 ZA KULEA WATOTO ILI WAWE WATUKUTU.................................................138
14.

ASSIGN 13
==============================================================
2. KANUNI 11 KWA AJILI YA MARAFIKI ZA WATOTO WETU .........................................138
15.ASSIGN 14
==============================================================....................139
16.

==============================================================....................139
17.


==============================================================
2.0 KANUNI 11 KWA AJILI YA MARAFIKI YA WATOTO WETU ........................................140
18.ASSIGN 18
==============================================================....................140
C,INDEX ....................................................................................................144

Lisa Jacobson ........................................................................................................................144

C:\E:Mwalimu Marwa.docx

**5.BIBLIA NI RAMANI – *Biblia inasema, Ninaamini, na tatizo linaisha.***

Kitabu hiki kimebeba fikra ya Mungu, Hali ya mwanadamu, Njia ya wokovu, Hatima ya wadhambi, na furaha ya wenye haki. Mafundisho yake ni Matakatifu, kanuni zake zadumu milele, historia yake ni ya kweli na Suluhisho lake ni la kuaminika, Kisome upate hekima, kiamini ili uwe salama na kijaribu ili uwe Mtakatifu.

Kina nuru ya kukuongoza, chakula cha kukuwezesha, na faraja itakayokujaza furaha. Ni ramani kwa msafiri, Fimbo kwa mahujaji, dira ya rubani, upanga wa askari, na Mkataba kwa Mkristo. Hapa Paradiso hur.ejeshwa, Mbingu hufunuliwa, na milango ya kuzimu hufungwa. Kristo ndiye muhusika mkuu: Wema wetu, muundo wake, utukufu wa Mungu, na mwisho wake. Kitabu hiki hakina budi kujaza akili, kutawala moyo, na kuongoza mapito yetu.

Kisome taratibu, mara kwa mara na kwa maombi. Ni madini ya utajiri, paradiso ya utukufu na mto wa furaha. Kimetolewa kwako maishani, kitafunguliwa wakati wa hukumu, na daima kitakumbukwa milele. Kinatoa kiwango cha juu cha uwajibikaji, Kitatoa ujira kwa kila mtenda kazi bora na kitawahukumu wote waliochezea mambo matakatifu. Kamwe hakuna kitabu kingine kinachoinua akili na kuongeza uwezo wa kufikiri kama Biblia.

Iamini upate hekima, isome uwe salama, Ijaribu uwe mtakatifu.Biblia si kitabu cha kukupatia taarifa bali kitabu cha kukubadilisha. Ni Sauti ya Mungu ikizungumza, tena yenye Mamlaka kuu Mbinguni na Duniani. Bwana amelikuza Neno lake juu ya Jina lake. Mbingu na nchi zitapita lakini si Biblia. Biblia imeshinda kila aina ya changamoto za nyakati zote.

6.Shughuhuli nyingi ni adui MKUBWA WA MAOMBI.

"SHETANI ALIITISHA MKUTANO WA ULIMWENGU: Kuwa na shughuli nyingi Hii ni kanuni ambayo shetani anaipenda kuitumia.
Muovu daima yupo kwa ajili ya kutafuta, kuua na kuharibu. Anahitaji kupora amani yetu na kutajaza na maovu yote yasiyotokana na Mungu. Kadri ambavyo nilitafakari na kugundua katika amani yangu leo, nilikumbushwa jinsi ambavyo shetani hufanya kazi katika maisha ya watu wengi kwa kuwapatia shughuli nyingi na hivyo kuhamisha tafakari yao mbali na Mungu na kuwapeleka katika masuala mengine yasiyo na tija.

*Kadri unavyosoma habari hii, hebu na ikusaidie kwa kurejesha mawazo yako kwa mambo ya Kiroho na kuondoa macho yako katika mambo ya dunia hii ambayo kwanza si nyumbani kwetu na muda m,fupi ujao itapita isiwepo tena. Nakutakia Mibaraka na Amani ya Bwana wetu Yesu Kristo.*

Shetani aliitisha mkutano wa roho chafu (mapepo) ulimwenguni kote. Katika hotuba yake ya ufunguzi alisema,
"Mnajua kuwa hatuwezi kuwazuia wakristo wasiende kanisani"
"Hatuwezi kuwazuia wasisome Biblia na kuutambua ukweli"
Na wala kamwe hatuwezi kuwazuai wasiwe na mahusiano ya karibu na Mwokozi wao"
"Punde wanapopata muunganiko huo na Yesu, nguvu yetu ya kuwatawala inavunjika."
"Hivyo waache tu wahudhuria ibada makanisani mwao; waache wapate chakula kizuri kilichofunikwa, LAKINI tuhakikishe kuwa tunapora muda wao, ili kwamba wasipate muda wa kuunganika na Yesu Kristo."

"Hiki ndicho ninachowataka mfanye," Shetani akaawaagiza:

"Muwapumbaze kiasi kwamba wasimfikirie tena Mwokozi wao na kuwa na huo muunganiko wa muhimu kwa siku nzima!"

"Tutawezaje kufanikisha hili?" Mapepo yakauliza.

"Wapeni shughuli nyingi katika mambo yasiyo na umuhimu katika maisha na vumbueni program nyingi za kushika akili zao, mambo ambayo yatawafanya waone fahari kuyatenda, tamaa ya pesa, visasi, wivu, hasira, kutosamehe, na kila aina ya hila" Akajibu
"Wajaribuni katika matumizi, matumizi, matumizi na kukopa, kukopa, kukopa."

"Washawishini wanawake waliolewa kutafuta kazi za kuajiriwa na waume zao kufanya kazi kati ya siku 6-7 kwa juma, masaa 10-12 kwa siku, ili kwamba waweze kupata pesa ya kukidhi mfumo wao wa maisha uliojaa matumizi."
"Wafanye wasipate muda wa kutulia na watoto wao." Kadri familia zao zinavyoparaganyika, ndivyo na nyumba zao hazitaweza kuwaokoa na misongo ya kazini."

"Sisimueni akili zao kiasi kwamba wawe hawawezi kuisikia ile sauti ndogo nyembamba."
"Warubuni kusikiliza miziki ya kidunia, ama kutuma meseji zisizo na umuhimu, wakati wakiwa wanaendesha magari, ama wanapokuwa katika Ibada. Badala ya kufanya Ibada ya maombi wafanye washughulike na vifaa vya teknohama kama IPOD, IPhone, IPAD, CDs, TV n.k. Majumbani Makanisani na hakikisheni kuwa kila duka la kuuza CD na DvD na kwenye kila kumbi za starehe zimejaa program za kupiga miziki ya kidunia tu.

"Hili litajaza akili zao na kuvunja ule muunganiko na Kristo."
"Hakikisheni kwenye kila meza za kahawa mnaweka magazeti ya udaku na umbea"
"Shindilia kwenye akili zao taarifa zisizo na uhalisia kwa masaa 24 kwa siku"
"Wafanye waduae wakati wanaendesha magari yao kwa kuona mabango ya matangazo ya bidhaa yanavyobadilika badilika pembezoni mwa barabara."

"Gharikisheni barua pepe zao kwa jumbe za kitapeli, matangazo ya biashara, michezo ya bahati nasibu, na kila aina ya gazeti la kujaribu bahati, promosheni za kupata bidhaa, huduma za bure na matumaini ya uongo..."

“Wawekeni wasichana wembamba, warembo kwenye magazeti na TV ili kwamba waume zao waamini kuwa uzuri wa nje ndilo jambo la msingi na wao wataanza kutoridhika na wake zao”

“Wafanyeni wanawake walioolewa wakate tamaa na kuchoka kuendelea kuwapenda waume zao. Endapo hawataweza kuwajali waume zao vyema, wataanza kutafuta wanawake wengine mahali kwingine.”

“Hilo litaharibu familia zao kwa haraka!”
“Mleteni Father Chrismas mfanye awe mkarimu kwao ili kuwapumbaza wasiwafundishe watoto wao maana halisi ya Kuzaliwa kwa Kristo.”

“Kadhalika wafanyeni wafikiri juu ya vyakula na sherehe za siku za shukrani na Chrismas, ili kwamba wasiwe na muda wa kuomba kwa ajili ya roho mtakatifu kwa ajili ya wokovu wao na wa wengine.”

“Wapeni mkate wa Pasaka ili kwamba wasizungumze kuhusu UFUFUO Wake na Nguvu kushinda dhambi na mauti au Nguvu ya kuwawezesha KUJISALIMISHA kwa KRISTO kwa hali zote.”

“Hata katika maburudisho yao, yafanyeni yasiwe na maana. Wafanyeni wakitoka katika maburudisho hayo wawe wamepumbuaa na kuchoshwa zaidi, wafanyeni waendelee kutazama picha na kutafuta watu wa kusikiliza visa vya hadithi zao wenyewe.”

“Msiwape muda wa kwenda kutazama viumbe asili na kutafakari Uumbaji wa Mungu. Wapelekeni katika maeneo ya maburudisho, Michezo, Matamasha na kutazama movie”

“Wapeni shughuli, shughuli, shughuli! Na watakapokutana kwa ajili ya ushirika wa Kiroho, wafanye wapige umbea na vijembe ili watakapoondoka waondoke na dhamira zilizochafuliwa. Bila shaka hili litawafanya wasahau Dhima na Dhamira yao ya kutanganza Injili.”

“Punde watakuwa wakijitaabisha, kutoa kafara ya afya na familia zao kwa kujaribu, kuunganisha program nyingi pasipo kuhusianisha maombi. Kwa njia hii wataendelea kuwa na shughuli nyingi, bila kugundua tofauti ya kuwa Roho Mtakatifu hayupo katika wingi wa shughuli zao kwani KUTENDA na KUWA ni mambo mawili yasiyofanana.”

“Inawezekana!”
“Inawezekana!”
“Inawezekana!”

Ulikuwa mkakati mzuri!

Mapepo yaliondoka kwa shauku kutekeleza wajibu wao kuwafanya Wakristo mahali popote wawe watu wa shughuli nyingi, usiku na mchana wakitoka hapa na kuelekea kule., huku wakiwa na muda kidogo sana kwa ajili ya Mungu na familia zao.

Hawakupata kabisa muda wa kuwaambia wengine juu ya nguvu ya Kristo kubadili maisha yao, wala hawakuwa na muda wa kuhudhuria ibada kanisani.

*Nadhani swali kwa sasa laweza kuwa, je shetani ameweza kufanikiwa katika mkakati wake?* Je umewahi kusikia sauti nyingi zikikuelekeza kutimiza majukumu mengi na kwahiyo unaomba kidogo ambapo ulihitajika kutulia,kwa muda kiasi na ukaendelea kujenga mahusiano na Yesu? Hebu na uwe Hakimu!!!!

**"ACRONYM"**
**UFUPISHO WA NENO LA KIINGEREZA**
**"B.U.S.Y." is "B-eing U-nder S-atan's Y-oke"?**
**(Kuwa chini ya kongwa la Shetani?)**

7.**<u>Kwanini tuombe? MAOMBI NI JIBU</u>**

"Maombi ni jibu la kila tatizo maishani. Mara nyingi hatuombi kwa mazingira Fulani maishani, kwasababu kutoka sehemu tulipo, tunaonekana kupoteza tumaini, lakini hakuna jambo lisilowezekana kwa Mungu.

Hakuna jambo lililofungika kiasi kwamba haliwezi kupata tiba. Hakuna mahusiano ya wanadamu ambayo yameharibika kiasi kwamba Mungu hawezi kurejesha suluhu na maelewano.

Hakuna mazoea ambayo yamekita mizizi kiasi cha kushindikana kutibika.

Hakuna aliye mdhaifu kiasi kwamba hawezi kupata nguvu tena.

Hakuna aliye mgonjwa kiasi kwamba hawezi kutibiwa tena

Hakuna aliye mjinga kiasi kwamba hawezi kuwa na akili tena

Chochote tunachohitaji ama kustahili, kama tunamwamini Mungu, Atatupatia.

Kama kuna jambo lolote la kututia hofu na mashaka, hebu na tuache kuutazama ugumu wake na tumwamini Mungu kwa ajili ya uponyaji, Upendo na nguvu Herald OCT 7, 1865.

**Kama unahitaji kufanya jambo Fulani kwa ajili ya Mungu, unda kamati, na endapo unahitaji Mungu afanye jambo fulani kwa ajili yako omba…**

9.**Kanuni zinazohusiana na MAMLAKA katika familia yetu…**

1. Tunampenda na kumtii Bwana wetu, Mungu kwa unyenyekevu wa moyo wote
2. Tunasoma Biblia na kuomba kila jambo kwa Mungu kwa moyo mnyoofu
3. Tunawajali na kuwatii wazazi wetu katika Bwana bila kuonesha hali ya dharau

4. Tunakubali kukosolewa na kuonywa kwa moyo wa unyenyekevu.

**Kuhusiana na masuala ya MAHUSIANO katika familia yetu….**

5. Tunapendana, kwa kuchukuliana kwa huruma, utu na staha
6. Tunasaidiana, kwa upole tunatanguliza mahitaji ya wenzetu kabla ya mahitaji yetu.
7. Tunatiana moyo, kwa kutumia maneno yale tu yanayojenga tabia njema na kubariki wengine.
8. Tunasameheana, kwa kufunika kosa kwa upendo pale tunapokosea ama kuwakosea wengine.

**Kuhusiana na UMILIKI WA MALI katika familia yetu……**

9. Tunashukuru Mungu kwa kile tulicho nacho, kwamba kiwe kidogo ama kingi.
10. Tunaridhika kwa kile tulicho nacho, na sio kutamani vingine wengine walivyo navyo.
11. Tu wakarimu kwa vile tulivyo navyo, kwa kushiriki kwa uwazi na wengine.
12. Tunajali vile tulivyo navyo, kwa kuvitumia kwa busara na kwa umakini.

**Kuhusiana na KAZI katika familia yetu……**

13. Tunabidii kukamilisha kazi kwa uaminifu na kwa umakini tunapoombwa kufanya hivyo.
14. Tunachukua juhudi binafsi kufanya kazi zetu zote pasipo kuhitaji kuambiwa
15. Tunafanya kazi kwa roho ya ushirikiano, kwa uwazi tunatoa na kupokea msaada.
16. Tunafanya juhudi binafsi kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani yanadumu kuwa masafi muda wote.

**Kuhusiana na TABIA katika familia yetu…..**

17. Tunachagua kuwa na furaha, hata pale ambapo tunahhisi tulitakiwa kulalamika
18. Tunachagua kuwa wapatanishi, hata pale tunapojihisi kupisana kauli.

19. Tunaamua kuwa watulivu, hata pale tunapojihisi kama tunashindwa kutulia
20. Tunaamua kuwa wapole, hata kama tunahisi hatukutakiwa kuwa hivyo.

.

**Kuhusiana na CHAGUZI katika maisha yetu.....**

21. Tunafanya kile tunachojua kuwa ni sahihi, bila kujali wengine watasema nini.
22. Tunauliza kabla ya kutenda, pale ambapo hatujui nini sahihi cha kufanya
23. Tunajaribu kujizuia mar azote na kwa kila hali.
24. Daima tunasema ukweli na kamwe hatujaribu kusema uongo wa aina yeyote.

**10 JINSI YA KUTOKUWA NA FURAHA MAISHANI**

Jifikirie Mwenyewe
Jizungumzie mwenyewe muda wote
Tumia kiwakilishi "mimi" mara nyingi iwezekanavyo
Jipime muda wote kwa kutumia mawazo na maoni ya wengine
Sikiliza kwa shauku kuhusu kile wengine wanasema kukuhusu wewe
Kuwa na mashaka
Tarajia watu wakukubali
Kuwa na wivu na tamaa
Kasirika kwa kila anayekutukana
Kamwe usisahau kukosoa wengine
Usimwamini mtu yeyote isipokuwa wewe mwenyewe
Sisitiza watu wakukumbuke na kukuheshimu.
Lazimisha mawazo yako juu ya kila jambo yaheshimiwe.
Kasirika endapo watu hawakukumbuki na kukupa fadhila.
Usisahau huduma uliyowahi kutoa.
Daima tegemea nyakati njema kwa ajili yako.
Jaribu kukwepa majukumu yako kama utaweza.
Wajali watu wengine kwa kiwango kidogo sana kadri inavyowezekana.
Jipende mwenyewe kupita kiasi.
Kuwa mbinafsi.
Kanuni hizi zitakuhakikishia kutokuwa na furaha maishani.

**Njia nyepesi 11 za kujenga uhusiano na watoto wako.**

1. **Mchukue mtoto pamoja nawe kila mara unapokwenda mahali Fulani kwa gari**. Hii itakupa muda wa kuongea pamoja. Watoto wako watajifunza kutoka kwako wakati unaponunua, unapohudumu, unapoendesha, na watajifunza kutumika pamoja nawe.

2. **Fanya kazi pamoja**. Katika bustani, jikoni na nyumbani. Siyo tu kwamba hii itakupa muda zaidi wa kuongea na kuwafundisha watoto wako katika kazi unazozifanya, lakini pia itaokoa muda wako na kukuachia muda zaidi wa kuwa pamoja nao katika mambo mengine.

3. **Soma vitabu na kuangalia picha pamoja kama familia.** Hata mtoto mdogo kabisa anaweza kufurahia kuangalia picha za kitabuni na kukusikiliza unaposoma kwa sauti. Mbali na kuweka kumbukumbu za pamoja utakuza upendo wa wakujifunza na kujenga fursa kubwa za majadiliano, kuangalia na kujadili picha zinazofaa pamoja pia husaidia watoto wako kukuza stadi muhimu za kufikiri na utambuzi wa kiroho.

4. **Ongea nao – na usikilize!** Chukua muda unapowaingiza kitandani, na waulize siku ilivyoenda au wasimlie hadithi fupi. Wasikilize kwa uvumilivu wanapotaka kukuelezea jambo fulani. Anza hili mapema, na watoto wako wanaopenda kuongea nawe watakapopevuka bado watapenda kuongea nawe.

5. **Onyesha ukarimu na mjumuike pamoja kama familia.** Punguza muda ambao wanao wanautumia na wenzao wa rika moja, na tumieni muda zaidi pamoja kama familia, katika shughuli pamoja, katika kukaribisha familia nyingine nyumbani kwenu, na kuwakaribisha marafiki wa watoto wako nyumbani kwako.

6. **Tafuta miradi ya kufanya kama familia.** Kushiriki malengo ya pamoja mnapoendelea kufanya kazi na kutoa huduma pamoja vitaivuta familia yenu pamoja. Tafuta njia ya kutoa huduma pamoja kupitia kanisa lako, kuwahudumia waliozuiwa na mazingira au katika nyumba za wazee kwa pamoja, anzisheni biashara ndogondogo pamoja, iweni wenyeji wa matukio ya familia nyingine,

wasaidieni bibi na babu, anzisheni mifugo, pigeni chombo cha muziki pamoja! Imetolewa bure na Pam Forster, © Doorposts- www.doorposts.com

1. 12. KANUNI 12 ZA KULEA WATOTO ILI WAWE WATUKUTU

3.1 Anza tangu utotoni kumpa mtoto kila kitu akitakacho. Kwa njia hii atakuwa akiamini kuwa anapaswa kuishi duniani.

3.2 Anapojifunza maneno machafu mchekee. Hivyo atajidhania yu mwerevu.

3.3 Usimpe mafunzo yoyote ya kiroho. Subiri hadi awe na umri wa miaka 21 halafu mwache "ajiamlie mambo yake mwenyewe".

3.4 Epuka matumizi ya "hilo ni kosa", atajisikia hatia. Hili litamfanya aamini baadae kuwa, atakapotiwa mbaroni, jamii haimpendi na anateswa.

3.5 Okota kila kitu anachoacha ovyo. Mfanyie kila kitu ili azoee kuwatupia wengine kila wajibu.

3.6 Mtetee dhidi ya majirani, walimu na Polisi. Hao wote wanamchukia mwanao.

3.7 Gombaneni mara kwa mara mbele ya watoto wenu. Hivyo hawatastuka nyumba itakapovunjika baadae.

3.8 Mpatie mtoto fedha zote za matumizi anazotaka. Usimwache azalishe za kwake mwenyewe.

3.9 Timiza haja yake ya kila anachotamani, chakula,vinywaji na raha. Hakikisha kila jambo mwili wake unalotamani linapatikana.

3.10 Mwache asome kila kilichochapishwa, na asikilize kila wimbo ambao mikono yake itaufikia. Uwe mwangalifu kuhakikisha kuwa vyombo vya chakula na bilauri zote ni safi isipokuwa ubongo wake ulishwe takataka.

3.11 Anapokuwa ameingia matatani, jifariji kuwa "nisingeweza kumsaidia lolote".

3.12 Jiandae kwa maisha ya huzuni. Hakika utayapata.

Yametwaliwa kutoka jarida linaloitwa, *Kanuni 12 za kulea mtoto awe mtukutu* linalosambazwa na Houston Police.

## 2. KANUNI 11 KWA AJILI YA MARAFIKI ZA WATOTO WETU

2.1 Wazazi huamua lini, wapi na akina nani watoto wao wanaweza kucheza nao.

2.2 Marafiki hawaruhusiwi kwenda nyumbani kwao mtu yeyote, au kwenda popote, hapo wazazi wao wameruhusu kufanya hivyo.

2.3 Marafiki hawana budi kuheshimu sheria za nyumba za wenzao na viwango vyao wakati wote na mahali popote

.

2.4 Marafiki hawana budi kuwa wema kwa watu wote wa familia za wenzao.

2.5 Marafiki wanaweza tu kuchezea vitu vya michezo vya wenzao endapo wapo tayari kuviomba kwanza, kuwa waangalifu na kuvirudisha pale walipovitoa kabla hawajaondoka.

2.6 Marafiki wanaweza kugawa au kuazimishana vitu endapo tu wamepata idhini kwanza kufanya hivyo kutoka kwa wazazi wa wenzi wao.

2.7 Marafiki hawawezi kuondoana wasimalize kwa furaha shughuli za kifamilia pamoja na kazi za shule.

2.8 Marafiki wasisababishe wenzao kukosa huduma za kanisani au shughuli nyingine muhimu za kifamilia.

2.9 Wanafamilia ndio marafiki zetu walio muhimu zaidi. Hivyo kaka na dada hawana budi kuwa waaminifu kila mmoja kwa mwenziwe.

2.10 Watoto ambao wanasababisha au wanasema vitu vinavyosababisha wenzao wasiwe watiifu hawataruhusiwa kucheza pamoja tena hadi hapo watakapoomba msamaha kila mmoja kwa wazazi wa mwenzake.

2.11 Marafiki wanaweza kuingizwa na kuwa miongoni mwa shughuli maalum za wenzao endapo wameonyesha kuwa wanaweza kucheza pamoja vizuri katika matukio mengine.

na Greg na Josh Harris

**5.Tabia za mwanamke mkali anayeburuza wengine**

1. Husimama mwenyewe kama mamlaka binafsi. Utambulisho wake umejengeka katika mtizamo potofu ya kuwa maisha yake ni jukumu lake binafsi na uhuru wake ndilo jambo la thamani kubwa
2. Daima anavutwa na tamaa ya kutaka Zaidi, tamaa zake kamwe si rahisi kuzitosheleza
3. Hatambui kuwa kutokuwa na shukrani, majivuno, na mashaka ndio vichocheo vya maisha yake.
4. Huhamasika na vitu vilivyo na umuhimu kwake, anaishi na dhana ya ubinafsi
5. Anatamani kupendwa na kubembelezwa, lakini anaweza kuumia sana anapohisi kukataliwa
6. Anaingia kwenye magomvi mara kwa mara, akichanganya tabia ya ukatili na ushujaa
7. Ana shauku ya madaraka na hakuna mtu ama chochote cha kumzuia katika kufanikisha hilo
8. Anatumia uwezo wake kumnyanyasa mumewe na wengine, anaweza asijulikane kama mnyanyasaji ila kitendo chake cha ukosoaji, mtizamo hasi na uzungumzaji wa sauti kali ni kama tindikali
9. Ni mkali na si muwazi na huona fahari kufanya hivyo
10. Mara nyingi huingia katika migogoro na wengine
11. Anaweza kudai kuwa Neno la Mungu ndiyo mamlaka yake kuu, lakini kusoma kwake ni kama kitabu cha kitaaluma, haimsaidii kurekebisha mahusiano yake na wenzake.
12. Mara nyingi haoni shida kuzozana, lakini nia yake ni kwa ajili ya manufaa binafsi ama faraja na mwenendo wake waweza kuwa wenye kudharau wengine.

Hutembea kwa kiburi na jeuri lakini ni kipofu kwa kukosa unyenyekevu. Anaona tabia ya unyenyekevu kama ishara ya udhaifu. Anaamini kwa dhati kuwa tabia

ya kutofautiana na wenzake inatokana na wao kuwa na uwezo mdogo, kutokuwa watu wa kiroho, ama tabia ya kutojiamini.

13. Anataka kuwa mtawala wa wengine na amefanikiwa kukuza uwezo wa kuwa juu yaw engine kwa kutumia hila na mbinu za ujanja ujanja
14. Hata kama hawezi kukubali, maisha yake yamejengeka katika ubinafsi. Anaridhika tu pale anapopata mambo yanayomhusu;

**Hatua saba za kuelekea kileleni:**

**Hizi ni hatua saba katika kanuni ya asilimia 1.000 ambazo zitakushangaza endapo utazifanyia mazoezi kama mzazi**

Hatua ya 1:Amka masaa mawili kabla ya miadi yako ya kwanza au kabla ya kufika kazini. Wekeza masaa ya mwanzo kwa kusoma vitabu vya kiroho, Elimu na vya kutia hamasa. "Masaa ya kwanza ndio gurudumu la kuendesha siku" Unapoamka, jiongezee mwenyewe maarifa ya kiakili ili uwe na siku njema. Utakuwa na mtazamo sahihi, makini, mbunifu na mwenye tija kazini kwa siku yote kama utafanya hivi. Kama utawekeza katika fani yako saa moja tu kwa siku, hiyo itakuwa ni sawa na kusoma kitabu kimoja kwa juma, na vitabu hamsini kwa mwaka. Mtu mzima kwa kawaida anasoma kitabu kimoja kisicho cha hadithi kwa mwaka. Endapo unasoma kitabu kimoja kwa juma unafikiri utakuwa mkuu katika taaluma yako na kusonga mbele katika hekima dhidi ya watu wengine wote kwenye biashara yako? Ni hakika ndivyo itakavyokuwa! Hiyo itakuwa ni sawa na vitabu 500 kwa mwaka, utahitaji nyumba kubwa ya kuhifadhi vitabu vyako! Hii itakufanya uwe mtu mwenye mamlaka katika taifa lako kuhusiana na taaluma yako kwa miaka mitatu hadi mitano.

Hatua ya 2: Andika tena malengo yako makuu kila siku katika daftari katika wakati uliopo kila asubuhi kabla ya kuondoka, bila kuangalia kile ulichoandika jana. Kitendo cha kuandika na kurudia ni cha kuunda kanuni ya uundwaji wa taarifa katika mfumo wa kuongoza akili yako. Unaporudia kuandika malengo kumi kila asubuhi unataendelea kuona na kufikiri juu ya fursa za kufikia malengo hayo hatimaye. Utakuwa makini, mwenye mwelekeo sahihi na usiyeyumbishwa, utakuwa mtu

mwenye malengo na nia thabiti. Na utafanikiwa katika malengo yako kwa haraka zaidi kuliko kama yangekuwa ni mawazo tu yanayoelea katika akili yako.

Hatua ya 3: Kila siku weka mipango mapema. Andaa orodha na panga vipaumbele katika kazi yako kabla ya kuondoka nyumbani. Uwezo wako wa kuona vipaumbele na kuchagua kile ambacho ni cha muhimu zaidi ambacho utakuwa ukifanya kila wakati ni ufunguo wa kupangilia maisha yako na kuzidisha matokeo yake.

Hatua ya 4: Jenga nidhamu ya kushughulisha akili yako yote katika jambo MOJA. Chagua kitu ambacho ni cha muhimu kuliko vyote ambacho unaweza kufanya kila siku. Halafu anza nacho kwanza na kifanyie kazi mpaka kimekamilika kwa 100%. Uwezo wako wa kuwa makini na kufanya kazi, wakati unaendelea na na zoezi la kujijengea hiyo kuwa tabia, yenyewe, itakuwezesha kukuza uzalishaji wako, ufanisi, na matokeo mazuri katika mwezi unaofuata.

Hatua ya 5: Sikiliza vipindi vya kuelimisha katika gari lako: mfanyabiashara wa kawaida anayeendesha gari anatumia masaa 500 – 1000 kwa mwaka akiwa katika usukani wa gari. Unapogeuza gari lako kuwa jingo la chuo kikuu ama darasa la simu ya mkononi unapata elimu sawasawa na kuhudhuria mihula miwili ya masomo ya chuo kikuu wakati unapokuwa unaendesha gari. Watu wengi wamebadilika toka katika ufukara hadi kuwa matajiri kwa kusikiliza vipindi mbalimbali vya sauti kwenye magari yao.

Hatua 6: Uliza maswali mawili ya tafakuri kila baada ya kupiga simu, kuhudhuria sherehe au kukutana na mtu fulani: swali la kwanza ni "Je ni jambo gani nimefanya vyema?" swali la pili "ni kitu gani naweza kufanya tofauti?" Swali la kwanza linakulazimisha kufikiri kwa kina na kukumbuka mambo yote sahihi uliyoyafanya mara ya mwisho ulipokutana na mtu fulani, katika mkutano, ulipofanya uwasilishaji ama sherehe: hata kama haikufanikiwa. Swali la pili linakulazimisha kufikiri juu ya njia mbalimbali tofauti unazoweza kutumia kuongeza ufanisi katika mazingira yaleyale. Andika mawazo haya mahali fulani pia. Njia hii ndiyo ya haraka na zoezi la muhimu zaidi katika ukuaji binafsi na kuendelea kwa mtu.

Hatua ya 7: Mchukulie kila mtu unayekutana naye kama lulu ama thamani kubwa ya fedha: kote nyumbani na ofisini, unapotembelea watu nyumbani kwao na kila unayekutana naye. Unapowachukulia watu kuwa wa muhimu na wa thamani,

watarejesha fadhila kwa kukuchukulia kama mtu wa thamani pia. Watatamani kuhusiana nawe, kufanya kazi nawe, na kununua vitu kutoka kwako na kukutambulisha kwa marafiki zao. Anza kwa watu wa nyumbani kwako unapoamka asubuhi, washukuru, kuwa na mtizamo sahihi utajikuta una amani na furaha siku nzima. 85% ya mafanikio yako yanategemea mahusiano yako na watu, usiwe mtu wa kukasirika kasirika.

te:

**Ubongo wako ulivyoumbwa yapasa uyafanye haya.**

1. Fikiria kama ambavyo mazoezi ya viungo humsaidia yeye afanyae, ndivyo nawe inavyokuwa unapoizoesha sehemu ya mbele ya ubongo wako kufikiri, uwezo wako wa kufikiri unaongezeka.

2. Kuwa mtu anayependa ukweli, kuwa na shauku nao, tunashindwa kuufikia ukweli kwa sababu Mungu hana ukomo, Naye huudhihirisha upendo wake kwetu kila siku ( Maandiko, Sayansi na uzoefu)

a. Jifunze na ufurahie Amri za Mungu na kanuni zake. Sheria ya Upendo, Sheria ya uhuru.

3. zithibitishe nadharia zote kuhusu Mungu kwa kutumia maandiko

4. kwa kulingana na ushahidi wa tabia ya Mungu Uaminifu wa kiwango cha juu na tabia ya upendo, jisalimishe kwake. Anza kila siku kwa kumualika Roho wake.

5. tafakari kila siku kuhusiana na tabia ya Mungu ya upendo na ufahamu, Ukweli uliojazwa na shukrani, na tafakari juu ya Mungu na ufalme wake wa upendo na kazi ya uumbaji.

6. Mwamini Mungu katika maisha yako, siku za usoni na matokeo yake baada ya kuelewa uaminifu wake na kupitia uzoefu wake.

7. Fanya mazoezi ya kanuni za Mungu. Ishi bila choyo, kwa kuwapatia wengine, jitolee na tafuta kuwashirikisha wengine kile Mungu alichokupa. Kadri unavyotoa ndivyo utakavyopokea.

8. Tafuta namna ya kushiriki ukweli kuhusiana na ufalme wa Mungu na upendo kwa wengine, jiunge na taasisi zinazojishughulisha na kudhihirisha upendo wa Mungu ulimwenguni. Anzisha huduma, ongoza masomo ya biblia, shirikiana na waumini mlio na mtizamo sawa wa kiimani. Ushirika hukuza uwezo na maarifa, hudhihirisha upendo wa Mungu katika kuponya na kuhuisha.
9. Ishi kwa kulingana na mpango wa Mungu wa maisha ya kimwili. Jiepushe na sumu zinazoweza kudhuru mwili na roho kama vile, tumbaku, pombe, madawa ya kulevya, viburudisho, michezo ya kupigana, kusoma vitabu vya kidunia, ama mambo yanayohafifisha tabia ya Mungu.

10. Fanya mazoezi ya mara kwa mara ya viungo na ukuaji wa mishipa ya fahamu, pamoja na chembechembe za kusawilisha kiwango cha hasira.
11. Pata muda wa kutosha wa kupumzika, kunywa maji, vuta hewa, kula vizuri na kulala ili kwamba ubongo wako usije ukaathirika katika uwezo wake wa kufanya kazi.
12. Ishi kwa kulingana na kanunu ya Mungu ya Asili. Kula vyakula vyenye afya, hakikisha unatoa uchafu mwilini, pata mwanga wa jua, utapunguza magonjwa mengi.
13. Samehe: usishikilie jambo kifuani, Kutunza hasira kifuani kunakufanya kuwa mtu wa hofu na mashaka na hatimaye hupunguza Amani na afya kwako

14. Usiwe na hatia: inapunguza Amani, na kuongeza mashaka, na inawathiri wengine wasio na hatia, ungama dhambi zako na endelea na maisha.
15. Kama hofu na mashaka imekujaribu ili kutenda kinyume na dhamiri yako ili kwamba upate ukubali wa wenzio, kumbuka kujiweka pembeni na kujiuliza.

a. Ukweli ni nini? Kipi ni sahihi? Kipi kina afya? Na kipi kinastahili? Je nifanyeje?
b. Jiulize mwenyewe endapo mtu fulani amekukataa ama amekukasirikia kwa kufanya kile unachoamini kuwa ni sahihi je huyu aweza kweli kuwa ni rafiki yako, je unahitaji ukubali wao?
c. Kuwa tayari kuwaweka watu wengine huru kufikiri ama kuhisi kadri watakavyo kuhusiana na wewe. Endapo unafikiri "kama nikifanya kile wanachohitaji, basi hawatanikasirikia". Basi jaribu kuwaacha huru wafikiri kadiri wanavyochagua kufikiri juu yako na utakuwa huru kutokana na misongo ya kutaka kuridhisha matakwa yao.
d. Kumbuka upendo hufanya kile kilicho sahihi kiafya na kimantiki, kwakuwa ndivyo, si kwakuwa inasikika vizuri wakati huo. Tazama ng'ambo na utumie kanuni hizi za Mungu hata kama zinaonekana kuwa ngumu kwa wakati huo.
e. Daima MTAZAME YESU, ishi kwa ujasiri katika uzuri wa MUNGU, ukijua ukweli wa SHERIA YAKE ya upendo, mpango wa maisha, kwa moyo wako wote itazamie siku ya YA MAREJEO YAKE.

**Sheria 21 za nyumba yetu**

*by Gregg Harris*

1. We obey God.
Tunamcha, Tunampenda na kumtii Mungu
2. We love, honor and pray for one another.
Tunapendana, tunaheshimiana, na tunaombeana
3. We tell the truth.
Tunasema kweli bila kuleta ulaghai
4. We consider one another's interests ahead of our own.
Tunatanguliza mbele maitaji ya wenzetu kisha yetu
5. We speak quietly and respectfully with one another.
Tunazungumza zizokuwa za kufoka, na kwa heshima
6. We do not hurt one another with unkind words or deeds.
Hatuumizani na maneno makali
7. When someone needs correction, we correct him in love.
Pale mtu anapohitaji masahihisho, tunamsahisha kwa upendo
8. When someone is sorry, we forgive him.
Akiomba msamaha tunamsamehe
9. When someone is sad, we comfort him.
Mwenzetu akiwa na huzuni tunamfariji
10. When someone is happy, we rejoice with him.
Mwenzetu akiwa na furaha, tunafurahi naye
11. When we have something nice to share, we share it.
Tukiwa na kitu cha kushiriki pamoja tunashirikiana
12. When we have work to do, we do it without complaining.
Tukiwa na kazi ya kufanya, tunafanya bila malalamiko
13. We take good care of everything that God has given us.
Tunatunza alivyotupa Mungu kwa uwakili aliotuusia
14. We do not create unnecessary work for others.
Hatufanyi kazi ya wengine kuwa ngumu
15. When we open something, we close it.

Tukifungua kitu tunakifunga tena (e.g begi, bomba)

16. When we take something out, we put it away.

Tukitoa kitu nje tunakirudisha tulipokikuta

17. We read the Bible and pray every day

Tunasoma Neno la Mungu, tunaomba kwa moyo ulio tayari kujifunza na kutenda hata yaliyo mapya

18. When we make a mess, we clean it up.

Tukichafua mahali, tunasafisha vizuri

19. When we do not know what to do, we ask.

Tusipojua la kufanya kitu tunauliza

20. When we go out, we act just as if we were in this house.

Kanuni za familia yetu

Sally Clarkson

**Kuhusu mamlaka ya nyumba yetu**

.

Tunampenda na kumtii Mungu, kwa mioyo yetu yote

Tunasoma Neno la Mungu na kuomba kila siku na moyo mkunjufu

Tunawaheshimu na kuwatii wazazi wetu na ari njema

Tunasikiliza mausia na kukubali adhabu kwa roho ya unyenyekevu

**Kuhusu mahusiano kwenye familia yetu**

Tunapendana na kuchuliana kwa wema, upole na adhabu

Tunahudumiana kwa unyenyekevu, tukifikiria mahitaji ya mwenzetu kwanza

Tunatiana moyo, kwa kutumia maneno ya kujenga na kubariki.

Tunasameheana, na kuyasahau hayo kwa upendo hata pale tulipoumizwa na kukwazwa

**Kuhusu umilikaji wa familia yetu**

Tunamshkuru Mungu kwa vyote tulivyonavyo, vidogo au vikubwa

Tunaridhika na tulivyonavyo, hatutamani walivyonavyo wengine

11. We are generous with what we have, sharing freely with others.

Tu wakarimu kwa tulivyanavyo, tunashirikiana na wengine kwa moyo mkunjufu.Tunasaidiana kwa tulivyo navyo, tukivitumia kwa hekima na kuwajibika

**Kuhusu Kazi katika familia yetu**

Tunanuia kumaliza kazi tuliyopewa kwa uaminifu na kwa muda wake.

Tunanuia kumaliza kazi tuliyopewa, bila ya kukumbushwa kumbushwa

Tunafanya kazi kwa moyo mkunjufu, tunasaidiwa na kusaidia wengine bila kinyongo

Tunachukua jukumu la kuweka nyumba yetu nadhifu na safi wakati wote

**Kuhusu mtazamo wa familia yetu**

Tunachagua kuwa wacheshi, hata pale tunapojaribiwa kunung'unika

Tunachagua kuwa wapatanishi, hata tupatapo majaribu ya kubishana bishana

Tunachagua kuwa wavumilivu, kinyume cha nia zetu

Tunachagua kuwa watu wa shukrani, kinyume cha vishawishi vya kibinadamu

**Kuhusu uchaguzi wa familia yetu**

Tunafanya yale ambayo yanapasa haki, hata wengine wakitushawishi mengine

Tunauliza kabla ya kutenda, pale ambapo hatujui lile jema kulifanya

Tunatawala nafsi kwa hali na mali wakati wote

Tunasema kweli daima, na tunaepuka ulaghai wa aina yoyote

Tukienda popote kwa wengine, tunafanya haya 21 mema kama vile tu tupo kwetu

Tukikiuka au kusahau sheria 21 za Nyumba hii, tunakubali hatua za nidhamu na maagizo toka kwa Mungu

Kuweka kwenye index za nyuma

*Lisa Jacobson*

Njia za kumwandaa mvulana awe Mwanamume bora

1. **Mche Mungu ndiyo chanzo cha hekima.** Mithali 1:7
2. **Sikiliza kwa makini.** Mwanamume mwenye hekima husikiliza na kujifunza mengi, Mithali 1:5
3. **Tilia maanani maagizo ya baba yako.** Utafurahi kwa hilo. Mithali 1:8
4. **Usiyasahau mafundisho ya mama yako.** Ana hekima kwako. Mithali 1:8
5. **Tawala hasira.** Yeye anayetawala hasira ni bora kuliko shujaa, ni zaidi ya anayeteka mji. Mithali 16:32
6. **Tunza ahadi zako.** Mwanamume anasema na kufanya aliyosema.
7. **Usishikamane na wale wasiomjali Mungu.** Wwatu waovu wanaharibu tabia njema 1 Kor 15:33
8. **Wekeza kwenye urafiki mzuri na bora.** Marafiki ambao ni msaada zaidi ya ndugu wa damu. Mithali 18:24
9. **Fanya yanayohitajika bila kuambiwa.** Usingoje kuambiwa wakati unajua unachopaswa kufanya.
10. **Uwe mtanashati.** Usivae ovyo, uonekana nadhifu na msafi.
11. **Mtegemee Mungu, na siyo akili zako.** Mithali 3:3-5
12. **Usipuuzie masahihisho.** Chukulia kama nafasi ya kujifunza na kukua. Mitahli 3:11
13. **Julikana kama Mfanyakazi bora.** Jifunze kufurahi kazi yako na fanya lolote jema linalotakiwa kulifanya.
14.
15. **Uwe na usafi moyo, mawazo na matendo . Kuna nguvu kwenye usafi**
16. **Uwe mwungana.** Uungwana ni kipimo cha mwanamume kama vile ujasiri ulivyo.
17. **Fanya mazoezi, usijiachie mwili wako utepete tepete.** Kijana anapashwa kuwa na nguvu, na aliye tayari kufanya yanayobidi kufanywa/

18.**Uwe wakili wa wa watoto na wanyonge kwako.** Usiwe mtu wa juu sana kwa walio chini.

19.**Hudumu kwa unyenyekevu kama Mwanamume bora.** Usiache mtu akutoe kwenye ubora, Fuata mfano wa Mungu kwenye Wafilipi 2

20.**Wasaidie wanawake/wadada.** Wafungulie mlango, wapishe kiti, wasaidie kubeba mizigo. Walinde na kuwatetea,

21.**Jitoe kujifunza masomo mengi unavyoweza.** Soma vitabu, fanya utafiti, chunguza na uliza maswali.

22.**Wape heshima wale waliokuzidi umri.** Wasalimu kwa salaam zinazotakiwa, wape mkono, na sikiliza yale wanayosema.

23.**Kimbia dhambi, Toroka mara kwa haraka kama Yusufu unapokumbana na majaribu.** 1Tim 6:11

24..

25.**Uwe jasiri kama simba.** Mtu mwenye haki hana haja ya kuona aibu kuhusu yale yasiyo ya haki. Mithali 28:1.

26.**Mpende Mungu sana na Neno lake.** Amebarikiwa mwanamume ambaye anafurahia sheria ya BWANA. Zaburi 1

a. **Njia za kumtayarisha msichana awe bora**
b. **Lisa jacobson**

.

1. **uwe mpole na maneno, hata matendo yako.** HEbu uzuri wako uonekana kwa upole wako na roho iliyotulia. 1 Petro 3).
2. **Uwe jasiri.** Kama mwanamke utakabiliana na mambo ambayo yatahitaji uwe imara na mwenye akili bora zilizotulia. Mithali 31:25
3. **Ishi maisha ya usafi wa moyo, mawazo na matendo.** Kuna uzuri wa kuishi maisha safi.
4. **Chagua furaha.** Utabariki wote wanaokuzunguka na uso wenye ucheshi. Isitoshe ndiyo njia nzuri ya kuishi

5. **Chagua furaha.** Utabariki wale wanaokuzunguka na uso wenye ucheshi. Isitoshe ndiyo njia bora ya kuishi.

6. **Itafute hekima.** Hekima ya kweli yatoka mbinguni tu. Yakobo 3

7. **Uwe huru kucheka.** Itakufanya uburudike na wale waliokuzunguka utaondoa kiwingu kwao.

8. **Shugulikia afya yako. Hakikisha unakula vyakula bora, unafanya mazoezi, na kupata wasaa wa kupumzika. Jitunze vizuri, ndivyo utakavyoweza kusaidia wengine pia.**

9. **Zungumza maneno ya matamu.** Watu wataweza kukuzikiliza ukifanya vile, kuliko kuwasuta na kuwakosoa kosoa.

10. **Uwe tayari kufanya kazi kwa bidii.** Jifunze kufurahia kazi, na kushugulikia lolote linalobidi kufanya.

11. **Imba kwa sauti.** Nyimbo za kumtukuza Mungu hubadilisha mtazamo (mood) humpa Mungu utukufu, HEbu imba kwa sauti kubwa! Zaburi 98:4.

12. **Soma mambo mbali mbali.** Amua kuwa mwanafunzi wa kudumu. Jifunze yanayohusu bustani, Historia, kuoka mikate, lugha mpya, tiba mbadala, jiografia, na mengine mazuri yanayokupendeza moyo

13. **Angalia wale wenye mahitaji.** Uwe na huruma kwa wengine, na tumia talanta zako kuwabariki

14. **Leta uzuri katika maisha yako nay a wengine.** Iwe ni maua, usanii, mashairi, kazi za mikono, au rangi zinazovutia

15. **Tembea kwenye matatizo na changamoto ukiishika imani.** Usitembee kwa nguvu zako mwenyewe bali mtumaini BWANA MWEZA naye atakubeba

16. **Vaa kwa adabu, Utapendenza na utafurahia 1 Tim 2:**9

17. **Wekeza kupata marafiki wazuri.** Chukua muda kupata marafiki wema watakaokutia moyo, kuhuisha na kukupa changamoto kukubariki

18. **Tayarisha vyakula vitamu vitamu.** Wabariki wanaokuzunguka na talanta zako za upishi.

19. **Tumia muda ukiwa peke yako kusoma Neno la Mungu na kulitafkari .** Kamwe usiwe mwenye shuguli nyingi wakati wa Muda wako na Mungu

20. **Uwe mwema kwa wengine.** Wema sio ghali kutenda, ila unaleta mvuto mkubwa kwa wale wanaokuzunguka. Mithali 31:26

21. **Serve cheerfully.** Look to Christ as your example, not what the world says about service. Nothing begrudging or stingy there (Phil. 2).

22. **Hudumu kwa ucheshi.** Mwangalie Kristo mfano wetu, na siyo dunia inavyohudumu watu. Usiwe mlalamika au bahili. Wafilipi 2

23. **Ombea mambo yote.** Usitatue mambo mwenyewe, nenda kwa BABA yako wa mbinguni na furaha zako, huzuni zako na shida zako. Efeso 6:18.

24. **Chunga unayosema.** Maneno au ulimi una nguvu kujenga au kubomoa, hivyo yatumie vizuri

25. **Wapende watu saana.** 1 Wakorintho 13

**Vitabu, CD au DVD zilizotumika kununukuliwa au kupata mawazo**

1. Misingi ya huduma ya mtoto. Learn and Share publishers. Arusha Tanzania. Dr Emmanuel Mbennah, 2008

2. How to Have Kids With Characters Even if Your Kids are Characters by Nadine Brown . Tyndale House Publishers in, Wheaton, Illinois. USA, 1990.

3. It is Your Money Isn't It?. Practical Money Management for Christians. Review and Herald. 1993. Edward Reid. Hagerstown M.D.

4. Morris. The Blessed life. DVD

5. Successful Parenting. Ann and John Murphy. St Pauls Edition. 1983. Boston MA, USA.

6. Parenting Your Child by the Spirit. By Sally hohnberger. Pacific Press Publishing Association, Nampa Idaho, USA. 2005

7. Uponyaji wa Mungu. By Dr Ann Mc Neilus and Moses Mwalumbili. African Herald Publishing House. Kendu Bay , Kenya.

8. Balanced Living by Vicki Griffin. Balancedlivingliterature.com

9. You Never stop being a parent: The Myth of Empty Nest . Helen Hosier.

10. Biblia takatifu. The Bible Societies of Tanzania. Dodoma 1994.

11. Adult children. The secrets of Dysfunctional families, John and Linda Friel. Health Communication Inc, Deerfield beach. Fla, USA. 1988

12. Ministry of healing. Pacific Press. Idaho, USA. Ellen G White.

13 Child Guidance. Pacific Press. USA. Ellen G White

14. Nusuru Ndoa Yako. Pastor David makoye, Morogoro Tanzania.

15 The Medical Missionary. Harvestime books.2004

16. Bringing up Your Child. A Homegrown Perspective. Jane Kaibiria. 2009. Aura creations. Nairobi Kenya

17. Dr James Dobson. Answers your Questions About Raising Children. And Parenting is not for Cowards. 1974. Tyndale House. Wheaton IL, USA.

18. Successful Parenting. Ann and John Murphy. St Paul.1983. Boston Ma.

19. Huduma ya Doorpost.org. USA

20.Mr and Mrs Nyantika. Raising Children for eternity, Kenya.

2. Dr Lehman. Have a New Child by Friday. USA

3. Changing the Heart of a Rebel , Freedom From Anger, Dating and what to Expect when a Child is 12 years old by Dr Davis. Solvefamilyproblems.com USA

23 Visit these websites for more: Revivingourhearts.org, fly.com (finallyloveyourself), onewithoutwords, doorpost.org, 21rules in this house, Breakingsilencenow.org, aboverubies.

24 On line Bible school (www.bibleschools.com/1416)

25 James Dobson. Preparing for Adolescence. Straight talk to teens and Parents. Regal books, Ca, USA

26 Dorothy Moore. Home grown Kids CD.

27 Anger. Dr Davis. CD.

28. Difference between Dating and Courtship. Dr Davis

29 Websites : Reviveourhearts.com, aboverubies.com, amazingdiscoveries, fly.com, doorpost.org